# Nipashe

Ijumaa Septemba 4, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580328
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



Nipashe Jumapili
Wavuvi 24 wajitosa ziwani kwa hofu ya kupigwa risasi
Maswali magumu 35 kupatikana MO Dewji

**Nipashe Jumapili linarudi tena mtaani**

Usikose nakala yako ya Nipashe Jumapili hii kwa habari motomoto za kisiasa, kijamii, burudani na safu maarufu ya 'Maisha ndivyo yalivyo' 'Madongo ya Mgagagigikoko' na 'Fikra mbadala'. Watoto nao hawakuachwa nyuma, bila kusahau mapishi, michezo, hadithi, mitindo, katuni na muziki wa enzi zilee...



## Membe atamba kumaliza tatizo la ajira na korosho

UKURASA 2



# Magufuli awaahidi neema wakulima, wafugaji

UKURASA 2

## Mwandishi ITV afariki ghafla Dar

UKURASA 7

MAHOJIANO MAALUM

## Lissu aanika sababu nne kuwania urais



• **Afafanua** tuhuma kutumiwa na mabeberu... *Endelea uk. 3*



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play
App Store

**Fursa kwa Wagombea! 2020**

Gazeti la Nipashe linawapongeza wateule wote waliopitishwa na vyama vyao kugombea ubunge katika majimbo mbalimbali nchini
Je ungependa kukishukuru chama chako ?
Je ungependa kutangaza sera zako kwa wapiga kura ?
Nipashe inatoa nafasi kutangaza sera zako kwa gharama nafuu

Nipashe
Wasiliana nasi
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz
VOTE

# Membe atamba kumaliza tatizo la ajira, korosho

**Na Enock Charles**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya ACT-Wazalendo, Bernard Membe, ameahidi kuajiri wanataaluma waliosomea ualimu katika shule za msingi na sekondari ili kukidhi mahitaji ya wanafunzi shuleni.

Akizungumza katika kijiji cha Ikwiriri wilayani Rufiji, mkoani Pwani, Membe amesema pamoja ni vijana kulalamikia ajira, lakini yapo maeneo yenye uhitaji wa watu kuajiriwa, na kwamba hawajaajiriwa, hivyo atakapochaguliwa na kuingia madarakani, atahakikisha vijana wanaajiriwa.

"Ni lazima kuajiri vijana, shule hazina walimu, lakini wapo waliosoma na hawajaajiriwa," alisema Membe alipokuwa anajinadi kwa wananchi kuomba kura.

**KUTENGA MAENEO YA WAKULIMA, WAFUGAJI**

Pia Membe ameahidi kutenga maeneo ya wakulima na wafugaji ili kuondoa migogoro ya mara kwa mara inayoibuka kati ya makundi hayo.

**KUTAFUTA MASOKO YA MAZAO**

Kadhalika, ameahidi kuunda wizara ya biashara itakayoshughulikia utafutaji masoko nje ya nchi kwa ajili ya mazao ya wakulima, kitu ambcho alisema kwa sasa hakifanyiki, wakulima kukosa masoko ya mazao yao.

Akizungumzia masoko ya zao la korosho, Membe alisema atahakikisha wakulima wanaondolewa kero kwa kuwatafutia soko la uhakika.

Alisema wakulima wamekuwa wakitaabika kuuza korosho zao kutokana na serikali kuzinunua, lakini inasuasua kuwalipa.

Vilevile, alisema atawaruhusu wanaonunua korosho kwa utaratibu wa kangomba, ambao serikali imekuwa ikiuzuia kwa maelezo kuwa ni kuwanyonya wakulima wa zao hilo.

**ATAKA MAPINGAMIZI KUTUPWA**

Ametaka pia wagombea wote waliowekewa mapingamizi kuachiwa kabla ya Septemba 10, ili wakashindane na wagombea wengine katika sanduku la kura, hatua aliyosema itaepusha kuvunjika kwa amani na utulivu nchini.

AFARIJI WAATHIRIKA MAFURIKO

Kabla ya kufika katika eneo la mkutano wa kampeni, Membe alipita katika eneo lililokumbwa na mafuriko yaliyodumu kwa siku nne Januari mwaka huu ili kuwapa pole.

"Kabla ya mafuriko nilipita hapa Njinjo, ulikuwa mji mzuri kwelikweli, kulikuwa na maduka mazuri na makazi mazuri, poleni sana."

Kwa mujibu wa mkazi mmoja wa eneo hilo aliyejitambulisha kwa jina la Ally Ng'ambage, mafuriko hayo yalianzia katika Mto Matandu.

"Mafuriko yaliyotekea hapa yamesababisha baadhi ya wanakijiji kufariki, wengine kupoteza makazi," alisema Ng'ambage.

Alisema kutokana na mafuriko hayo, pia Shule ya Msingi ya Njinjo katika Kata ya Njinjo yenye vijiji vitatu vya Kipindimbi, Njinjo na Kisima Mkika iliathiriwa na mafuriko hayo.

Mkazi mwingine, Mosi Buriani, alisema wakazi wa eneo hilo wanahitaji msaada wa hali na mali ili kurejea katika hali ya kawaida baada ya athari za mafuriko hayo.

"Mafuriko yalitokea usiku, tukiwa tumelala vitu vilisombwa na mpaka sasa hali ni ngumu," alisema Buriani.

Alisema baadhi ya wakazi walihama na wengine kuishi katika mahema, jambo ambalo limewaathiri zaidi wanawake na watoto.

Alimweleza Membe jinsi alivyopoteza mtoto wa kaka yake mwenye umri wa miaka 20.

Mvua hiyo ilinyesha kwa siku tatu mfululizo Januari 25, 26 na 27, mwaka huu na kusababisha mafuriko yaliyoacha madhara makubwa kwa wakazi wa Kata ya Njinjo.

# JPM awaahidi neema wakulima, wafugaji

**Na Gwamaka Alipipi,**
SHINYANGA

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. John Magufuli, amewaahidi neema wakulima na wafugaji, endapo akichaguliwa tena kuiongoza nchi kwa miaka mitano ijayo.

Amesema Ilani ya Uchaguzi ya CCM 2020-2025 imegusa sehemu kubwa ya maisha ya wakulima na wafugaji, wakiwamo wa Mkoa wa Shinyanga alikokuwa jana.

Dk. Magufuli, akihutubia wananchi waliojitokeza kumsikiliza kwenye Uwanja wa Kambarage mjini Shinyanga jana, pia alisema serikali itaendelea kuchukua hatua kuhakikisha sekta ya maliasili inazidi kuimarika ili kuyafanya mazao yatokanayo na maliasili hususan misitu na nyuki kuchangia uchumi.

Aliahidi kuwa miaka mitano ijayo, serikali itahakikisha wakulima wanaongeza kipato chao na kuongeza fursa za ajira, akisisitiza kuwa atahakikisha vyama vya ushirika vinaimarika na kwenda kwa kasi.

"Kama Ilani ya CCM inavyosema, katika kipindi cha miaka mitano ijayo, tutahakikisha tunajenga maghala na vihenge vya kisasa, vitakavyokuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 250,000 za chakula. Katika baadhi ya halmashauri ujenzi umekamilika," alisema.

Dk. Magufuli pia aliahidi kujenga vituo vya kuchakata na kuhifadhi mazao katika mikoa ya Arusha, Mwanza, Tabora, Morogoro, Mtwara, Singida, Shinyanga, Songwe na Tanga.

Alisema kuwa katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kutejengwa viwanda vya nyama katika mikoa mbalimbali kwa lengo la kuwawezesha wafugaji kuuza nyama na kujipatia kipato.

"Katika ukurasa wa 45 wa Ilani ya CCM, inazungumzia kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo, wananchi wa Mkoa wa Shinyanga ni wakulima wazuri wa pamba, hivyo mtauza mazao yenu, kikubwa ndugu zangu ninaomba kura," alisema.

Dk. Magufuli pia alisema atahakikisha uzalishaji wa mazao yatokanayo na wanyama unaongezeka, akitolea mfano uzalishaji wa maziwa ambao wameweka lengo la kuongeza uzalishaji kutoka lita bilioni 2.7 hadi bilioni 4.5 kwa mwaka.

"Tunataka uzalishaji wa nyama uongezeke kutoka tani 81,220 hadi kufikia tani 150,000," alisema mgombea huyo na kuongeza kuwa serikali yake itahakikisha inaanzisha miradi ya ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki katika mikoa yenye ukame.

Pia, alisema serikali itahakikisha inaanzisha ujenzi wa mabwawa ya kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya binadamu, mifugo na kilimo katika mikoa ya Dodoma, Singida, Tabora, Mara, Simiyu, Arusha, Shinyanga, Manyara na maeneo mengine yenye ukame.



Mgombea urais wa CCM, Rais John Magufuli, akicheza muziki uliokuwa ukiimbwa na msanii wa Bongo Fleva, Chege Chigunda, baada ya kuhutubia wananchi wa Shinyanga Mjini katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu, kwenye uwanja wa Kambarage jana. **PICHA: IKULU**

**KATAMBI, MASELE**

Katika hatua nyingine, Dk. Magufuli aliahidi kumpa kazi aliyekuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini, Stephen Masele, ambaye alienguliwa na Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM licha ya kuongoza mchakato wa kura za maoni ndani ya chama hicho kuwania ubunge wa jimbo hilo.

"Ninawaomba wananchi wa Shinyanga mumchague Patrobas Katambi kuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini... yale mambo mengine achaneni nayo, huyo Masele nitampangia kazi nyingine. Kuna sehemu mtu anafanya ovyo ovyo, kuna kazi nyingi za kufanya serikalini, nileteeni Katambi.

"Huyu kijana (Katambi) ninamfahamu, ninajua utendaji kazi wake, aliacha u-DC (ukuu wa wilaya) makao makuu ya nchi, akaja kugombea ubunge, ni mchapakazi... sasa ukishinda ninaomba usibadilike," alisema.

Kwenye mchakato wa kura za maoni Jimbo la Shinyanga Mjini, Masele ambaye aliwahi kuwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini wakati wa serikali ya awamu ya nne, aliongoza kwa kura 152 akifuatwa na Jonathan Manya (65) na Gasper Kileo (51) huku Katambi akiambulia kura 12 kwenye nafasi ya saba.

Hata hivyo, majina yalipopelekwa Dodoma, vikao vya juu vya chama vilimrudisha Katambi kuwakilisha CCM kuwania ubunge wa jimbo hilo ambalo kwa miaka 10 iliyopita lilikuwa chini ya Masele.

# Lissu aanika sababu kuwania urais

## ■Afafanua tuhuma kutumiwa na mabeberu

**Na Waandishi Wetu**

MGOMBEA urais kwa tiketi ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Tundu Lissu, (pichani) ametaja sababu nne zilizomsukuma kujitosa kuwania nafasi hiyo kubwa zaidi ya uongozi nchini katika uchaguzi mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Katika mahojiano maalum na kituo cha runinga cha ITV jana, Lissu alisema ameamua kugombea nafasi hiyo kwa sababu kuu nne ukiwamo uwezo wake wa kuongoza.

"Ninaamini nina uwezo, nina nia ya kuirudisha Tanzania katika misingi yake ya mwanzo ya uhuru. Tulipopata uhuru, ulikuwa uhuru wa kazi, uhuru na umoja, uhuru na maendeleo," alisema.

Alisema wanahitaji maendeleo ya watu wakiwa huru na ya haki na hiyo ndiyo sababu nyingine iliyomsukuma kuomba ridhaa ya Watanzania kugombea urais mwaka huu.

Lissu alisema katika mazingira ya kawaida siyo jambo la ajabu kwa mtu yeyote ambaye ni mwananchi na mzalendo kutaka kuwa kiongozi.

"Urais ndiyo nafasi ya juu ya uongozi. Kama mwanasiasa, mwanasheria na mwananchi wa Tanzania, nimekuwa nikifikiria hivi nina uwezo kiasi gani wa kuwa rais wa nchi hii.

"Kwa kujibu swali lako ni kweli nilikuwa nikifikiria. Katika kipindi cha miaka mitano nilichokuwa nikifikiria juu juu, nimekuwa imara zaidi kwa sababu ya haya tuliyoyaona miaka mitano," alisema Lissu baada ya kuulizwa kama ilikuwa ndoto yake kuwania nafasi hiyo.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Lissu na kituo hicho cha runinga:

**SWALI:** Utawafanyia nini Watanzania ikiwa utashinda nafasi hiyo katika uchaguzi wa mwaka huu?

**LISSU:** Nitarudisha uhuru wa wananchi uliopotea, uhuru wa vyombo vya habari, uhuru wa kuisema serikali, uhuru wa watu kuzungumza na kuwajibisha, uhuru wa vyombo vya uwakilishi, uhuru wa kuabudu na uhuru wa taasisi za kiraia.

Uhuru ambao ninauzungumzia ni wa watu kutoa maoni yao, kujiunga katika makundi ya kiraia, kisiasa na kijamii pamoja na uhuru wa kuabudu na kufanya biashara za kiuchumi.

**SWALI:** Je, Ilani ya CHADEMA imejikita katika uhuru?

**LISSU:** Ilani ya CHADEMA inasema uhuru, haki na maendeleo ya watu. Afrika Kusini wakati wa ubaguzi wa rangi ilikuwa na maendeleo, lakini haikuwa nchi ya haki hata kidogo, watu walikufa ili kupata uhuru na haki.

Mfano mdogo, kuna kazi kubwa imefanyika ya kujenga miundombinu, ukipita Barabara ya Morogoro hadi Kibaha, eneo ambalo linajengwa zamani yalikuwa makazi ya watu kwa maelfu ambao wamebomolewa biashara zao na makazi.

Barabara ni nzuri, lakini ina maana gani kwa maelfu uliowavunjia vitega uchumi vyao? Maendeleo hayawezi kuwa barabara, inakuwa barabara kwa namna inavyowasaidia hao unaowabomolea.

**SWALI:** Ipo hoja kwamba CHADEMA ni chama cha walalamikaji na wakosoaji. Kuna ukweli katika hili?

Ninafikiri kwa katiba na sheria zilivyo, uhuru wa kuzungumza ni pamoja kulalamika pale unapoona mambo hayatendeki sawasawa na wale ambao wana wajibu wa kuyatenda. Uhuru ni pamoja na kukosoa pale panapohitaji kukosolewa.




**SWALI:** Tangu uhuru, Tanzania ilikuwa na maadui watu ambao ni ujinga, umaskini na maradhi. CHADEMA imekuwa na silaha gani kuwakabili?

**LISSU:** Ni kaulimbiu ya mwaka 1958 na umekuwa ni wimbo ambao bado wanaimba maadui wale wale. Tumejaribu kwa miaka 17 kuanzia 1967 hadi 1984 ilishindikana.

Tukaingia miaka ya mageuzi ya kiuchumi na kisiasa na kurudishwa nyuma kulikoshindikana. Inabidi twende kwenye msingi wa uhuru, haki na maendeleo.

**SWALI:** Suala la Katiba mpya ni kipaumbele chenu?

**LISSU:** Kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CHADEMA tumeandika katika mambo ambayo tutafanya siku 100 ya kwanza za urais ni kurejesha mchakato wa katiba mpya, kwa sababu yote wanayozungumza hayatawezekana kwa mfumo huu wa sasa uliokuwapo tangu mwaka 1962.Wengi wanafikiri shida ni katiba ya mwaka 1977.

Imejengwa katika msingi wa katiba ya mwaka 1962 na msingi ule ni kwamba Rais ni Alpha na Omega Tanzania, tunataka tukipata ridhaa, lazima tuweke utaratibu mpya wa kuongoza nchi.

Watu wanazungumza wabunge, hivi mnajua kwamba hawawezi kuleta muswada wowote wa fedha, hawana uwezo huo tangu tulipoanzisha Bunge mwaka 1926? Sheria kuanzia mwaka huo masuala yote ya fedha huanzia kwa Gavana.

Katiba yetu baada ya mwaka 1962, inasema itakuwa marufuku kwa mbunge kuleta hoja au muswada wowote au kuujadili isipokuwa tu umeanzishwa na kuruhusiwa na Rais na kuwasilishwa na waziri.

Alisema Rais hawajibiki kufuata ushauri wa mtu yeyote pale anapotekeleza wajibu wake, hivyo CHADEMA tutatengeneza utaratibu wa kiutawala ambao yeyote atakapokuja atadhibitiwa, atawajibishwa na kushughulikiwa.

**SWALI:** Je, wananchi wanaelewa ilani na sera zenu?

**LISSU:** Zipo siku 60 za kuzungumzia ilani na sera za CHADEMA katika mambo yote yanayohusu maisha yao kwa sababu hilo ndilo agano letu na Watanzania kwa miaka mingi ijayo.

Sikuwapo nchini miaka mitatu, hivyo sikukutana nao, lakini nimeshangaa namna ambavyo Watanzania wamebadilika na wapo tayari kufanya mabadiliko.

Tumefanya mikutano mikoa 17 katika kipindi cha siku 12, watu kwa maelfu wametulaki, wapo tayari kwa mabadiliko, miaka mitano hii imekuwa ya adha kubwa kwao.

**SWALI:** Mmefikia hatua gani katika kuunda kile kinachoitwa UKAWA mpya?

**LISSU:** Mwaka 2015, tuliunda UKAWA (Umoja wa Katiba ya Wananchi) ambao ulileta mafanikio makubwa na ambao hawatutakii mema walijua hatari yake na mwaka jana walifanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa.

Yanasema hivi; 'chama cha siasa kina uhuru wa kuungana na kingine wakati wa uchaguzi ili mradi kila kitu mnachokipanga lazima mkiwasilishe kwa Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye ana mamlaka ya kuwakubalia au kuwakatalia'.

Masuala ya mtatumia fedha kiasi gani, kwenye jimbo gani, eneo gani, kila jambo linalohusu mkakati wenu wa ushindi, lazima mmpelekee Jaji Francis Mutungi.

Mazingira ya kisheria ya sasa ya vyama kuungana ni mitego mitupu, ambayo haijatengenezwa na vyama vya upinzani bali CCM ili watakaojiingiza wanaswe.

Tutakuwa wajinga sana kama vyama kuingia kwenye mitego hii bila tahadhari. Tunazungumza na ACT-Wazalendo, tuangalie hii mitego tunaweza kuiepuka namna gani, tushirikiane kwa namna ambayo itatuepusha na hizi hatari tulizotegewa kila mahali.

**SWALI:** Dhana iliyopo ni kwamba upinzani ni watu wa shari, vurugu, migogoro na kuvunja usalama. Je, ndivyo mlivyo?

**LISSU:** Sisi siyo wa shari na katika mwezi mmoja tumefanya mikutano na maandamano. Julai 27 niliporejea kutoka Ubelgiji, maelfu walijitokeza na hakuna aliyeibiwa simu.

Viongozi wetu wameshambuliwa mchana na watu wasiojulikana, niangalie mie unaniuliza 'hujambo?' kwa sababu unajua yaliyonitokea.

Mnadhimu wa Kambi Rasmi Bungeni kupigwa risasi 16 na watu wasiojulikana ndani ya eneo linalolindwa saa 24, ninafikiri tafsiri ya haya maneno tuanze kuzifikiria upya.

**SWALI:** Ipo hoja kwamba mnatumiwa na watu wa nje kwa manufaa yao. Watu hao wamekuwa wakiwafadhili. Kuna ukweli katika hili?

**LISSU:** Hizo ni porojo za watu waliokosa hoja ya kujibu. Nimekuwa na msimamo huu tangu nikiwa kijana na sijawahi kubadilika.

Mwaka 1999 wakati wa Benjamin Mkapa (Rais wa Awamu ya Tatu) niliyasema nikashtakiwa kwa uchochezi. Wakati wa Jakaya Kikwete (Rais wa awamu ya nne) na hata sasa nimeendelea kusema.

Wakiumwa hawa wanakwenda kutibiwa nje. Nyerere alitibiwa Uingereza, Mkapa alitibiwa Uswizi, Kikwete Marekani na mimi Ubelgiji, hawa watu ni marafiki zetu, tukipata shida, tunawakimbilia halafu tunawatukana huku tunawategemea.

Nitajenga uhusiano wa kimataifa kwa sababu nchi inahitaji dunia kuliko dunia inavyoihitaji Tanzania.

**KAMPENI TABORA**

Katika mkutano wake wa uzinduzi wa kampeni mjini Tabora jana, Lissu aliahidi kuwa akiwa Rais, atahakikisha anavirejesha serikalini viwanja vya michezo vinavyomilikiwa na CCM katika maeneo mbalimbali nchini.

Alisema viwanja hivyo ni mali ya umma kwa kuwa vilijengwa kwa kodi za Watanzania, lakini sasa vinamilikiwa na chama kimoja cha siasa. Alisema viwanja hivyo vitakuwa chini ya manispaa na vitakuwa huru kwa ajili ya matumizi ya umma tofauti na ilivyo sasa.

Katika kampeni hizo, mgombea huyo pia aliahidi kutoa bima ya afya kwa Watanzania wote atakapoingia madarakani ili kusaidia upatikanaji wa uhakika wa matibabu kwa wote na kwa gharama nafuu.

***Imeandikwa na Romana Mallya na Mary Geofrey**

HAKIARDHI

LAND RIGHTS RESEARCH & RESOURCES INSTITUTE

# MADAI YA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 TAFSIRI NA VIGEZO VYA WAZALISHAJI WADOGO

Wazalishaji wadogo wanatafsiriwa kuwa ni wale ambao hawategemei nguvu kazi ya ajira ya kudumu au rasmi badala yake uzalishaji mali wao hutegemea nguvu kazi ya familia na zana za asili. Kuna makundi mbalimbali ya wazalishaji wadogo hapa nchini ambayo kwa kiasi kikubwa yanategemea kilimo, ufugaji, uvuvi, kuokota matunda na uchimbaji mdogo wa madini katika kuendesha maisha yao kila siku. Makundi haya ni pamoja na: ***wakulima wadogo, wafugaji wadogo, wachimbaji wa madini wadogo, wavuvi wadogo, waokota matunda na warina asali.***

### 1.2 MUKTADHA NA MCHANGO WA WAZALISHAJI WADOGO NCHINI

Ardhi ni mojawapo ya rasilimali muhimu kwa uhai wa binadamu na viumbe vyote. Ardhi hubeba rasilimali nyingine zote za asili na miundo mbinu. Vilevile, ardhi huchangia katika ukuaji wa maendeleo ya mtu mmoja mmoja, jamii kwa ujumla na uchumi wa Taifa. Makundi ya wazalishaji wadogo yanategemea ardhi katika shughuli mbalimbali za kilimo, uvuvi, ufugaji, uchimbaji wa madini na shughuli nyinginezo za kiuchumi. Mfano, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania wote ni wazalishaji wadogo wanaotegemea ardhi katika shughuli zao za uzalishaji mali.

Umuhimu wa ardhi kwa makundi haya, si tu unatanabaishwa kwenye sera na sheria, bali umeainishwa kwenye mikakati na programu za maendeleo ya nchi. Mfano, moja ya malengo ya Sera ya Ardhi ya 1995, ni kuhakikisha kuwa kuna ugawaji na upatikanaji sawa wa ardhi kwa wananchi wote. Hii ina maana kuwa ugawaji na upatikanaji wa ardhi lazima uzingatie haki za makundi yote nchini, ikiwemo makundi haya ya wazalishaji wadogo hasa wanawake. Vile vile sera inasema kuwa haki za kimila za wazalishaji wadogo, yaani wakulima wadogo na wafugaji, ambao ni wengi nchini, zitambuliwe, ziainishwe, na kulindwa kisheria.

Sera ya Mifugo ya mwaka 2006, inaainisha kuwa serikali itaweka utaratibu wa kuibua mifumo bora ya uzalishaji itakayoongeza tija miongoni mwa wafugaji wadogo. Kwa upande mwingine, Sheria za Ardhi, yaani sheria namba. 4 na 5 za mwaka 1999, zote kwa pamoja zinatambua mfumo wa umiliki wa ardhi kimila. Mfumo huu unalenga kutambua haki na maslahi ya wazalisha wadogo wanaopata, kutumia na kumiliki ardhi kwa njia ya kimila. Vilevile, programu ya Kuendeleza Kilimo ya Awamu ya Pili (ASPD II), inalenga kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo (kilimo, mifugo na uvuvi) ili kuongeza uzalishaji na pato la wakulima wadogo kwa ajili ya kuboresha maisha yao, usalama wa chakula na lishe.

Kwa kiasi kikubwa wazalishaji wadogo ndio wachangiaji wakubwa katika ukuaji wa pato la Taifa na kukuza uchumi wa nchi. Kwa mfano, sekta ya kilimo inachangia zaidi ya asilimia 40 ya pato la Taifa na wakulima wadogo ndio wawekezaji wakubwa katika sekta ya kilimo ambapo wanazalisha takribani asilimia 75 ya chakula chote kinachozalishwa nchini. Uzalishaji wa mazao ya bustani hususan mboga, matunda na viungo huchangiwa kwa asilimia 85 na sekta isiyo rasmi ambayo wakulima wadogo ndio wanaozalisha na kuuza mazao hayo katika masoko ya ndani.

Wafugaji wa asili wanachangia kwa kiasi kikubwa katika uzalishaji wa nyama, maziwa, ngozi na mbolea. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka 10, kuanzia mwaka 1995 mpaka mwaka 2005, ufugaji wa asili ulichangia uzalishaji wa tani 134,500 za nyama. Hivyo uzalishaji wa nyama kwa kipindi hicho uliongezeka kutoka tani 244,000 hadi tani 378,500 sawa na ongezeko la asilimia 55 ambapo sehemu kubwa ilitokana na ufugaji wa asili. Pia, uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 555 hadi bilioni 1.38 ambapo asilimia 70 ilichangiwa na sekta ya ufugaji wa asili. Vilevile, uzalishaji wa mayai uliongezeka kutoka mayai milioni 380 hadi bilioni 1.8. asilimia kubwa ikiwa imechangiwa na wafugaji wa asili.

Wachimbaji wadogo wa madini, wanachangia kiasi kikubwa katika kuongezeka pato la Taifa. Mfano, kwa kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Februari 2020, kupitia masoko ya madini nchini, wachimbaji wadogo wamefanya biashara ya madini yenye thamani zaidi ya shilingi trilioni moja na wameiingizia Serikali mapato kwa kulipa mrabaha na ada ya ukaguzi wa zaidi ya shilingi bilioni sabini na nane. Vilevile, wachimbaji wadogo wanachangia karibu asilimia 0.3 ya mapato yao kwenda Halmashauri za wilaya na hivyo kuongeza kipato katika serikali za mitaa.

Wanawake nao ni mojawapo ya kundi la wazalishaji wadogo lenye mchango mkubwa katika ujenzi wa jamii na kukuza uchumi wa Taifa. Inakadiriwa kuwa takribani asilimia 52 ya idadi ya watu wote nchini ni wanawake. Pia wanawake wanashiriki katika uzalishaji mali kwa takribani asilimia 60 hadi 80 ya chakula kinachotegemewa katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Tafiti nyingi zinaonyesha kuwa asilimia 20 tu ya wanawake ndio wanaomiliki ardhi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hali hii inachangia wanawake kuendelea kuwa masikini, kunyanyaswa na kudhalilishwa.

### 1.3 CHANGAMOTO ZA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI

Pamoja na mchango mkubwa wa wazalishaji wadogo katika uchumi wa nchi, bado wanaendelea kukumbana na changamoto mbalimbali zinazohusisha ukosefu wa masoko ya uhakika, pembejeo za kutosha na za wakati, mapungufu katika mifumo ya kisera na kisheria inayokumbatia wazalishaji wakubwa na wawekezaji kutoka nje kuliko makundi haya ya wazalishaji wadogo. Vilevile, wakulima wadogo wanakosa ruzuku na pembejeo za kilimo, pamoja na ukosefu wa ulinzi wa uhakika wa ardhi kwa ajili ya uzalishaji. Ukiachana na changamoto hizi za jumla, sehemu hii inaangazia changamoto za wazalishaji wadogo zenye mguso wa moja kwa moja na upatikanaji, matumizi na usimamizi wa ardhi kama inavyoainishwa hapa chini:

**Moja** ni kukosekana kwa mifumo imara inayolinda haki na maslahi mapana ya wazalishaji wadogo katika ardhi. Mfano, mfumo wa umilikaji wa ardhi, changamoto za upatikanaji wa rasilimali za maji na malisho zinazoathiri wazalishaji wadogo. Hii ni pamoja na kasi ndogo ya kutenga na kumilikisha ardhi kulingana na taratibu za kisheria au kimila.

**Mbili** ni kupanuka kwa shughuli za kilimo, hasa kilimo biashara, katika maeneo yaliyokuwa yanatumika kwa kufuga na kuchungia mifugo.

**Tatu** ni kasi ya kuhuisha na kupanuliwa kwa maeneo ya hifadhi za wanyamapori kama hifadhi za taifa, mapori tengefu, mapori ya akiba, na maeneo ya hifadhi za jamii ambayo kwa pamoja yanazuia kuendelezwa kwa maeneo ya wakulima na wafugaji. Hii imesababisha hifadhi za wanyamapori kuwa karibu na wananchi na hivyo kusababisha migogoro ya wanyama na binadamu hasa pale wanyama wanapoingia kwenye mashamba ya wananchi na kula mazao au mifugo yao.

**Nne** ni ushirikishwaji hafifu wa wazalishaji wadogo katika kutoa maamuzi ya upangaji wa matumizi na usimamizi wa ardhi yao. Mfano, pamoja na ukweli kuwa wafugaji wa asili ni kundi kubwa la wazalishaji wadogo, lakini wamekuwa hawashirikishwi kikamilifu katika mchakato wa uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji. Hivyo kusababisha maeneo mengi yanayofaa kwa ufugaji kutengewa matumizi mengine. Vilevile, baadhi ya maeneo ya mashamba ya wakulima wadogo yamekuwa yakiainishwa na kutengwa kama maeneo ya mipango miji bila kushirikisha wakulima wenyewe na bila kufanya utafiti wa kina juu ya madhara ya kutangaza mashamba hayo kuwa maeneo ya mipango miji. Hii imesababisha wakulima wadogo kushindwa kuendeleza shughuli za kilimo na kubaki kwenye sintofahamu ya hatma ya maisha yao.

**Tano** ni haki za wanawake katika kupata, kutumia, kumiliki na kufanya maamuzi juu ya ardhi hazizingatiwi ikilinganishwa na wanaume. Hii ni kutokana na mila na desturi zinazowanyima wanawake njia halali za kumiliki ardhi ikiwemo kurithi ardhi za wazazi na wenza wao na hivyo kutoshiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi. Wanawake wanapewa fursa ya kutumia ardhi na kufanya shughuli za uzalishaji lakini wanaume ndio wanaoamua namna ya kutumia mapato yanayotakana na nguvu ya mwanamke.

**Sita** ni ubidhaishaji wa huduma za kijamii kama vile afya, elimu, maji na pembejeo za kilimo, hii imepelekea changamoto kubwa kwa wazalishaji wadogo ambapo hufikia hatua wanauza chakula cha akiba ili wamudu gharama za huduma hizi muhimu.

**Saba** ni ushirikishwaji hafifu wa wazalishaji wadogo katika michakato ya utungaji na mabadiliko ya sera na sheria za ardhi na rasilimali nyinginezo, hivyo kupelekea sera na sheria husika kutoakisi maoni na mahitaji ya wazalishaji wadogo.

### 1.4 HATUA ZILIZOCHUKULIWA NA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MIAKA MITANO (2015 – 2020)

Kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, serikali imechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuimarisha utawala na usimamizi wa ardhi nchini na hivyo kuwezesha wazalishaji wadogo kutekeleza shughuli zao. Kwa ujumla hatua hizi ni pamoja na kufuta hati za mashamba makubwa yasiyoendelezwa kwa muda mrefu, kuchukua hatua mbalimbali za kutatua migogoro ya ardhi, kutunga na kuboresha sheria na sera kwa lengo la kuimarisha usimamizi na umiliki wa ardhi. Mahususi kabisa, serikali imechukua hatua zifuatazo:

**Kwanza** ni ufutaji wa hati za mashamba ya uwekezaji ambayo yalikuwa hayajaendelezwa kwa muda mrefu katika maeneo mbalimbali nchini. Mfano, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli, alifuta jumla ya hati 14 za mashamba yaliyoshindwa kuendelezwa katika Wilaya za Kilosa, Mvomero na Kilombero. Vilevile, Mh. Rais alifuta hati ya shamba la mkonge la Kibaranga, wilaya ya Muheza lenye ukubwa wa hekta 5,730. Mashamba mengine yalipunguzwa ukubwa kama vile shamba la Kampuni ya KPL Kilombero lilipunguzwa hekta 810 na shamba la Kapunga Mbarali hekta 4,620.

Pamoja na ufutaji wa hati hizi lakini bado kuna changamoto ya wazalishaji wadogo kutokurudishiwa mashamba hayo kama alivyoagiza Mhe. Rais. Kwa mfano, katika Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro wakulima na wafugaji wameendelea kudai kurudishiwa mashamba hayo kwa usawa.

**Pili** ni jitihada za kutatua migogoro ya ardhi, hasa ile ya wananchi na maeneo ya hifadhi, mwaka 2019, Rais aliunda Kamati ya Mawaziri kubainisha vijiji vyote vilivyoainishwa kuwa katika hifadhi za wanyamapori. Kufuatia mapendekezo ya Kamati, Baraza la Mawaziri mnamo mwezi Septemba 2019, liliridhia kuwa vijiji 920 kati ya vijiji 975 vilivyokuwemo ndani ya hifadhi, mapori ya akiba na ranchi kuhalalishwa rasmi kwa ajili ya shughuli za kilimo, ufugaji na kijamii. Aidha, Serikali inaendelea kufanya tathmini ya vijiji 55 vilivyobaki ili kutoa maamuzi. Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara nyingine za kisekta na wadau mbalimbali inaendelea kuhakiki mipaka ya vijiji husika, kupanga na kupima ili kuzipa Serikali za vijiji mamlaka ya kusimamia ardhi za vijiji hivyo.

**Tatu** ni serikali kuanzisha na kutekeleza miradi mbalimbali ya mipango ya upimaji wa mashamba na viwanja kwenye ardhi za mijini na vijijini. Miradi ya urasimishaji wa ardhi ambayo imekuwa ikifanywa na serikali yenyewe pamoja na makampuni binafsi ya upimaji wa ardhi. Vilevile kumekuwepo na miradi mikubwa ya mipango ya matumizi ya ardhi na utoaji wa vyeti vya Hakimiliki za kimila katika wilaya za Ulanga, Malinyi na Kilombero pamoja na miradi mingine katika wilaya nyinginezo nchini. Changamoto kubwa katika miradi ya upimaji wa ardhi imekuwa ni ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu matumizi ya Hati za Hakimiliki za Kimila. Kuna dhana iliyojengeka kuwa Hati ya Hakimiliki ya kimila ni kwa ajili ya kuchukulia mikopo benki. Dhana hii ni matokeo ya ukosefu wa elimu na inaweza kuhatarisha uhakika na usalama wa kumiliki ardhi za wazalishaji wadogo pale watakaposhindwa kurejesha mikopo waliyochukua.

**Nne** ni serikali kuanzisha mchakato wa mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na Sera ya Kilimo ya mwaka 2013. Sheria na Sera hizi zilikuwa na malengo ya kuboresha usimamizi na utawala wa ardhi, na kutenga maeneo mahususi kama ardhi ya kilimo. Hata hivyo, michakato ya utungaji wa sheria na uandaaji wa sera ilifanyika kwa ukimya bila kushirikisha makundi makubwa ya wazalishaji wadogo.

**Tano** ni kutengwa kwa bajeti ndogo ya sekta ya ardhi kwa kuzingatia ukweli kuwa sekta ya ardhi sio kipaumbele katika vipaumbele mahususi vya serikali. Kwa mfano, kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, sekta ya ardhi haikupewa kipaumbele cha bajeti ya kutosha. Mafanikio ya sekta nyingine muhimu kama vile afya, elimu, kilimo, maliasili na utalii, viwanda, miundombinu, ujenzi, nishati na madini hutegemea jinsi ardhi ilivyopangwa na kuratibiwa. Kutokana na umuhimu huo ni vyema Bajeti ya Wizara ya Ardhi ikapewa kipaumbele katika sekta tano za juu zinazotengewa bajeti ya kutosha ili kuwezesha maendeleo ya sekta nyingine.

Pamoja na ufinyu wa bajeti katika sekta ya ardhi, pamekuwepo na changamoto nyingine zinazowaathiri wazalishaji wadogo. Baadhi ya changamoto hizo ni pamoja kuongezeka kwa migogoro ya ardhi inayosababishwa na matumizi mbalimbali ya ardhi, mabadiliko ya tabianchi, migogoro ya mipaka ya vijiji na vijiji, kupanuka kwa miji, kuongezeka kwa ardhi za uwekezaji na hifadhi za wanyamapori, kukosekana kwa mipango thabiti na ya kutosha ya matumizi ya ardhi.

Kwa muda mrefu wazalishaji wadogo wamekuwa na madai mbalimbali ambayo yanapaswa kupewa kipaumbele na serikali ili kuhakikisha kuwa ardhi na rasilimali nyingine zinatumika kuwanufaisha wao kijamii na kiuchumi. Madai haya yamegawanywa katika makundi tisa kama ilivyoainishwa katika sehemu ya pili.

**SEHEMU YA PILI**

### 1.5 MADAI YA WAZALISHAJI WADOGO KATIKA ARDHI NA RASILIMALI NYINGINEZO

### 1.6 UTAWALA NA USIMAMIZI WA ARDHI

**Muktadha:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ndio yenye dhamana ya kuhakikisha kuwa ardhi yote nchini inapangwa, inapimwa na kumilikishwa, hii ni katika kuhakikisha kuwa kuna uboreshwaji wa huduma mbalimbali hasa katika nyanja za uwekezaji katika ardhi, makazi na milki. Katika kuhakikisha huduma zinaboreshwa Wizara hapo awali ilianzisha ofisi za ardhi katika kanda tisa, pamoja na jitihada hizi bado kumekuwepo na vikwazo na changamoto mbalimbali, ni katika muktadha huu Wizara imeamua kuanzisha ofisi za ardhi kwa kuwateua makamishina wasaidizi katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. Kwa takribani miaka mitano iliyopita kumekuwapo na jitihada za kurejesha ardhi zilizotwaliwa kwa ajili ya uwekezaji kwa wananchi ama wazalishaji wadogo, na pia ardhi zilizotengwa kwa minajili ya uhifadhi kurejeshwa kwa wanavijiji hasa pale ambapo kumekuwapo na migogoro ya kimatumizi.

**Changamoto:** Sheria za ardhi zinampa Kamishna wa Ardhi kuwa na mamlaka ya ushauri kwenye Halmashauri za Vijiji na wanavijiji juu ya usimamizi wa ardhi ya kijiji. Kumekuwepo na matumizi mabaya ya mamlaka hiyo hasa pale ushauri unaotoka kwa Kamishna kuchukuliwa kama ni uamuzi wa mwisho hivyo kuchukua nafasi ya maamuzi ya wanakijiji kuhusu ardhi yao. Wakati mwingine wanavijiji wamekuwa wakikosa ushauri wanaohitaji kutoka kwa Kamishna na pale unapopatikana basi unatolewa kwa lengo la kufanikisha maombi ya ardhi yanayohusisha uhawilishaji kutoka ardhi ya Kijiji kuwa ya Jumla kwa ajili ya shughuli za uwekezaji.

Utaratibu ulioainishwa kisheria wa ardhi ya kijiji kusimamiwa na Serikali ya kijiji na maamuzi ya mwisho kufanywa na Mkutano Mkuu wa Kijiji. Utaratibu huu umefanya kazi vizuri hasa katika maeneo ambayo wanakijiji wana uelewa mzuri wa haki zao za kisheria na taratibu za ardhi. Changamoto kuu ni kwamba elimu juu ya haki za ardhi na nafasi ya vyombo kama Mkutano Mkuu wa Kijiji haijawafikia wanavijiji walio wengi na pia hili ni suala endelevu, kwani kila mwaka wanapatikana wanavijiji wapya kwa maana ya kigezo cha kutimiza umri wa miaka 18 ili kukidhi takwa mojawapo ya kuwa mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Kijiji.

**Mapendekezo:**

- Halmashauri za vijiji na Mikutano Mikuu ya vijiji viendelee kuwa na dhamana juu ya ardhi ya kijiji hususani katika usimamizi, matumizi na ugawaji.
- Mkutano Mkuu wa kijiji uendelee kuwa ndio chombo chenye mamlaka ya juu (Milki ya hatma) katika maamuzi juu ya ardhi ya kijiji na wananchi wapewe elimu zaidi juu ya mamlaka yao hii.
- Halmashauri za vijiji zijengewe uwezo wa kusimamia ardhi na maliasili zilizopo ndani ya vijiji kwa niaba ya wanakijiji wote.
- Ugatuaji uliofanyika wa kuwateua Makamishina wasaidizi katika ngazi ya mikoa bila shaka utasaidia zaidi kufikisha huduma za kiushauri hadi ngazi ya kijiji kwa ufanisi zaidi.
- Ardhi zote ambazo zimetelekezwa na wawekezaji wa ndani na nje ya nchi zirejeshwe kwa wazalishaji wadogo hususani wakulima, wafugaji na makundi mengineyo ya wazalishaji wadogo. Katika hili haki ya wanawake kumiliki ardhi izingatiwe
- Elimu juu ya sera na sheria zinazosimamia ardhi ijumuishwe katika mitaala ya elimu ya msingi, sekondari pamoja na vyuo ili kuwawezesha vijana kuwa na uelewa juu ya masuala yanayohusu haki za ardhi.

### 1.7 MFUMO WA KUMILIKI ARDHI NCHINI

**Muktadha:** Sera ya Taifa ya Ardhi 1995 pamoja na Sheria za Ardhi namba 4 na 5 za mwaka 1999 zinatambua aina mbili za umiliki wa ardhi nchini ambazo ni umiliki wa ardhi kwa Hati na umiliki wa ardhi Kimila. Hati hutolewa kwa mmiliki wa ardhi katika kundi la ardhi ya jumla wakati umiliki wa kimila ambao umetengenezewa cheti cha hakimiliki ya kimila hutolewa kwa mmiliki wa ardhi ndani ya Kijiji.

Sheria za Ardhi zimeweka usawa katika aina hizo mbili za umiliki na tofauti ya msingi iliyopo ni kuwa hati itatolewa kwa ukomo wa muda maalum, yaani miaka 33, 66 au 99 wakati umiliki wa ardhi kimila hutolewa bila ukomo wa muda. Vilevile, mmiliki wa ardhi kwa hati anakuwa na hadhi ya mpangaji kwa kuwajibika kulipa kodi ya ardhi kwa Kamishna wa Ardhi kila mwaka wakati mmiliki wa ardhi kimila hana tozo ya kodi ya ardhi isipokuwa kama kijiji kimejiwekea utaratibu wa kutoza kodi hiyo.

**Changamoto:** Mfumo wa umiliki wa ardhi unakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa uhakika wa umiliki pale ardhi inapohitajika kwa manufaa ya umma. Sheria ya Utwaaji namba 47 ya mwaka 1967 inampa Rais mamlaka ya kuchukua ardhi yoyote kwa manufaa ya umma ambapo sheria hiyo wakati mwingine imekuwa ikitumiwa vibaya na mamlaka za serikali kwa kuchukua ardhi za wananchi kwa kisingizio cha maslahi ya umma.

Vilevile, mfumo wa umiliki wa ardhi kimila umeshindwa kuakisi uhalisia wa umiliki kimila ambapo ardhi inamilikiwa kwa misingi ya koo husika kwa kuwa cheti cha hakimiliki ya kimila kinachotolewa ni lazima kiandikwe kwa jina la mtu. Hii imepelekea kuleta migongano kwenye koo ambazo bado zinahitaji kumiliki maeneo hayo kimila kwa kuwa wanapotaka kupima na kupatiwa hati ya kimila wanapaswa kukubali ardhi hiyo igawanywe kwanza ndio upimaji ufanyike kwa kipande cha mtu mmoja mmoja.

**Mapendekezo:**

- Mfumo wa umiliki ardhi kimila ufanyiwe marekebisho ili kuweza kuakisi uhalisia wa umiliki ardhi kimila.
- Utwaaji wowote wa ardhi sharti uzingatie ridhaa huru na fidia ya haki na kwa wakati itakayomuweka muathirika katika nafasi nzuri zaidi ya aliyokuwa nayo mwanzo.
- Ukomo wa ukubwa wa umiliki wa ardhi ndani ya vijiji uwe ni Ekari 100, hii inazingatia mahitaji ya ardhi ndani ya kijiji na kuondoa uwezekano wa kuhodhiwa ardhi kubwa na kikundi kidogo cha watu.
- Endapo mtu anamiliki ardhi zaidi ya kijiji kimoja ukomo wake utahesabiwa kwa kujumlisha ukubwa wa ardhi zote anazomiliki. Ikiwa mmiliki anahitaji eneo zaidi ya ekari 100 basi mtu huyo aombe ardhi kwenye kundi la ardhi ya jumla.

### 1.8 HAKI ZA WANAWAKE NA WATU WENYE ULEMAVU KATIKA ARDHI

**Muktadha:** Katiba ya nchi na sheria za ardhi zinatambua haki za wanawake katika ardhi kwa maana ya kupata, kutumia, kumiliki na kudhibiti ardhi, bado wanawake wameendelea kupata changamoto ili kuzifikia haki hizo. Hata hivyo kwa miaka ya karibuni kuna mabadiliko chanya katika jamii ambayo imeanza kutambua kuwa mwanamke anayo haki sawa na mwanaume katika umiliki wa ardhi. Mabadiliko hayo yamechangiwa hasa na jitihada mbalimbali za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kupitia mafunzo na kampeni mbalimbali zinazolenga kuhakikisha haki za wanawake katika ardhi zinatambulika na kulindwa.

Haki za kumiliki mali kwa wanawake zinaboresha usawa wa kijinsia ambao unapelekea maendeleo. Hivyo haki ya kumiliki mali kwa wanawake ni muhimu kwani ndiyo inayompa mwanamke ulinzi wa kiuchumi, hadhi ya kijamii na kisheria na hivyo kuweza kuendelea kiuchumi. Ikumbukwe kuwa, wanawake wanachangia kwa kiasi kikubwa pato la Taifa hususani walio katika sekta isiyo rasmi kama vile kilimo. Mpaka kufikia mwaka 2014, wanawake waishio vijijini walikuwa wanashiriki katika kilimo kwa asilimia 90.

**Changamoto:** Uwepo wa mila, desturi na dini kandamizi ni tatizo kubwa katika umiliki wa ardhi kwa wanawake. Mila na desturi za jamii nyingi zimekuwa zikimnyima mwanamke haki ya kumiliki na kufanya maamuzi juu ya ardhi ya familia au ukoo. Mwanamke amekuwa akionekana ni mtu asiyestahili kumiliki ardhi kwa fikra kwamba akiolewa atakwenda kumiliki ardhi kwa mumewe. Vilevile watoto wa kike hawarithi ardhi za wazazi wao kwa usawa kama walivyo watoto wa kiume.

Kukosekana usawa wa kijinsia, hususani chini ya mifumo ya kimila, inachangia sana kunyima haki za wanawake katika ushiriki wa maamuzi kuhusu ardhi na rasilimali na umiliki wa ardhi ingawa ndio wazalishaji mali wakubwa hali inayowafanya kutonufaika na matunda ya kazi yao.

Udhaifu wa kimaamuzi katika vyombo vya usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi katika ngazi za vijiji na kata ni changamoto katika upatikanaji wa haki za ardhi kwa wanawake. Kukosekana kwa vitendea kazi na weledi miongoni mwa wajumbe wa vyombo hivi unapelekea haki za wanawake kucheleweshwa au kutopatikana kabisa.

Uzoefu unaonyesha kuwa ushiriki wa wanawake katika vyombo vya usimamizi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kwa kiasi kikubwa sio mzuri. Mfano idadi ya wajumbe wanawake kwenye Mabaraza ya Ardhi ya vijiji, Mabaraza ya Kata na Halmashauri za vijiji imeendelea kuwa pungufu.

**Mapendekezo:**

- Wazalishaji wadogo wanahitaji mambo yafuatayo yatekelezwe ili kuhakikisha kuwa wanawake wanapata haki zao za msingi kama ambavyo Katiba na sheria za nchi zinaelekeza;
- Vyombo vya usimamizi wa ardhi na utatuzi wa migogoro ya ardhi kama vile Mabaraza ya Ardhi ya vijiji, Mabaraza ya Kata na Halmashauri za vijiji vijengewe uwezo ili kutekeleza majukumu yao kwa usahihi ikiwa ni pamoja na kuzingatia na kutunza haki za ardhi za wanawake na watu wenye ulemavu.
- Serikali ielekeze nguvu kubwa katika kukuza uelewa wa jamii juu ya sheria za ardhi na haki za ardhi kwa wanawake na watu wenye ulemavu.
- Kuwepo na usimamizi thabiti wa serikali juu ya utekelezaji wa sheria za ardhi ili kukabiliana na mila na desturi kandamizi dhidi ya wanawake na watu wenye ulemavu.

# TANGAZO

### 1.9 UKUAJI WA MIJI

**Muktadha:** Katika kipindi cha takribani muongo mmoja uliopita, Tanzania imeshuhudia kasi kubwa ya ukuaji wa miji, kiwango cha ongezeko la watu katika miji mingi nchini kimeendelea kuwa kikubwa kila mwaka. Uhamiaji wa watu kutoka vijijini kwenda mijini kumepelekea kupanuka kwa maeneo ya miji. Pia idadi ya miji inaongezeka kadri vijiji vinavyopanuka na kubadilika kuwa miji. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 1967 wakazi wa miji walikuwa asilimia 5.7 na mwaka 2012 iliongezeka kufikia asilimia 29.1. Ukuaji wa miji nchini una kasi ya asilimia 7 – 11 kwa mwaka kiwango ambacho ni kikubwa ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.5 kwa Afrika.

Eneo linapokuwa tayari kuendelezwa kimji, hupangwa na kupimwa kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Namba 8 ya mwaka 2007 ambayo imeainisha taratibu za upangaji na uendelezaji wa maeneo mapya ya miji ambazo ni;

**Hatua ya kwanza** ni eneo kutangazwa kama ni eneo la mpango linalotakiwa kuendelezwa kimji;
**Hatua ya pili** ni uhamasishaji wa wadau mbalimbali;
**Hatua ya tatu**, ni ukusanyaji wa takwimu na taarifa mbalimbali;
**Hatua ya nne**, ni uchambuzi wa takwimu na taarifa mbalimbali;
**Hatua ya tano**, ni kutayarisha misingi ya mpango wa jumla;
**Hatua ya sita**, ni kutayarisha mpango wa awali;
**Hatua ya saba**, ni wadau kupitia na kuthibitisha mpango wa awali;
**Hatua ya nane**, ni kurekebisha mpango wa awali uliopitishwa na mkutano wa wadau; **Hatua ya tisa**, ni kuthibitishwa kwa mpango;
**Hatua ya kumi**, ni kufanyika kwa uthamini wa mali za wananchi, na ulipaji wa fidia kwa nia ya kutwaa eneo la mpango;
**Hatua ya kumi na moja,** ni upimaji wa maeneo kwa kuzingatia mpango uliotayarishwa; **Hatua ya kumi na mbili**, ni kutangazwa kwa viwanja vilivyopimwa, kupokea maombi ya wahitaji wa viwanja na ugawaji kwa waombaji waliokubaliwa na kamati ya kugawa ardhi.

**Changamoto:** Kuna changamoto kadhaa zinazokabili ukuaji wa miji nchini, changamoto hizi ni pamoja na kutokufuatiliwa ipasavyo taratibu zilizoainishwa na Sheria ya Mipango Miji kama zilivyojadiliwa hapo juu.

**Kwanza**, ni kukosekana kwa ushirikishwaji wa wanavijiji kwenye vijiji vilivyoko kwenye mpango wa mipango miji;

**Pili**, kumekuwepo na dhana ya kuwa ukuaji wa vijiji kuwa miji hufanyika kwa lengo la kuongeza thamani ya ardhi ya eneo husika hivyo kuchochea soko la ardhi pamoja na kutoza kodi ya ardhi na majengo;

**Tatu**, ni wanavijiji kutokulipwa fidia za haki na kwa wakati. Wakati mwingine wanavijiji hulipwa fidia hata baada ya miaka kadhaa kupita jambo ambalo ni kinyume na taratibu za ulipwaji wa fidia ambazo zinataka fidia kulipwa kwa wakati;
**Nne**, ni utaratibu wa mipango miji kuondoa shughuli zote ambazo zilikuwa zikifanyika katika ardhi ya Kijiji kama vile kilimo na ufugaji na kupelekea wazalishaji wadogo kushindwa kuendeleza ardhi zao pale vijiji vyao vinapotangazwa kuwa miji.

**Mapendekezo:**
- Wazalishaji wadogo wanahitaji masuala yafuatayo kuzingatiwa katika ukuaji wa miji;
- Kuruhusu ukuaji wa miji wima na sio mlalo ili kuondoa madhara ya kupanuka kwa miji na kumeza maeneo ya vijiji.
- Kuhakikisha taratibu za upangaji wa miji zinazingatia shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwemo pia kilimo na ufugaji ili kuwezesha wananchi wa kada zote kuweza kumudu na kuendesha maisha yao mijini.
- Kuhakikisha kuwa uchukuaji wowote wa ardhi kwa ajili ya kufanikisha mahitaji ya ardhi kwa matumizi ya umma unafanyika kwa mfumo ulio wazi na utakaompa mmiliki anayepoteza ardhi yake maslahi yatakayoboresha hali aliyokuwa nayo mwanzo.
- Kuhakikisha kuwa mchakato mzima wa ukuaji wa miji unakuwa shirikishi katika kila hatua na elimu ya kutosha inatolewa kwa makundi yote ikiwa ni pamoja na wakulima, wafugaji, wanawake, vijana, wazee, walemavu n.k.

### 1.10 UKUAJI WA VIJIJI

**Muktadha:** Kwa muda mrefu dhana ya maendeleo ya vijiji imekuwa ikihusishwa na kuongezeka kwa watu, shughuli na huduma ambapo mwisho wake ni kufikia hatua ya kuwa sehemu ya mji. Nadharia hii imepelekea kupungua kwa ardhi ya vijiji ambavyo hubadilishwa na kuwa sehemu ya miji hivyo kubadili pia mfumo wa umiliki na aina ya shughuli zinazopaswa kufanyika katika maeneo ya mji.

Kwa mujibu wa kifungu cha 7(2) na jedwali la 5 kwenye Sheria ya Mipango Miji ya mwaka 2007 kinaainisha kuwa kijiji ambacho kimeweza kufikia zaidi ya watu elfu kumi, kina kituo cha afya, shule ya sekondari, soko, maduka 20 yaliyosajiliwa, na mahakama ya mwanzo kinapaswa kujumuishwa kuwa sehemu ya mji.

**Changamoto:** Utaratibu huu wa kupandisha ardhi za vijiji kuwa sehemu ya mji sio tu unapunguza ardhi ya kijiji lakini pia una madhara kwa umiliki wa ardhi na shughuli za kawaida zilizokuwa zinatekelezwa kwenye ardhi ya vijiji. Maeneo ya vijiji yanavyopanda hadhi na kuwa miji mfumo wa umiliki hubadilika pia kutoka mfumo wa umiliki kimila ambao hauna ukomo wa muda na tozo za kodi ya ardhi kwenda kwenye mfumo wa umiliki kwa hati ambao una ukomo wa muda wa umiliki na tozo za kodi ya ardhi. Vilevile, mipango miji haizingatii shughuli za asili za matumizi ya ardhi kama vile kilimo na ufugaji badala yake huzingatia zaidi utengaji wa viwanja vya makazi, biashara na maeneo ya matumizi ya umma kama vile shule.

**Mapendekezo:**
- Ili kuweza kuongeza ulinzi wa ardhi ya kijiji ambayo ndio hutegemewa na wazalishaji wadogo ambao ndio sehemu kubwa ya Watanzania nchini, masuala yafuatayo yanapendekezwa;
- Serikali ihakikishe kuwa asilimia 50 ya ardhi yote nchini inaendelea kuwa sehemu ya ardhi ya kijiji na vyovyote vile haitabadilishwa kwa matumizi mengine.
- Nadharia ya maendeleo na ukuaji wa vijiji ijielekeze katika kuboresha huduma na miundombinu iliyopo kijijini bila kulazimu kubadilisha hadhi ya kijiji kuwa mji.
- Vijiji vitambuliwe kuwa vitovu na msingi wa maendeleo kwa kuhakikisha kuwa uwekezaji wa kutosha unafanyika kuwawezesha wazalishaji wadogo kuwa gurudumu la maendeleo nchini.

### 1.11 UPIMAJI WA ARDHI

**Muktadha:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina jukumu la kusimamia na kuwezesha upimaji ardhi na kutayarisha ramani nchi nzima. Sheria ya Upimaji, sura namba 324 ya sheria za nchi inatoa mamlaka ya upimaji ardhi chini ya Idara ya Upimaji na Ramani iliyopo Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Katika ngazi ya Halmashauri, zoezi la upimaji linaratibiwa na Idara ya Ardhi na Maliasili na upimaji wowote utakaofanyika ni lazima uidhinishwe na Idara ya Upimaji na ramani ya Wizara ya Ardhi.

**Changamoto:** Changamoto zinazokabili upimaji wa ardhi ni pamoja na kasi ndogo ya upimaji wa ardhi ukilinganisha na mahitaji ya wananchi hivyo kupelekea uanzishwaji wa makazi holela. Vilevile, yapo matukio ya upimaji ambayo yamesababisha ongezeko la migogoro ya mipaka ya vijiji hii ni kutokana na ushirikishwaji hafifu wa wananchi wakati wa zoezi la upimaji wa mipaka. Pia, kipaumbele kikubwa kwenye upimaji kimewekwa kwenye ardhi ya jumla na hasa kwenye miradi ya viwanja kwa kuwa imekuwa ikitumika kama chanzo cha mapato kutokana na uuzwaji wa viwanja. Hii imesababisha hali ya upimaji wa ardhi za vijijini na hasa suala la utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji kuwa hafifu kwa kuwa haionekani kama chanzo cha mapato huku ikichangia ongezeko la migogoro ya ardhi inayotokana na kukosekana kwa upimaji.

**Mapendekezo:**
- Serikali iwekeze katika upimaji wa ardhi za vijiji ili kupunguza migogoro ya mipaka kati ya vijiji na umiliki wa ardhi kwa mmiliki mmoja mmoja.
- Miradi ya upimaji inayotekelezwa ni sharti izingatie haki za wakazi wa asili kuwa sehemu ya mipango ya upimaji badala ya kulipwa fidia tu na kuondoka au kupewa viwanja vichache.

### 1.12 MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI YA VIJIJI

**Muktadha:** Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina jukumu la kuwezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi na kufuatilia utekelezaji wake. Katika kufanikisha jukumu hilo Sheria ya Mipango Miji na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini zote za mwaka 2007 zimetoa mamlaka za utekelezaji wa mipango ya ardhi chini ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi, Halmashauri za Wilaya, Manispaa na Jiji, pamoja na Halmashauri za Vijiji. Mamlaka hizo zimekuwa zikiratibu na kusimamia utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika ngazi ya Taifa, Kanda, Wilaya na Vijiji ambapo mamlaka ya juu ya usimamizi ni Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini.

**Changamoto:** Pamoja na kuwepo kwa mamlaka hizo za upangaji wa ardhi nchini bado kumekuwepo na changamoto ya kasi ndogo ya utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ukilinganisha na mahitaji halisi. Mpaka kufikia sasa takribani vijiji 2000 kati ya vijiji 12,545 vilivyopo nchi nzima ndio vina mipango ya matumizi ya ardhi. Vilevile kumekuwepo na changamoto ya uwepo wa maslahi binafsi kama vile kutenga maeneo ya uwekezaji, misitu, vyanzo vya maji au maeneo ya hifadhi pekee hivyo kupelekea kuwepo kwa mipango ambayo haikidhi mahitaji ya wanavijij kwa kuwa haizingatii mahitaji yao halisi.

Halikadhalika, asilimia kubwa ya mipango iliyotekelezwa haijafikia hatua ya mwisho ya mipango kina ambayo inaainisha matumizi ya kina ya kila eneo. Hii imesababisha mipango hiyo ya matumizi ya ardhi kutozingatiwa na wanavijiji kwa kuwa hawaoni manufaa ya moja kwa moja katika kuboresha matumizi yao ya ardhi.

**Mapendekezo:**
- Serikali iboreshe mfumo wa uratibu wa mipango ya matumizi ya ardhi ili kufanikisha upatikanaji wa taarifa zenye muunganiko kutoka ngazi ya kijiji, wilaya, mkoa na Wizara.
- Serikali iweke juhudi za makusudi kuwezesha vijiji vyote kufanyiwa mipango ya matumizi ya ardhi ili kupima na kuainisha maeneo ya utekelezaji wa shughuli za kilimo na ufugaji zinazotegemewa na wazalishaji wadogo kuendesha maisha yao ya kila siku.
- Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji unafikia hatua ya mwisho ya kutekeleza mipango kina ili wanavijiji waweze kupata manufaa ya matumizi ya ardhi zao.
- Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Tume ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi iboreshe mchakato wa utekelezaji na usimamizi wa mipango ya matumizi ya ardhi ili kuwepo na mfumo utakaosaidia kuondoa msukumo wa maslahi binafsi ya wadau katika kufadhili mipango ya matumizi ya ardhi za vijiji nchini.

### 1.13 UWEKEZAJI KATIKA ARDHI

**Muktadha:** Katika miaka ya 2000, serikali ya Tanzania ilichukua mrengo wa kutazama uwekezaji katika kilimo cha mashamba makubwa. Mtazamo huu ulichagizwa zaidi na mabadiliko ya kisera kidunia na kikanda. Katika hatua nyingine mpango kama Kilimo Kwanza mwaka 2009 na uanzishwaji wa ukanda wa kusini wa kilimo Tanzania (SAGCOT) ilikuwa miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na serikali katika kukuza uwekezaji nchini. Uwekezaji katika ardhi ya vijiji huchukua mashamba makubwa mchakato ambao hujumuisha ulipaji wa fidia na uhawilishaji wa ardhi kwani mara nyingi wawekezaji hawa hutoka nje ya nchi.

Katika mchakato wa upatikanaji wa ardhi ya uwekezaji wazalishaji wadogo huhusishwa katika mijadala kupitia Mikutano Mikuu ya Vijiji yenye lengo la kupata ridhaa yao. Katika michakato hiyo kumekuwepo na mazingira ya rushwa na utaalamu wa hali ya juu unaowafanya wazalishaji wadogo kutokufikia maamuzi sahihi.

**Changamoto:** Kumekuwepo na changamoto mbalimbali zinazotokana na uwekezaji mkubwa katika ardhi za vijiji ambazo kwa kiasi kikubwa huwaathiri wazalishaji wadogo. Baadhi ya changamoto hizo ni kama zifuatazo;

- Migogoro na wananchi; Katika maeneo mengi yaliyo na uwekezaji wa mashamba makubwa, kumekuwa na migogoro ya mara kwa mara baina ya wazalishaji wadogo na wawekezaji. Hii ni mara tu wazalishaji wadogo wanapobaini kuwa kuchukuliwa kwa ardhi yao kuliwaondolea mamlaka ya kulifanyia maamuzi na pia fidia zilizotolewa haziendani na uhalisia wa thamani ya ardhi iliyochukuliwa.
- Uchukuaji maeneo makubwa kuliko uwezo wa kuyahudumia; Wawekezaji wengi katika maeneo mengi nchini wamekuwa wakichukua ardhi kubwa na kutumia sehemu ndogo tu ya ardhi. Wakati mwingine hutumia ardhi hiyo katika kupata mikopo na kutumia kwa matumizi mengine yasiyoendana na uwekezaji.
- Kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathimini; Kutokana na kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kumesababisha maeneo mengi ya uwekezaji kutokuendelezwa kwa muda mrefu hivyo kuwaathiri wananchi ambao ni wahitaji wa ardhi vijijini.
- Mtazamo potofu wa dhana ya uwekezaji; Mtazamo na mkazo mkubwa wa uwekezaji nchini wakati wote umekuwa ni uwekezaji kutoka nje hasa wa mashamba makubwa. Mtazamo huu umewaweka nje ya mfumo wa uwekezaji wazalishaji wadogo na kutotambulika kwa mchango wao katika kukuza pato la Taifa.

**Mapendekezo:**
- Kuweka sera na sheria zenye mrengo wa kuwekeza rasilimali na uwezeshaji kwa wazalishaji wadogo ambao ni wazalishaji wakubwa wa mazao ya chakula na biashara.
- Kuruhusu uwekezaji wa ubia. Kwa kuwa uwekezaji unaohusisha uhawilishaji ardhi umekuwa na changamoto nyingi, ni muhimu kubadili mtazamo na kuwaweka wazalishaji wadogo kama wabia na wanufaika wa moja kwa moja wa uwekezaji. Hii italeta tija kwa wazalishaji wadogo na serikali.
- Kuwekwa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya maeneo ya uwekezaji kwa lengo la kuhakikisha uwekezaji huo unakuwa na tija kwa wazalishaji wadogo na serikali pamoja na kuongeza uwajibikaji.
- Katika nyakati ambazo itaonekana ni lazima ardhi kuchukuliwa, fidia inayotolewa ijumuishe tathmini za maslahi ya vizazi vilivyopo na vijavyo ili kuleta maendeleo endelevu na kuepusha migogoro ambayo imekuwa ikileta hasara kwa pande zote zinazohusika.
- Kugawa ardhi kulingana na uwezo wa wawekezaji kuyahudumia. Ikiwa ardhi itachukuliwa kwa lengo la kupewa mwekezaji, ni muhimu kuzingatia uwezo wa wawekezaji hao kuihudumia ardhi husika. Vilevile muda unaotolewa kwa ajili ya uwekezaji uzingatie uhalisia wa upatikanaji ardhi na mahitaji ya wazalishaji wadogo.
- Pamoja na sheria kuruhusu vijiji kutoa hati hafifu kwa wawekezaji bado kumekuwepo na ukakasi kwa watendaji wa serikali kutokuruhusu vijiji kutoa hati hafifu. Ni jukumu la serikali kuvijengea uwezo vijiji kuweza kutoa hati hafifu za kimila kwa wawekezaji1
- Wazalishaji wadogo watambulike kama wawekezaji kutokana na mchango wao kwa Taifa.

### 1.14 MFUMO WA TAARIFA ZA ARDHI

**Muktadha:** Moja kati ya malengo ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 ni kuhakikisha kunakuwepo na mfumo thabiti wa kutunza na kusambaza taarifa za masuala ya ardhi. Sera inabainisha kuwa ni muhimu kuwa na mfumo mzuri wa taarifa ili kufahamu kiasi cha ardhi kinachomilikiwa, malengo ya umiliki, na kiasi cha ardhi kilichobaki kwa matumizi na maendeleo ya baadae. Hadi Sera inatungwa taarifa za masuala ya ardhi zilikuwa hazipatikani kwa urahisi na hazikuwa sehemu moja. Kwa mujibu wa Sera taarifa muhimu za ardhi zinazotakiwa kuonekana na kupatikana ni pamoja na mahali ilipo ardhi hiyo, ukubwa wa eneo, muundo wake, majina na anuani za mmiliki, aina matumizi, kodi ya mwaka na malipo yake.

Katika kutekeleza matakwa ya sera ya kuwa na mfumo thabiti wa taarifa za ardhi sheria mbalimbali zilitungwa zikiwemo Sheria za Ardhi Namba 4 na 5 za Mwaka 1999, Sheria ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi, Sheria ya Mipango Miji, Sheria ya Umiliki wa Pamoja, Sheria ya Rehani, Sheria ya Upimaji na Tathmini n.k. Utungwaji wa sheria hizi ulikuwa na lengo la kutatua changamoto zinazotokana na mahitaji makubwa ya ardhi lakini zaidi ni kuangalia ongezeko la mauzo ya ardhi ili kuongeza ukusanyaji wa kodi, uhifadhi duni wa kumbukumbu za ardhi na usimamizi na utawala hafifu wa ardhi.

Ili kukabiliana na changamoto tajwa Wizara ya Ardhi toka mwaka 2002 hadi 2016 imefanya mabadiliko katika mifumo ya utunzaji na utoaji taarifa za ardhi kuwa katika mfumo wa kieletroniki kwa kuja na mifumo mikuu mitatu. Mifumo hiyo ni pamoja na mfumo wa ukusanyaji kodi ya ardhi na utambuzi wa wamiliki ardhi (*Land Rent Management System*), Usajili wa upimaji (*survey registration system*), na mfumo wa kitovuti wa kutunza na kusimamia taarifa za ardhi (*Management of Land Information System-MOLIS*). Kwa zaidi ya miaka 15 toka mifumo hii ilipoanza kufanya kazi mwaka 2002 hadi 2018, mifumo hii imekuwa ikifanya kazi bila kutegemeana na hivyo kutoleta muunganiko wenye tija.

Katika kutambua ukosefu wa mfumo unaounganisha kwa pamoja taarifa za ardhi na kuweka kumbukumbu pamoja, mwaka 2019 – 2020 serikali ilikuja na Mfumo Unganishi wa Kuhifadhi Kumbukumbu za Ardhi (*Integrated Land Management Information System-ILMIS*) na Kujenga Kituo cha Taifa cha Taarifa za Ardhi. Mfumo huu kwa sasa unatumika katika Manispaa za Jiji la Dar es Salam tu ambapo umepunguza muda wa utoaji wa hati kutoka siku 90 hadi 7 pale ambapo mwombaji atawasilisha taarifa zote zinazotakiwa.

**Changamoto:** Tangu mwaka 2002 mifumo hii ilipoanza kubadilika, malengo ya mifumo hii yamekuwa yakilenga ukusanyaji wa kodi za ardhi zaidi kuliko kuangalia haki za ardhi za wazalishaji wadogo. Pia mifumo hii imekuwa ikiangalia zaidi masuala ya utawala ndani ya watendaji wa serikali kuliko utoaji wa taarifa hizo kwa umma. Changamoto nyingine ni pamoja na mifumo hiyo kuangalia tu sehemu ndogo ya nchi hasa Jiji la Dar es Salaam na maeneo ya Majiji zaidi kuliko kuangalia mfumo wa Kitaifa.

Halikadhalika, mifumo hii imekuwa katika lugha ya Kiingereza ambayo haifahamiki kwa wazalishaji wadogo. Mifumo hii pia imekuwa ikitengenezwa kama sehemu ya kutekeleza miradi ya wafadhili ambayo ina ukomo na inapoisha hukosa uendelezwaji.

**Mapendekezo:**
- Kuweka utaratibu wa kutangaza kila baada ya miezi 6 kupitia vyombo vya habari na tovuti ya serikali taarifa za ardhi hususani kuhusu hali ya usimamizi, umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi.
- Serikali itengeneze mfumo wa kidigitali na unaopatikana kwa kila mtu ukionyesha taarifa zifuatazo; hatua za upatikanaji wa hati, majina ya wamiliki wa ardhi, ukubwa wa ardhi, ardhi ya uwekezaji ilipo na migogoro ya ardhi iliyotatuliwa, n.k.
- Serikali kutenga bajeti ya kutosha katika eneo la taarifa za ardhi ili kutotegemea miradi ya ufadhili inayobadilika kutokana na mahitaji ya wafadhili.
- Mifumo ya taarifa za ardhi zote ziwe katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

### 1.1 MFUMO WA UTATUZI WA MIGOGORO YA ARDHI

**Muktadha:** Migogoro ya ardhi inasababishwa na umiliki na matumizi ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali wa ardhi. Migogoro hii inaweza kuwa baina ya wazalishaji wadogo, migogoro ya mipaka ya vijiji na vijiji, hifadhi za wanyamapori na vijiji, wananchi na wawekezaji, migogoro ya wananchi na mamlaka za kiserikali n.k.

Mifumo ya utatuzi wa migogoro huanzia katika ngazi ya kijiji ambapo kuna Baraza la Ardhi la Kijiji, Baraza la Kata katika ngazi ya kata, Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya katika ngazi ya wilaya, kanda au mkoa, Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani katika ngazi ya kitaifa.

Pamoja na uwepo wa mfumo huu bado kumekuwa na migogoro mingi ya ardhi. Mfano, katika bajeti ya Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya 2016/2017 katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Kinondoni na Temeke pekee kulikuwa na mashauri 3,149 kati ya hayo mashauri 1,692 yalikuwa mashauri mapya.

**Changamoto:**
- Uhaba wa Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya; Kati ya Wilaya 139, kumekuwa na Mabaraza 55 pekee yanayofanya kazi hivyo kushindwa kuwahudumia wadawa kwa wakati. Hii ni kutokana na kuwa wananchi hulazimika kusafiri umbali mrefu kufuata haki. Pia kutokana na uchache huo, Mabaraza haya yameelemewa na mashauri kiasi cha kushindwa kutoa maamuzi mapema.
- Rushwa; mfumo huu wa utoaji haki umekuwa ukilalamikiwa kwa kugubikwa na rushwa na hivyo kusababisha watu kukosa haki kwa wakati.
- Uwezo mdogo wa wajumbe wa mabaraza ya chini; Mara nyingi wajumbe wa Baraza la Ardhi la Kijiji na Baraza la Kata wamekuwa hawawezeshwi katika kufahamu vyema taratibu za utekelezaji wa majukumu yao hivyo kusababisha kupoteza haki za wadawa.
- Uhaba wa rasilimali fedha; Mabaraza ya ardhi kwa muda mrefu yamekuwa yakikabiliwa na ukosefu wa rasilimali fedha na hivyo kushindwa kujihudumia na kuchelewesha utoaji haki.
- Mwingiliano wa kiutawala; Kwa kuweka mfumo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi chini ya mhimili wa serikali kumevunja misingi ya kikatiba ya utengano wa kiutawala. Jambo hili limesababisha matatizo kwa wajumbe wa Mabaraza kukosa uhuru wa kufanya maamuzi kwa haki ama kuingiliwa na watendaji wa serikali wakati wa kuendesha mashauri. Jambo hili ni kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia ni kinyume na mapendekezo yaliyowekwa katika Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 iliyopendekeza Wizara ya Ardhi kutojihusisha na utatuzi wa migogoro ya ardhi

**Mapendekezo:**
- Ikiwa mfumo wa Mabaraza utaendelea kutumika ni vyema Mabaraza haya yaanzishwe kila wilaya ili kuwakaribia wananchi na kupunguza gharama za kutafuta haki na pia kupunguza mzigo wa Mabaraza katika kupokea na kuamua kesi.
- Ni muhimu kufanya mabadiliko ya mfumo na kuuweka chini ya mfumo mmoja wa kimahakama ili kuondoa mwingiliano wa kimamlaka.
- Inapendekezwa kuweka mifumo ya kushughulika na maadili ya wajumbe na Wenyeviti wa Mabaraza pamoja na mambo mengine ili kuondoa mazingira yanayosababisha utoaji na upokeaji rushwa.
- Kuwekwa kipaumbele katika kuwezesha mabaraza kifedha ili yaweze kujihudumia na kuondoa mianya ya rushwa.
- Kwa mamlaka zinazohusika kuweka mfumo mzuri wa kuwajengea uwezo wajumbe wa Mabaraza ya Ardhi mara tu wanapochaguliwa na kuthibitishwa.

### 1.15 TATHMINI NA UFUATILIAJI WA MASUALA YA ARDHI

**Muktadha:** Mfumo wa tathmini na ufuatiliaji wa masuala ya ardhi nchini Tanzania haujawekwa bayana katika Sera ya Ardhi ya mwaka 1995 wala sheria zake. Ingawa mfumo huu haupo bayana katika sera wala sheria, ni vyema kuangalia kuwa hata sheria na sera hizo ni zao la matokeo ya Tume ya Rais ya masuala ya ardhi iliyoundwa mwanzoni mwa miaka ya 1990 ambayo ilizunguka nchi nzima kuangalia mfumo wa utawala, umiliki na migogoro ya ardhi nchini. Taarifa ya Tume imeangalia kwa kutathmini tulipotoka, tulipo na kupendekeza masuala muhimu katika sekta ya Ardhi. Hivyo ni sahihi kusema kuwa tathmini ya kwanza ya masuala ya ardhi nchini ilifanywa na Tume ya Shivji.

Pamoja na Sera kutokuwa na mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ulio bayana katika sekta ya ardhi, kumekuwa na aina mbalimbali za ufuatiliaji na tathmini toka 1995 hadi 2016 kama vile mpango mkakati wa utekelezaji wa sheria za ardhi wa mwaka 2005, uboreshaji wa mfumo wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na usambazaji wa taarifa za ardhi na mapendekezo ya rasimu ya Sera ya Taifa ya Ardhi. Katika ngazi ya kimataifa kumekuwa na mabadiliko katika nyanja za ardhi ambapo jumuiya ya kimataifa imepitisha malengo ya maendeleo endelevu 2030 ambayo yameweka malengo katika masuala ya ardhi na ambayo nchi zote zitatakiwa kutoa taarifa. Hivyo basi, ni muhimu kwa serikali kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kama sehemu muhimu katika utekelezaji wa kazi na miradi mbalimbali katika sekta ya ardhi kama inavyopendekezwa hapa chini;

**Mapendekezo:**
- Kuwepo na mfumo wa kudumu wa kuhakikisha kuwa Mikutano Mikuu ya Vijiji inakuwa na ajenda ya kudumu ya ardhi ili kuweza kufuatilia masuala mbalimbali ya ardhi.
- Kuwepo na mawasiliano ya moja kwa moja baina ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu juu ya usimamizi wa ardhi.
- Kuwepo na mikutano ya mara kwa mara katika ngazi ya Taifa inayowaleta wadau wote kwa pamoja katika sekta ya Ardhi ili kujadili na kufuatilia maendeleo katika sekta.
- Itengwe bajeti kutokana na vyanzo vyake vya ndani ili kuhakikisha kuwa mipango ya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera na Sheria za Ardhi inafanyika.
- Mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya masuala ya ardhi utengenezwe kwa njia shirikishi ili uweze kuunganisha ngazi zote kuanzia vijijini hadi Taifa.

### HITIMISHO

Kwa ujumla haya ndio madai ya wazalishaji wadogo katika sekta ya ardhi ambayo yakifanyiwa kazi na kutatuliwa ipasavyo yataondoa changamoto zinazokwamisha uzalishaji mali katika kukuza uchumi wao na wa taifa kwa ujumla. Madai haya yanagusa mahitaji ya muda mrefu kuhusu usimamizi wa ardhi, ukuaji wa miji, uendelezaji wa ardhi ya vijiji, haki za ardhi za wanawake na walemavu, uwekezaji katika ardhi za vijiji, mipango ya matumizi ya ardhi, utatuzi wa migogoro ya ardhi, upimaji wa ardhi, utoaji wa taarifa na masuala ya ufuatiliaji na tathmini.

---

1 ***Kifungu cha 32 cha Sheria ya Ardhi ya Kijiji namba 5 ya mwaka 1999***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wananchi waulize maswali wagombea

**WAGOMBEA** mbalimbali wa udiwani, ubunge na urais kupitia vyama vya siasa wameanza kampeni za majukwani, wakiwaomba kura wananchi kwa ajili ya uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Kuna wagombea husuan wa ubunge na udiwani ambao wanagombea kwa mara ya kwanza na wengine ni zaidi ya mara moja, kwa maana sio wageni kwa wananchi kwa kuwa waliwahi kuwachagua na kuwawakilisha katika vyombo vya kufanya maamuzi (Bunge na Mabaraza ya Madiwani).

Kwa hiyo wagombea ubunge na udiwani kila mmoja anahitaji kura za wananchi ili aweze kuipata nafasi anayoisaka, na baada ya uchaguzi awawakilishe. Wabunge na madiwani jukumu lao ni kwenda kuwasemea wapigakura wao ili wapelekewe maendeleo; kwa maana ya kupatiwa huduma bora za afya, maji, elimu, barabara, madaraja, umeme na mengineyo.

Wabunge na madiwani kadhalika wana jukumu la kuwasilisha kero za wananchi kuhusiana na mambo mbalimbali kwa vyombo husika ili zipatiwe ufumbuzi.

Kwa hiyo kila anayegombea nafasi hizo lazima atambue kuwa wananchi hawamchagui tu kwa kumpendezesha, bali ana wajibu wa kuyatekeleza haya ili waliomchagua wapate maendeleo kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kisiasa.

Kwa kuwa wamejitokeza watu mbalimbali kugombea nafasi hizo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu, ni wakati mwafaka sasa kwa wananchi kuwasikiliza kuhusu hoja wanazozitoa husuan ahadi kwao watakazozitekeleza kwa kipindi cha miaka mitano ikiwa watachaguliwa. Wananchi wana wajibu wa kwenda katika mikutano ya kampeni kwa ajili ya kuwasikiliza kwa umakini na mwishowe kuamua ni wagombea gani wameonyesha kuwa na sifa zote kisha wawape ridhaa ya kuwatumikia kupitia sanduku la kura Oktoba.

Hata hivyo, tunaona kuwa kuwasikiliza tu bila kuwauliza maswali wagombea hakutoshi. Jambo tunalolishauri ni kuwa wapigakura nao wana haki ya kupewa fursa ya kuwauliza maswali wagombea hao, ili watoe ufafanuzi na maelezo kuhusiana na baadhi ya hoja na ahadi zao.

Hili ni muhimu kwa kuwa kuna ahadi na hoja zingine ambazo wagombea wanazitoa, lakini zinaacha maswali kadhaa magumu bila kuwapo majawabu.

Jambo la kusikitisha ni kuwa vyama vya siasa nchini haviweki utaratibu wa kuwapa fursa wananchi kuwauliza maswali wagombea wao kwenye mikutano ya kampeni majukwaani, kitu ambacho hakina tija na ni kutowatendea haki wananchi.


Vyama hivyo vimejenga utamaduni mbaya wa kuweka ulinzi kwenye mikutano yao, kiasi kwamba mtu yeyote akitaka kuuliza maswali, hujikuta katika wakati mgumu, ikiwamo kupigwa kwa kutuhumiwa kuwa ametumwa kuvuruga mkutano husika.

Kwa kuwa maeneo ya majukwaa ya mikutano ya hadhara ya kampeni siyo rafiki kwa wapigakura kuuliza maswali, tunazishauri taasisi kuandaa midahalo kwa ajili ya wagombea kujieleza kisha kuulizwa maswali na wananchi, tukiamini kuwa wapigakura watawajua vyema wagombea hao kabla ya kuamua nani wamchague.

Utaratibu huu sio mpya nchini. Mwaka 1995 gazeti moja nchini liliandaa mdahalo wa wagombea urais Benjamin Mkapa (CCM), Augustine Mrema (NCCR-Mageuzi) na John Cheyo (UDP) walishiriki, na hakika uliwasaidia sana wapigakura kuwafahamu kwa undani kabla ya kufanya maamuzi.

Kadhalika, mwaka 2010 midahalo mingine iliandaliwa na taasisi moja ya serikali ngazi ya ubunge katika majimbo mbalimbali nchini na kwa hakika ilivutia wengi na kuwawezesha wananchi kuwafahamu wagombea. Kupitia midahalo hiyo, wananchi watawauliza waliokuwa viongozi kwa nini hawakutekeleza waliyowaahidi na wengine kuhojiwa kwa nini kwa kipindi chote cha miaka mitano hawakuonekana kwenye majimbo au kata.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Tunapomtua mama ndoo kichwani, tutupe jembe la mkono kwa mkulima

Na Sabato Kasika

**KUNA** mikakati mingi ya kuboresha maisha ya Watanzania ikiwamo kuhakikisha upatikanaji wa maji salama unaojulikana kama kumtua mama ndoo ya maji kichwani. Vivyo hivyo uwepo mwingine wa kumwondolea mkulima jembe la mkono. Ni muhimu na taifa linahitaji jitihada za dhati za kuondoa kilimo kinachotegemea zana hiyo duni katika karne ya 21 ya sayansi na teknoloji.

Bajeti ya Wizara ya Kilimo ya mwaka 2020/2021 ilipewa Shilingi bilioni 229.8, huku vipaumbele vyake takribani kumi vikilenga kuimarisha usalama wa chakula na malighafi za viwandani. Pamoja na hayo kuna haja ya kuweka mkakati wa kumtua mkulima jembe la mkono na kumwezesha kuachana na kilimo cha kutegemea mvua.

Kuna umuhimu kwa kuwa kilimo kinatajwa kama uti wa mgongo wa taifa, kutokana na ukweli kwamba, asilimia takribani 70 ya Watanzania wamejikita katika sekta hiyo na ndiko kuliko na ajira nyingi.

Lakini kilimo chao ni cha kutumia jembe la mkono, huku wengine wakijaribu la kukokotwa na ng'ombe (plau) na kuna wachache wanaotumia trekta.

Hali hiyo inaonyesha wazi kwamba, dhana ya kilimo ni uti wa mgongo wa taifa inahitaji kupewa uzito zaidi, kwa kumwezesha mkulima kutumia trekta katika kilimo na pia kiwe na umwagiliaji.

Ikumbukwe kuwa mabadiliko ya tabianchi, yanachangia kwa kiasi kikubwa kukwamisha wakulima, kwa kuwa wanaweza kulima halafu mvua zisinyeshe, lakini kilimo cha umwagiliaji kinaweza kukabiliana na hali hiyo.

Hivyo, kauli za kilimo ni uti wa mgongo wa taifa, siasa ni kilimo, kilimo kwanza na nyingine nyingi, zisaidie kubadilisha kilimo cha Tanzania na kuwatoa wakulima katika mazingira ya sasa ili wafikie hatua nzuri.

Nikirejea vipaumbele vya wizara ya kilimo ni vinavyotajwa kwenye bajeti ya mwaka huu ni pamoja na kuendelea na kutekeleza progamu ya kuendeleza sekta ya kilimo awamu ya pili (ASDP II), inayolenga kuimarisha vyuo na vituo vya mafunzo na utafiti vya kilimo.

Vingine ni udhibiti wa visumbufu vya mimea, huduma za ugani, usajili wa wakulima na bima ya mazao, kuboresha mifumo ya kitaasisi, bodi na sheria za kilimo kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya mazao ya kilimo.

Aidha, wizara pia inatarajia kuunganisha wakulima wadogo na mashamba makubwa ili kuendeleza kilimo cha kibiashara na itawapa ujuzi na maarifa ya kilimo chenye tija, kurahisisha upatikanaji wa huduma za pembejeo na masoko, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji.

Halikadhalika itasimamia ujenzi wa maghala, masoko na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo, kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao na upatikanaji wa pembejeo na kuzisambaza kwa wakulima ili kuongeza tija kwenye uzalishaji.

Maeneo mengine yatakayopewa kipaumbele ni kuimarisha usimamizi wa maendeleo ya ushirika na kuweka mifumo itakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wanaushirika na wadau wengine wa sekta ya kilimo.

Wizara pia itaongeza matumizi ya teknolojia bora katika uzalishaji wa mazao na tija, kuimarisha vituo vya utafiti, vyuo vya mafunzo na vituo vya mafunzo kwa wakulima kwa kujenga miundombinu wezeshi na kuboresha maarifa na ujuzi kwa watafiti, wakufunzi na wazalishaji kwa lengo kukuza kilimo.

Waziri anasema, ili kuhakikisha ardhi inatumika vizuri na katika mwaka 2020/21 wataimarisha huduma za upimaji wa matabaka na ubora wa udongo kwa ajili ya kuendana na mahitaji ya mazao ya kilimo kimaeneo.

Hivyo ndivyo vipaumbele vya bajeti ya wizara hiyo ambavyo vinatajwa bungeni wakati wa kuwasilisha makadirio ya bajeti bungeni Dodoma.

Lakini kinachoonekana ni kwamba bejeti ya wizara hiyo imepungua kidogo kuliko ya mwaka uliopita kwa kuwa imetoka Sh. bilioni 253.8 mwaka 2019/2020 hadi Shilingi bilioni 229.8.

Lakini pamoja na vipaumbele hivyo ni muhimu kuwekeza katika miradi ya kimkakati ya kuzalisha chakula kingi ili kuondoa uhaba wa chakula nchini, hatua inayoweza kufikiwa kwa kumchomoa mkulima kwenye jembe la mkono na la kukokotwa na ng'ombe na kukifanya kilimo kisiwe cha kutegemea mvua ambayo zama hizi inaathiriwa na mabadiliko ya tabia nchi.



Mgombea mwenza wa kiti cha urais kwa tiketi ya CCM, Makamu wa Rais Samia Suluhu Hassan, akisalimia umati wa wanachama wa chama hicho, kijiji cha Kiwangwa, wilayani Bagamoyo mkoani Pwani jana, akiwa njiani kuelekea Bagamoyo Mjini kwa ajili ya kuhutubia mkutano wa kampeni za uchaguzi mkuu. **PICHA: OMR**

# Samia aahidi neema maji vijiji vyote

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MGOMBEA mwenza wa urais Chama Cha Mapinduzi (CCM), Samia Suluhu Hassan, amesema wananchi wa vijiji vyote katika Jimbo la Chalinze, watafikiwa na huduma ya maji iwapo chama hicho kitachaguliwa tena katika uchaguzi mkuu ujao. Sambamba na huduma hiyo, sekta za elimu na afya zitaimarishwa zaidi nchini kote na kuwa katika kiwango cha juu.

Samia alitoa ahadi hiyo jana wakati akiongea na wananchi wa Chalinze katika mkutano wake wa kampeni kuomba ridhaa kwa wananchi waendelee kukiamini chama hicho na kuwachagua kwa mara nyingine.

Alisema viko vijiji ambavyo havijafikiwa na huduma ya maji ambavyo katika awamu ijayo vitasambaziwa huku akiwasihi waliopata huduma hiyo, kulipa bili kwa wakati ili Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) iendelee kuboresha huduma zake.

Kuhusu elimu, Samia alisema endapo wananchi watawapatia ridhaa, pamoja na kuendelea kuboresha sekta hiyo, pia wale walioikosa watafikiwa kwa mfumo wa MEMKWA (Mpango wa Elimu Maalum kwa Walioikosa).

Samia alisema, watahakikisha ujenzi wa barabara ya Pangani-Mkange - Makurunge kilomita 178 itajengwa kwa kiwango cha lami na wananchi watalipwa fidia.

Alisema katika awamu ijayo, ujenzi wa viwanda utaendelea kupewa kipaumbele ili kutoa ajira 8000 kupitia sekta hiyo. Aliwaomba wananchi kuwachagua wagombea wa chama hicho ili kuendeleza yale waliyoyaanzisha na kumalizia miradi ya maendeleo.

Naye Rais mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete, aliwataka wananchi kutotishika na maneno ya wapinzani kwa kuwa kazi yao si kusema yale yaliyofanywa na serikali bali ni kutafuta sehemu ambayo ina kasoro na kukosoa.

"Maneno ya watani yasiwanyime usingizi, yasiwakatishe tamaa mkadhani mambo ni mabaya.

Hawawezi kuwasifia, kazi ya kujisemea yaliyofanywa na serikali ni yetu ambayo imefanyika sana," alisema Kikwete. Alisema wanachama wa CCM wanatakiwa kuendelea kufanya kazi ili mgombea urais, wabunge na madiwani wapate kura nyingi kwa asilimia 90 au zaidi kwa kuwa yako mambo mengi yamefanyika, hivyo inahitajika ridhaa kwa awamu nyingine kuyaendeleza.

Mgombea ubunge Jimbo la Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alisema iko miradi mingi ya maendeleo iliyofanywa na serikali ya awamu ya tano, hivyo wananchi wanatakiwa kuwachagua wagombea wa CCM ili waendeleze kazi waliyoianza.

Ridhiwani alisema katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, zahanati 38 zimejengwa pamoja na vituo vya afya vitatu, huku vituo viwili ambavyo vilikuwa havifanyi kazi vimeboreshwa na sasa vinatoa huduma.

# Mwandishi ITV afariki dunia ghafla

**Na Mary Geofrey**

MWANDISHI wa habari na mtangazaji wa Kituo cha Televisheni cha ITV, Agnes Almasy, amefariki dunia ghafla jana mchana jijini Dar es Salaam, wakati akiwahishwa hospitali.

Baba mzazi wa Agnes, John Almasy, alilieleza Nipashe jana kuwa, binti yake alifariki dunia muda mfupi kabla ya kufikishwa Hospitali ya Amana, baada ya kujisikia vibaya akiwa nyumbani kwake Buguruni akijiandaa kwenda kazini.

Alisema akiwa nyumbani kwake, alianza kujisikia maumivu makali ya kichwa ndipo alimpigia simu mumewe na kumweleza, hivyo alimshauri ajimwagie maji ya baridi ili kupooza hali hiyo.

Almasy alisema wakati Agnes akiendelea kuongea na mumewe, alidai kuendelea kujisikia vibaya na ghafla alishindwa kuendelea kuongea na simu na kuitupa chini.

"Kwa sababu alikuwa yupo na dada wa kazi, alituambia alivyotupa simu chini alianguka na kuanza kutoa mapovu mdomoni," alisema Almasy.

Aliendelea kueleza kuwa baada ya mumewe kuona amekata mazungumzo, alipatwa na mshtuko, hivyo kumpigia simu kumfahamisha hali hiyo, ndipo walipanga wote kumuwahi nyumbani kwa ajili ya kumpeleka hospitali.

Alisema wakiwa njiani, mama mzazi wa Agnes aliwahi nyumbani kwa binti yake na kumchukua kwa gari kumpeleka hospitali.



"Walipofika hospitali na mimi nikaingia pale, daktari alimpokea vizuri na kumpima ndipo akasema mbona huyu ameshafariki, basi tukawa hatuna la kusema tena," alisema Almasy.

Alisema mtoto wake huyo wa pili, hakuwahi kuwa na historia ya kuugua kichwa wala ugonjwa wa shinikizo la damu (BP), bali ni hali iliyomtokea ghala na kuwashtua.

Kuhusu taratibu za msiba, alisema zinafanyika nyumbani kwa Agnes Buguruni, na kwamba wanashirikiana na familia ya mume wake kupanga watamzika wapi na lini.

Agnes alifunga ndoa Februari 22, mwaka huu, ameacha mume na mtoto mmoja. **Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.**

# Kagera waombwa kuichagua CCM

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya wagombea ubunge katika majimbo ya mkoa wa Kagera kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), wamewaomba wananchi kuwachagua wagombea wa CCM ngazi za udiwani, ubunge na urais, ili washirikiane kutatua changamoto zinazowakabili wananchi ikiwamo za afya, elimu, maji na barabara.

Akizungumza katika uzinduzi rasmi wa kampeni za chama hicho mkoa wa Kagera, uliofanyika katika uwanja wa Uhuru, Manispaa ya Bukoba, mgombea wa Viti Maalum, Bernadetha Mushashu, alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali imewajengea hospitali tatu za wilaya.

"Serikali ya Rais (John) Magufuli imewajengea pia vituo vya afya 14 vyenye wodi za watoto, wajawazito na vyumba vya upasuaji. Pia imejenga chuo cha kisasa cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) na kukarabati shule kongwe za Rugambwa, Kahororo na Ihungo, lengo mpate huduma karibu, lakini watoto wetu wapate elimu bora," alisema.

Naye Regina Zachwa pia wa Viti Maalumu, alisema CCM inatambua mchango wa wabunge wanawake katika kuwaletea maendeleo wananchi kutokana na kufanya kazi kwa karibu zaidi na wananchi. "Wabunge wanawake ni injini katika kuwaletea wananchi maendeleo. Alipo mwanamke maendeleo ni lazima ndiyo maana CCM inatoa nafasi za uongozi na utendaji wao kutokana na kuaminika, kuwa wabunifu na uwezo wa kusimamia raslimali za wananchi kwa maendeleo endelevu," alisema.

Mgombea wa ubunge Bukoba Mjini, Steven Byabato, alisema maendeleo ya Jimbo la Bukoba yalisuasua kutokana na Rais kukosa kiunganishi cha moja kwa moja ambacho ni mbunge wa CCM na kuwataka wananchi kumchagua ili iwe rahisi kufikisha matatizo yao na kuwapatiwa ufumbuzi haraka.

"Mheshimiwa Rais alikosa mnara mzuri wa mawasiliano. Sasa msikosee tena katika uchaguzi huu, mchagueni mgombea wa CCM ili kupitia ilani yake ya mwaka 2020 hadi 2025 changamoto zetu zitatuliwe na kupata maendeleo endelevu," alisema.

# Wenje abainisha vipaumbele Rorya

**Na Timothy Itembe,**
RORYA

MGOMBEA ubunge katika Jimbo la Rorya kupitia Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Hezekiah Wenje, amesema kama atachaguliwa kuwa mbunge, atahakikisha kila shule ya sekondari inakuwa na hosteli ya wasichana ili kuepusha mimba zisizotarajiwa.

Wenje alisema hayo jana wakati akiomba kura kwenye mkutano wa hadhara wa kampeni za uzinduzi wa kampeni katika Kata ya Rablwo.

"Kama wananchi mkinichagua, nitahakikisha kila shule ya sekondari wilayani hapa inakuwa na hosteli na kwa kufanya hivyo, tatizo la ujauzito kwa wanafunzi litakuwa historia," alisema.

Mgombea huyo alisema wananchi wa Rorya hawana budi kumwamini na kumchagua kuwa mbunge wao ili kuwatumikia na kuwaletea maendeleo katika jimbo hilo.

Alisema pamoja na kuanza na hosteli za wasichana, atahakikisha miundombinu ya barabara inaboreshwa na wananchi wanasafiri kwa raha na kwa gharama nafuu.

Naye mgombea udiwani wa Kata ya Kitembe kupitia CHADEMA, Thomas Rissa, alimwomba mgombea huyo kuwasaidia watu wa Rorya kuondokana na wizi wa mifugo endapo atachaguliwa kuwa mbunge wao.

Rissa aliongeza kuwa anatetea nafasi yake katika kata hiyo na kuwa wakati akiwa diwani alipambana na wizi wa mifugo na watu wa Rorya kwa sasa wana ahueni wanalala licha ya kuwa bado kuna harufu ya wizi wa mifugo.

Aliongeza kuwa wakati akipambana na wizi wa mifugo, wakati mwingine alitumia gharama zake kuhakikisha watuhumiwa wanakamatwa na kufikishwa eneo husika pamoja na mifugo iliyoibwa inapatikana na kurudishwa kwa wenyewe.

# CCM yasema urais si kuvaa suti

**Na Thobias Mwanakatwe**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimezindua kampeni zake katika Jimbo la Rungwe, huku kikisema kipindi hiki si cha watu kuvaa suti na kuutaka urais bali anatakiwa kiongozi mwenye hofu ya Mungu anayeweza kusimamia taifa.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Jacob Mwakasole, alisema hayo jana wakati wa uzinduzi wa kampeni zilizofanyika Kata ya Mpuguso kwa ajili ya kumnadi mgombea urais kupitia chama hicho, Rais Dk. John Magufuli, na mgombea ubunge Jimbo la Rungwe, Antony Mwantona.

"Rais si zawadi ya kuwasaidia watu na kusema unajua mimi nilikuwa naumwa kwa hiyo nichagueni. Tunataka Rais mwenye hofu ya Mungu na mwenye uwezo wa kusimamia taifa hili," alisema.

Mwakasole alisema CCM ndicho chama pekee ambacho kiliingia mkataba na wananchi mwaka 2015 kwa ajili ya kuwaletea maendeleo, na mambo yote yamefanyika kwa ufanisi mkubwa. "Mtanzania wa leo anaweza kupanga jambo kesho na kesho kutwa. Sehemu nyingine hawapangi sababu hakuna amani," alisema Mwakasole.

Alisema ikifika Oktoba 28, mwaka huu, wananchi wachague Rais kutoka CCM, wabunge wa CCM na madiwani wa CCM ili waendelee kuwaletea maendeleo na kudumisha amani na utulivu.

Kwa upande wake, Mwantona alisema uongozi unapangwa na Mungu na kuwaomba wagombea wenzake 44 aliogombea nao kumuunga mkono ili CCM kuibuka na ushindi.

"Mungu amenipa miaka mitano niwatumikie wana Rungwe. Namwomba Mungu ili utumishi wangu uwe uliotukuka," alisema Mwantona.

Aliyekuwa Mbunge wa Rungwe, Amon Sauli, alisema wana CCM waungane ili kuhakikisha chama kinapata ushindi wa kishindo kwa nafasi ya Rais, ubunge na madiwani.




Wafanyabiashara wa nyanya wakipanga bidhaa hiyo, wakati wakisubiri wateja katika soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. Tenga moja la nyanya limeshuka bei kutoka 35,000/- hadi 15,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ulega ajinasibu kujenga chuo cha VETA

**Na Julieth Mkireri,**
MKURANGA

MGOMBEA ubunge Jimbo la Mkuranga, Abdallah Ulega, amesema atamwomba Rais John Magufuli kujenga chuo cha ufundi ili vijana wakidhi vigezo vya kupata ajira katika viwanda vilivyoko wilayani hapa.

Ulega aliyasema hayo juzi wakati wa uzinduzi wa kampeni katika jimbo hilo na kubainisha kuwa kwa sasa kuna zaidi ya viwanda 90 kutoka 20 ambavyo vilikuwapo mwaka 2015.

Alisema ili nafasi za ajira zisichukuliwe na wageni, ni vyema kukawa na chuo cha ufundi ili vijana wapate ujuzi utakaokidhi kupata ajira za kuwakwamua na umaskini.

Ulega aliwaomba wakazi wa Mkuranga kumpa ridhaa ya kuongoza kwa miaka mitano ijayo, ili aendeleze miradi ya maendeleo ambayo bado haijakamilika katika jimbo hilo. "Naomba mumpe kura Rais John Magufuli, mimi niwe mbunge wenu na madiwani wote wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) tukasimamie maendeleo ya wana Mkuranga, tukamalizie miradi ya maendeleo ambayo mingine tumeianza kuitekeleza," alisema.

Pia alisema endapo wananchi watamchagua, atamfikishia Rais kero ya miundombinu ili wilaya ipate bajeti ya kutosha kujenga na kukarabati kila eneo kufikika kirahisi bila kujali kipindi cha jua na mvua.

Awali, akifungua kampeni hizo, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Gaudensia Kabaka, aliwataka wananchi kuwachagua wagombea wa CCM ili waendeleze miradi waliyoianzisha.

Kabaka, alisema wananchi wanatakiwa kuwa makini kwa kuwa wakichanganya vyama hakuna jambo la maendeleo litakalofanyika. Mgombea udiwani wa Kata ya Magawa, Juma Abeid, alisema CCM katika Wilaya ya Mkuranga imejipanga kushinda kwa kishindo kuanzia ngazi ya udiwani hadi Rais kutokana na mambo ya maendeleo yaliyofanywa ikiwamo la ujenzi wa vituo vya afya 40 ambavyo vitaondoa kero ya upatikanaji wa huduma za afya.

# Kampeni kutibu wagonjwa wa TB yaanza

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

MAOFISA tabibu wa kitengo cha kifua kikuu (TB) na ukoma wa Hospitali ya Serikali ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma, wameanza kampeni ya kuwafuatilia watu waliobainika kupata ugonjwa wa kifua kikuu na kuanzishiwa dawa.

Lengo ni kuhakikisha wanakuwa na ufuasi mzuri wa matumizi ya dawa kadri ya maelekezo waliyopewa na wataalamu hao.

Kwa mujibu wa wataalamu hao, kampeni hiyo ni sehemu ya mikakati ya Wilaya ya Tunduru ya kuunga mkono jitihada za Wizara ya Afya na Shirika la Afya Dunia (WHO) ya kutokomeza TB ifikapo mwaka 2030.

Kutokana na hali hiyo, hivi karibuni Wilaya ya Tunduru ilizindua kampeni ya uelimishaji, uchunguzi na upimaji wa TB iliyowashirikisha waganga wa tiba asili nyumba kwa nyumba na shule kwa shule ambayo inakusudia kuwafikia wananchi wote katika wilaya hiyo.

Mratibu wa TB na ukoma wa Wilaya ya Tunduru, Dk. Mkasange Kihongole, alisema katika kampeni hiyo wataalamu wa kitengo cha TB watamfikia kila mgonjwa aliyebainika kuwa na ugonjwa huo na kuanzishiwa dawa. Alisema watakaobainika kukatisha kunywa dawa wataendelea kupewa elimu juu ya umuhimu wa matumizi ya dawa za TB pamoja na madhara yanayoweza kupatikana kwa mgonjwa kupuuzia matumizi yake.

Alisema mkakati mwingine kwa wagonjwa ambao wamekatisha dawa ni kuwashirikisha viongozi wa serikali wakishirikiane na wahudumu wa afya ngazi ya jamii kwenya maeneo waliopo ili waweze kutoa msaada wa kuwafuatilia wakati wa matumizi ya dawa kwa wagonjwa hao.

Alisema katika utekelezaji huo Hospitali ya Wilaya ya Tunduru imepewa lengo la kuwaibua wagonjwa 647 katika mwaka 2020, ambapo kila robo ya mwaka inatakiwa kupata wagonjwa 161.

Alisema hata hivyo katika robo ya kwanza ya Januari- Machi 2020 wamepata wagonjwa 180 sawa na asilimia 111 na wamevuka lengo la makadirio walilopewa kulitekeleza.

Alisema katika utekelezaji wa majukumu hayo katika robo ya pili ya Aprili ya mwaka iliyoanzia Juni, hadi kufikia Mei 30, 2020 tayari wamepata wagonjwa 102 na wanaamini kupitia kampeni hiyo na mapambano wanayoendelea watafanikiwa kuvuka lengo walilopewa la kupata wagonjwa 161 kwa kila robo.

Mmoja wa wagonjwa wa TB mkazi wa kijiji cha Nakapanya, Kata ya Nakapanya ambaye alipata ugonjwa kisha kukimbilia shambani ili asiendelee kutumia dawa, ameitaka jamii kutopuuza ugonjwa huo na kuhakikisha wanapata matibabu haraka pindi wanapobainika kupata ugonjwa huo. Mashono ambaye ana familia ya wake wawili na watoto wanane alisema, alipata maambukizi ya ugonjwa huo mwishoni mwa mwaka jana, lakini alichukua uamuzi wa kukimbilia shambani ili asijulikane hadi kitengo cha TB Hospitali ya Wilaya ya Tunduru ilipomwibua na kumwanzishia dawa kwa lazima.



Hakimu Mkazi Mfawidhi Wilaya ya Mufindi, Maua Hamduni (kulia), akifafanua jambo juu ya masuala ya mirathi kwa wananchi wa Kijiji cha Igoda, Kata ya Luhunga, wilayani humo, mkoani Iringa jana, ikiwa ni sehemu ya kampeni ya kupinga udhalilisha na aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto, inayowezeshwa na Halmashauri ya Wilaya Mufindi, kampuni ya chai ya Unilever na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na masuala ya wanawake (UN WOMEN). **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Tabora yakusanya mapato asilimia 73

**Na Tiganya Vincent,** NZEGA

HALMASHAURI za Mkoa wa Tabora zimefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 17.6 sawa na asilimia 72.89 makisio ya shilingi 24.1 kutoka kwenye vyanzo vya mapato ya ndani kwa mwaka wa fedha uliopita.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu Tawala Mkoa wa Tabora, Msalika Makungu, wakati akifungua kikao cha siku moja cha tathmini ya utendaji kazi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa mwaka wa fedha 2019/20. Alisema halmashauri zote zilipaswa kukusanya na kufikia lengo la asilimia 80.

Makungu alisema kuwa Halmashauri ya Mji wa Nzega ndio inaongoza kwa kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 1.7 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 1.9, Kaliua imekusanya bilioni 3.1 kati ya lengo kukusanya shilingi bilioni 3.8, Sikonge inafuatia kwa kukusanya bilioni 2.3 kati ya lengo la kukusanya bilioni 2.8 na Uyui imekusanya bilioni 2.2 ya lengo la kukusanya Sh. bilioni 2.5.

Alisema Igunga imekusanya kiasi cha Sh. bilioni 1.9 kati ya lengo la Sh. bilioni 2.7, Manispaa ya Tabora imekusanya bilioni 3.1 kati ya shilingi bilioni 4.6, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega imekusanya shilingi bilioni 1.5 ya lengo la bilioni 2.6 na Urambo imekusanya shilingi bilioni 1.4 ya lengo la bilioni.

Makungu alisema Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Manispaa ya Tabora, Nzega DC na Urambo zimeshindwa kuvuka lengo la kitaifa la asilimia 80.

Alizitaka halmashauri zote kuhakikisha katika mwaka huu wa fedha zinaongeza kasi, uadilifu katika ukusanyaji wa mapato ili hatimaye Mkoa uweze kuvuka asilimia 100 ya lengo.

Makungu alisema ni agizo la serikali kuwa itakapofika mwaka 2025 ziweze kujitegemea kwa asilimia 100, na kuongeza kuwa ni vema wakabuni vyanzo vipya vingi vya mapato na kuziba mianya ya upotevu wa mapato ikiwamo matumizi sahihi ya ukusanyaji mapato.

## Faidika yanunua mikopo benki, taasisi za kifedha

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya kifedha ya Faidika imeanza kununua mikopo ya wakopaji kwenye benki na taasisi zingine za kifedha na kutoa mikopo mipya yenye riba nafuu baada ya kununua mikopo ya awali.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Faidika, Baraka Munisi, alisema jijini Dar es Salaam jana kuwa huduma hiyo inatolewa kwa wafanyakazi wote wa serikali wenye mikopo katika benki na taasisi zingine za kifedha.

Munisi alisema lengo la kuanzisha mpango huo ni kusaidia wakopaji ambao kwa sasa wanalipa riba kubwa na kuwa na marejesho makubwa yanayokatwa katika mishahara yao na kufanya kushindwa kufikia malengo ya maendeleo.

Alisema taasisi yao pia imelenga kuwawezesha wakopaji kufikia malengo yao yaliyoonekana kutofikiwa kutokana na kutokupata mikopo mikubwa yenye marejesho ya muda mrefu.

"Tumeamua kutoa fursa kwa kila mfanyakazi wa serikali kupata mkopo mpya wenye riba nafuu na kulipiwa mkopo wake wa sasa wenye riba kubwa.

"Faidika ni moja ya 'microfinance' inayotoza riba ndogo na kutoa mikopo yenye muda mrefu wa marejesho kuliko 'microfinance' nyingine nchini," Munisi alitamba.

Alisema ununuzi wa mikopo ya benki na taasisi zingine utafanyika kwa haraka bila kumchelewesha mkopaji, akifafanua kuwa Faidika itanunua na kuwapa mikopo ya kuanzia Sh. 200,000 mpaka Sh. milioni 70.

Alisema kuwa muda wa mrejesho ya mkopo utakuwa kuanzia miezi sita mpaka miezi 84 kulingana na matakwa ya mteja, akifafanua kuwa mkopaji anatakiwa kuwa na taarifa ya deni kutoka kwa taasisi au benki aliyokopa iliyoidhinishwa na kugongwa mhuri.

"Pia mkopaji anatakiwa kuwa na kitambulisho cha kazi kikiambatanishwa na kitambulisho cha taifa au pasipoti au kitambulisho cha mpigakura au leseni ya udereva na picha moja ya pasipoti," alisema.

Kwa mujibu wa Munisi, mkopaji pia anatakiwa kuwa na stakabadhi moja ya mshahara wa mwezi uliotangulia na taarifa za kibenki kuanzia miezi miwili na kuendelea.

# Mufti Zanzibar aasa mgawanyiko uchaguzi

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MUFTI Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kaabi, amesema ujio wa vyama vingi vya siasa nchini, haukuletwa kwa malengo ya kubaguana, kukashifiana na kulipuana bali ni kuchochea maendeleo kwa wananchi wote.

Alisema sasa imekuwa ni kero, kebehi, matusi, kubaguana, kuacha kuzikana na kuondoleana heshima, wakati hilo sio lengo lake tofauti na baadhi wanavyofanya.

Akizungumza na masheikh na maimamu wa misikiti ya Pemba, kwenye mkutano wa siku moja uliofanyika Gombani Chakechake, alisema lazima wananchi waondokane na mawazo finyu juu ya uwapo wa vyama vingi vya siasa.

Alieleza kuwa moja ya kazi ya viongozi wa dini ni kuhakikisha wanakaa na kuwaeleza wafuasi wao kila wakati, juu ya umuhimu wa kuishi kwa kuheshimiana huku amani ikitawala katika maisha yao na siasa isiwe chanzo cha kuwabagua, kiimani.

"Nyinyi masheikh na maimamu mnao wajibu wa kuwatuliza wafuasi wenu, wasiwe chanzo cha uvunjifu wa amani, unaotokana na siasa, maana lengo la hii ni kuongeza kasi ya maendeleo," alieleza.

Aidha, Mufti Kaabi alisema hakuna haja ya kuivuruga amani iliyopo na kuzalisha migogoro, kwani zipo njia kadhaa zinazoshauriwa kufuatwa inapozuka migogoro.

Naibu Mufti Mkuu wa Zanzibar anayefanya kazi zake kisiwani Pemba, Sheikh Mahamouda Mussa Wadi, alieleza kusikitishwa na baadhi ya mitandao ya kijamii, inavyotumika vibaya na kuwapo kwa viashiria vya uvunjifu wa amani.

Alisema, baadhi ya mitandao hiyo imekuwa ikitoa habari zisizo na maadili na kushawishi kundi moja kufanya vurugu, hivyo ni wajibu wa wananchi kujihadhari nayo.

Akiwasilisha mada ya amani, Katibu wa Mufti, Sheikh Khalid Ali Mfaume, alisema kuvunjika kwa amani mara zote huwa rahisi, lakini kuirejesha kwake ndio huwa kazi.

Alisema viongozi wa dini wakiwa karibu mno na wafuasi wao kila wakati na kuwaeleza madhara ya kukosa amani, inaweza kusaidia kuitunza iliyopo.

Katika hatua nyingine, Katibu huyo alisema matumizi ya maneno ya jazba na lugha za kejeli huwa ni miongoni mwa viashiria vya uvunjifu wa amani.

Akichangia mada, Sheikh Bakar Salim Bakar wa Gando Wete, alisema ni vigumu kwa baadhi ya viongozi wa dini kusikilizwa na wafuasi wao kutokana na baadhi yao kujiingiza kwenye vyama vya siasa.

Naye Sheikh Mohamed Khasmi Mohame wa Chakechake, alisema kwao huo ni mwanzo mzuri, wa kupewa elimu na kuiomba ofisi ya Mufti kukutana na wagombea wa vyama vyote

# Malinyi yapata fursa ya dhahabu

**Na Ashton Balaigwa,** MALINYI

WILAYA ya Malinyi mkoani Morogoro itaanza kufunguka kiuchumi baada ya kujitokeza kwa fursa mbalimbali ikiwamo ya kugundulika kwa machimbo ya dhahabu.

Machimbo hayo yapo katika Kijiji cha Misegese na kuwa kivutio kwa wachimbaji wadogo kutoka maeneo mbalimbali nchini na kuweka kambi.

Mkuu wa Wilaya ya Malinyi, Mathayo Masele, ambaye alitembelea eneo hilo, aliwaagiza wachimbaji hao kufanya uchimbaji kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa na Wizara ya Madini pamoja na halmashauri ya wilaya hiyo.

"Tunajua mmetoka maeneo mbalimbali ya nchini kwa ajili ya kuchimba haya madini ya dhahabu, hatujamkataza mtu, lakini tunachotaka mfuate taratibu zote za uchimbaji wa madini ikiwamo ulipaji wa kodi na ushuru ili serikali ipate mapato yake," alisema.

Alisema hiyo ni fursa nyingine kwa wananchi wa wilaya hiyo mbali na kilimo cha mpunga ambacho kimewapa fursa wakazi wa wilaya hiyo na kuwabadilisha kimaisha.

Mkuu huyo wa wilaya alisema baada ya moja ya taasisi ya fedha kufungua tawi lake hivi karibuni katika wilaya hiyo, sasa itakuwa kimbilio la wafanyabiashara na kutoa fursa kwa wakulima kuzalisha mazao ya biashara.

Msimamizi wa wachimbaji hao, Ismail Hanga, alisema wameanza uchimbaji katika mgodi huo kwa kupasua miamba kwenye mashimo kumi ambayo kwa kipindi kifupi yameonyesha mafanikio makubwa, ikiwamo upatikanaji wa dhahabu, na kwamba kazi iliyopo hivi sasa ni kupasua miamba hiyo kwa kutumia mashine za uchimbaji.

Hata hivyo, alisema changamoto kubwa wanayokabiliana nayo ni ukosefu wa huduma mbalimbali za kijamii katika eneo hilo ikiwamo maji, huduma za afya na ubovu wa barabara hali ambayo inaathiri eneo kushindwa kufikisha vifaa kwa ajili ya uchimbaji wa kisasa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Malinyi, Hawa Mposi, alisema fedha zote zitakazokusanywa kutokana na tozo mbalimbali katika machimbo hayo, zitasaidia kujenga miundombinu mbalimbali katika eneo hilo, ikiwamo zahanati na kufikisha eneo hilo huduma za maji ili kuwasaidia wachimbaji hao.




Mlinzi wa Shule ya Kimataifa Hazina ya Magomeni jijini Dar es Salaam, Said Ramadhan (kushoto), akiwafundisha wanafunzi wa shule hiyo namna ya kutumia moja ya vifaa vya kisasa vya kuzimia moto vilivyofungwa kwenye maeneo mbalimbali shuleni hapo, kwa ajili ya tahadhari ya moto. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Ukatili wa kijinsia kinara kwenye familia

**Na Yasmine Protace**

IMEELEZWA kuwa asilimia 90 ya vitendo vya ukatili wa kijinsia vinatokea katika familia.

Hayo yalibainishwa jijini Dar es Salaam na Rose Munyema, mkaguzi msaidizi wa kituo cha Polisi Mburahati.

Rose ambaye yupo katika kitengo cha dawati la jinsia katika kituo hicho, alisema matukio ya ukatili yapo na yanatokea sana katika familia.

Aliyasema hayo wakati akitoa mada ya masuala ya ukatili wa kijinsia kwa washiriki wa semina na jinsia na maendeleo (GDSS) zinazoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP-Mtandao).

"Matukio ya ukatili yapo ya aina mbalimbali na mengi yamekuwa yakitokea katika familia," alibainisha Munyema.

Alisema jamii inatakiwa kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi pale panapotokea ukatili ili wahusika wachukuliwe hatua.

Alisema Jeshi la Polisi kazi yake ni kumlinda raia na mali zake, na kuongeza kuwa mwaka 2006 jeshi hilo lilifanya maboresho na kuanzisha kitengo cha dawati la jinsia la watoto.

Alisema dawati la jinsia la watoto lipo kila kituo cha polisi.

"Ukatili upo wa aina nyingi, upo katika makundi matano ambayo ni ukatili wa kimwili, kingono, kisaikolojia, kiuchumi na mila potofu na tamaduni," alisema na kufafanua zaidi kuwa ukatili upo zaidi mitaani, lakini matukio yanayoripotiwa ni madogo. Munyema alisema katika kipindi cha mwaka huu pekee eneo la Magomeni watu 13 wamefungwa maisha watu katika kesi za ukatili zilizoripotiwa Magomeni.

"Jamii inatakiwa kutoa taarifa kila panapotokea ukatili ili wahusika wachukuliwe hatua za kisheria," alisema.




Ukurasa 13

Amani ya Tanzania mikononi mwa NEC

BUFE

IJUMAA SEPTEMBA 4, 2020

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA



Ukurasa 12

## Ubora, viwango misingi inayojenga imani ya mlaji



# Corona ilivyowavuruga wanaushirika

Wanachama wa Umoja Amcos wakiwa kwenye mkutano uliofanyika kabla ya corona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**Na Mwandishi Wetu**

COVID-19 pamoja na kuathiri afya za binadamu, kuvuruga utalii na kukwamisha elimu, haikuiacha salama sekta ya ushirika.

Ni kilio cha wanachama wa vyama vya ushirika vya msingi wilayani Liwale mkoani Lindi, ambao wanasema kila mwaka hufanya mikutano, lakini safari hii corona imewakwamisha.

Wadau hao wanasema mikutano yao ni muhimu kwa lengo la kuwapatia wanachama taarifa za mapato na matumizi ya vyama hivyo, mafanikio, changamoto na mipango ya kusonga mbele.

Chama cha Ushirika cha Msingi cha Umoja (Umoja Amcos) ni miongoni mwa vyama hivyo, ambacho kila mwaka huitisha mkutano wa wanachama wake inapofika mwezi Aprili au Mei kwa ajili ya kuwapa wanachama taarifa za maendeleo ya umoja wao, kimekwamishwa na COVID-19.

Wanachama wake wanasema kwa mara ya kwanza tangu chama hicho kilipoanzishwa mwaka 1988, kimeandika historia 2020 kwani kimekwama kutokana na tishio la corona na kulazimika kuahirisha mkutano huo hadi mwakani.

Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mpako, anaeleza hayo katika mazungumzo na Nipashe na kufafanua kuwa sasa mkutano huo utafanyika mwaka ujao.

"Corona ilikwamisha mambo mengi sana ikiwamo shughuli za ushirika, hasa baada ya serikali kuzuia mikusanyiko, pamoja na kwamba baadaye iliruhusu shughuli ziendelee, tuliona ni bora tuahirishe mkutano wetu," anasema Mpako.

Anataja miongoni mwa mambo hayo kuwa ni uchaguzi wa viongozi wapya wa chama hicho, kwa kuwa anamaliza kipindi chake cha uongozi ambacho ni miaka minne na taarifa ya ujenzi wa ghala la pili la chama hicho.

"Hili suala la uchaguzi wa viongozi ndilo limenisukuma kuweka mambo sawa, kwani huenda wakawapo wanachama wanaotaka nafasi hii nilionayo, ambao wanadhani mkutano umeahirishwa tu.

Mpako anasema, kwa mujibu wa katiba ya vyama vya ushirika, viongozi hukaa madarakani kwa miaka minne, na kwamba kipindi chake cha uongozi kimeisha mwaka huu. Anaeleza kuwa wanachama walikuwa wamejiandaa kuchagua viongozi wao wapya, lakini inabidi wasubiri hadi mwaka ujao, na kuwashauri wale wanaotaka uongozi waendelee kujipanga.

Anawaambia kuwa muda wake wa uongozi umekwisha, lakini analazimika kuendelea kushikilia nafasi hiyo hadi mwaka kesho mkutano utakapoitishwa, ambapo atatoa taarifa za maendeleo ya chama na kuachia ngazi.

**MIRADI INAYOTAZAMWA**

Mwenyekiti huo anasema, ujenzi wa ghala hilo ni miadi muhimu kwani ni la kukusanyia mazao mbalimbali na ulianza mwaka jana na limejengwa kwa fedha za mkopo.

"Ghala hilo ambalo pia ni sehemu ya mradi wetu wa kujiongezea kipato, tumelijenga kwa gharama ya Sh. milioni 500, ambazo chama kilikopa," anasema Mpako.

Anafafanua kuwa, ghala hilo lenye uwezo wa kuchukua tani 10,000 za mazao mabalimbali, ni tofauti na la kwanza ambalo linahifadhi tani 5,000 za mazao mbalimbali zikiwamo korosho.

Anasema, kutokana na wakulima kuhamasika na kujitokeza kwa wingi kulima korosho, chama hicho kiliamua kujenga ghala hilo, baada ya lile la kwanza kushindwa kuhimili wingi wa korosho.

Mpako anasema, Umoja Amcos ni chama kikubwa wilayani Liwale chenye wanachama 1,063, ambao ni muhimu kila mwaka kuwapa taarifa za maendeleo ya chama chao, lakini bahati mbaya mwaka huu haikuwa hivyo.

Anasema, kukamilika kwa ghala hilo kutasaidia kumaliza tatizo la ukosefu wa sehemu ya kutunzia mazao uliokuwa unatokana na udogo wa ghala la kwanza

**WANACHAMA WAKUBALI**

Fikira Ponera ni mwanachama wa Umoja Amcos, ambaye anasema anakubaliana na hatua hiyo, kwa madai kwamba iko juu ya uwezo wa uongozi hivyo cha msingi ni kuomba uzima.

"Mwaka huu tumepitia katika kipindi kigumu hasa hili suala la corona, kwa hiyo uamuzi wa uongozi wetu kuahirisha mkutano ni sahihi kwani mkutano unahitaji maandalizi ya kutosha," anasema Fikira.

Anasema, kwa jinsi ambavyo serikali ilizuia mikusanyiko na baadaye kuruhusu iendelee, isingefaa kufanya maandalizi ya kulipuka, bali kujipanga upya kama ambavyo viongozi wameamua kuahirisha.

Bakari Chikojo ni mwanachama mwingine, anayesema, Umoja Amcos ni chama kikubwa ambacho hakipaswi kufanya mambo yake kwa kubahatisha, bali kuwa na muda wa kutosha.

BIASHARA

# Ubora, viwango misingi inayojenga imani ya mlaji

**Na Joseph Mwendapole**

SOKO la Tanzania linapokea bidhaa zinazozalishwa ndani na nje ya nchi, hivyo uhakiki wa ubora na usalama wa kinachouzwa dukani au popote ni jambo la msingi.

Ni la lazima kwani bila ubora kinacholiwa au kutumiwa kinaweza kuwa hatarishi kwa watu na mazingira.

Kwa hiyo kudhibiti ubora wa bidhaa na kuhakikisha kuwa zinakuwa na viwango ndilo jukumu la mamlaka zinazosimamia ubora ambao ni nyenzo katika kuongoza mabadiliko na kuainisha njia zinazoweza kufungua masoko na kujenga mazingira bora ya kibiashara na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Msingi huo, ndiyo unaowasukuma wataalamu kusimamia ubora wa bidhaa kwa maslahi ya umma kwa kukutana na kutayarisha viwango ambavyo husambaza ubunifu na uvumbuzi katika nchi zao, hivyo kuweka jukwaa la mabadiliko chanya kwa taasisi za biashara, serikali na jamii.

Kwa Tanzania, jukumu la kusimamia viwango lipo chini ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ambalo lipo chini ya Wizara ya Viwanda ya Biashara likiwa limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 3 ya mwaka 1975. Sheria hiyo ilihuishwa mwaka 2019,

iIiboreshwa ili kulipa shirika nguvu zaidi ya kusimamia majukumu yake katika masuala ya viwango na udhibiti ubora wa bidhaa mbalimbali.

Mabadiliko hayo yalifanya baadhi ya kazi zilizokuwa zikitekelezwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) kuhamishiwa kwa shirika hilo. Majukumu hayo ni usajili wa bidhaa, vyakula, vipodozi na majengo.

Moja ya majukumu ya shirika hili ni kueneza uelewa na kukuza matumizi ya viwango na kanuni za udhibiti wa ubora katika sekta za viwanda na biashara, kwa nia ya kuunga mkono juhudi za kitaifa za kuzalisha bidhaa bora zenye uwezo wa kushindana katika masoko ya ndani na nje.

Lengo la hatua hiyo ni kukuza uwepo wa bidhaa na huduma bora na salama kwa Watanzania na kuchochea maendeleo ya uchumi.

Kwa kutambua umuhimu huo, TBS imekuwa ikifikisha mafunzo kwa wadau ili waweze kuthibitisha bidhaa na huduma zingine zinazotolewa shirika na maelekezo mengine kupitia Kitengo cha Utafiti na Mafunzo.

Meneja wa Utafiti na Mafunzo wa TBS, Hamisi Sudi, anasema mafunzo yanayotolewa ni ya namna tatu tofauti au zaidi na ni yale yanayotokana na viwango vya mifumo (Management System Standards).



Wateja wanaongeza imani ya bidhaa wanapoona usafi, viwango na ubora kwenye kile wanachonunua kinazingatiwa na kudumishwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> **Wakati huu tumepata kundi la watu wanaoishi na ulemavu wa kusikia (viziwi) kutoka Tanga na Kigoma wanataka mafunzo na tunajipanga kwenda kuwafikishia mafunzo hayo.**



Kwenye sekta ya usafiri matairi ni kila kitu. Ni lazima yawe na ubora na viwango ili kulinda maisha ya wasafiri, wapita kwa miguu, vyombo vya moto na miundombinu.

Anasema wana mafunzo kwa ajili ya kuwaelimisha wajasiriamali ambao wamepitia SIDO, wafanyabiashara na kwingineko ambako taasisi zimewasajili ili wazalishe bidhaa, lakini kutokana na ushindani wa biashara lazima wafike TBS kwa ajili ya kufuata utaratibu ili waweze kudhibitisha ubora wa bidhaa zao kwa lengo la kuziongezea thamani.

Mbali ya kuziongezea thamani, Sudi anasema hatua hiyo inawapatia wajasiriamali na wafanyabiashara masoko zaidi ndani na nje ya nchi.

"Kwa kufanya hivyo tunakuwa tumeongeza imani kwa wateja wetu pale bidhaa zinapoonekana zimedhibitishwa na hivyo hata walaji wanakuwa na uhakika na usalama wa afya zao." Anasema Sudi.

Anasema kujiamini kwa walaji kunaongezeka kwa kuwa wananunua bidhaa ambazo wana uhakika nazo kwa afya na usalama wao, lakini pili hatua hiyo inaenda sambamba na thamani ya fedha wanazozitoa.

"Kwa hiyo, iwapo utanunua fungu la nyanya labda kwa Sh. 200, halafu baadaye ukapata matatizo ya tumbo utatumia hela nyingi kujitibu, wakati kumbe kama nyanya hizo zingethibitishwa gharama hizo zisingetokea," anafafanua Sudi na kuongeza.

"Kwa hiyo haina maana kununua bati ambayo haina kiwango na ndani miaka miwili ikawa imeshika kutu. Lakini kama ungetoa hela ukanunua bati ambayo imedhibitishwa ungeweza kuepuka usumbufu kwa kununua bati ambayo itadumu muda mrefu."

Anaongeza kwamba wanatoa mafunzo baada ya kupokea maombi ya makundi mbalimbali yanayohitaji huduma hiyo kutoka kwao.

"Kwa mfano watu wanasema sisi Bodi ya Maziwa tunataka wanazalishaji wapate uelewa wa kuzalisha kwa ubora hatimaye wathibitishiwe ubora wa maziwa yao, lakini pengine hiyo ikawa haipo kwenye programu yetu ya kila mwaka, wakija kwetu tunawapatia mafunzo," anasema Sudi na kuongeza;

"Lakini wanakuja watunzaji wa mafuta ya kupikia, pengine chama cha wazalishaji wa mafuta ya alizeti ambao wamekuwa wakianika juani na wakati wote kukamua mafuta, mwisho wa siku kazi wanayofanya ni kubwa na kipato hawakipati, matokeo yake wenye magari wakienda kama wateja, wanayaangalia na kuondoka kwa sababu hayana ubora, hiyo ni kwa sababu wateja wanataka kuona kazi zenye TBS, hivyo tunawapatia mafunzo kwa kuwa tunataka wabadilike kupitia mafunzo."

Vile vile, Sudi anasema pale wanapohitajika viwandani wanatoa mafunzo ambayo ni ya kwenye uzalishaji kwa ajili ya kutoa tafsiri ya viwango.

Anasema wanapopelekewa maombi kwa ajili ya kuwafundisha, wanafanya hivyo na kwamba wanaohitaji kufundishwa wanahudumiwa kwa mfano watengeneza vilainishi vya mitambo, waliomba na TBS iliwapatia mafunzo.

Pia anasema kuna wadau wengine ambao shughuli zao ni kuondoa mizigo bandarini, nao walipatiwa mafunzo. Mbali na hao anasema wajasiriamali wameendelea kupewa mafunzo mengi karibu kila mwaka.

"Wakati huu tumepata kundi la watu wanaoishi na ulemavu wa kusikia (viziwi) kutoka Tanga na Kigoma wanataka mafunzo na tunajipanga kwenda kuwafikishia mafunzo hayo."

Kwenye kufundisha mafunzo kuhusu mifumo ya viwango (Management System Standards), Sudi anasema kuna viwango kama vya aina nne au tano.

Mojawapo ya viwango hivyo ni ISO 9001;2015 ambacho matakwa yaliyoainishwa humo yanaweka wazi kuwa taasisi inaweza kuanza na watu wawili au zaidi wanaofuata utaratibu uliomo humo kuendesha taasisi au kampuni yao ili iwe na tija katika uzalishaji wake, kutoa huduma bora, kwa haraka na kuondoa ukiritimba.

"Lakini kila mshiriki katika kampuni au taasisi husika anakuwa na umuhimu wake," anafafanua Sudi.

Anasema kunakuwa na menejimeti ya juu katika kutoa maamuzi, lakini kunakuwa na utaratibu watendaji kujifanyia tathmini ili kujua wapi wamekwama, wamekosea nini ili mwisho wa siku waone huduma zile katika hiyo kampuni au taasisi zinakidhi kile ambacho kinatarajiwa na wateja.

Kwa mujubu wa Sudi kiwango kingine kwenye huo mfumo ni kuhusu masuala ya mazingira cha ISO 140001.

Kinahusisha kampuni kama Twiga Cement kinachozalisha sementi zinapofuata matakwa ya kiwango katika uzalishaji wao, mazingira yanakuwa salama na hatua hiyo inaleta picha nzuri kwa wale wanaopata huduma.

Vinginevyo, anasema uzalishaji usiozingatia utunzaji mazingira unaweza kuleta picha mbaya na kampuni husika kujikuta ikitumia nguvu kuondoa uchafu kwa sababu ya kutojua utaratibu wa kufuata ili mazingira yawe mazuri.

Anataja kazi nyingine za kitengo hicho ni kuwa ni kutoa mafunzo kuhusiana na masuala ya afya na usalama.

"Unazalisha sawa lakini usafi wako ukoje? Unachokizalisha kama ni mafuta au mkate usafi wake ukoje? Kwa hiyo mzalishaji anatakiwa kufahamu jengo analotakiwa kulitumia kuzalisha bidhaa zake liwe vipi, mfumo wa hewa uwe vipi," anasema Sudi.

Anasema viwanda vinatakiwa kuwa sehemu ya kudhibiti vihatarishi kwenye bidhaa zinazozalishwa ili kuhakikisha kitu kinapotoka sehemu moja kwenye nyingine, mfano eneo la kusagia na kikifika sehemu ya kuchanganywa labda maji katika kila hatua ya uzalishaji kusiwe na vihatarishi vinavyoweza kuingia kwenye bidhaa inayotengenezwa.

Kwa msingi huo anasema ni muhimu kila sehemu ya uzalishaji kuwa na ufuatiliaji na kila malighafi ikajulikana imezalishwa siku gani, hivyo inakuwa ni rahisi kutambua sehemu yenye matatizo yanapojitokeza.

Anatoa mfano kwamba kama mifumo ya uzalishaji inaposhindwa kutambua kuwa malighafi fulani hazina ubora, ni dhahiri kile kitakachozalishwa hakitakuwa bora pia.

Kwa mujibu wa Sudi unapokuwa na mfumo huo inakuwa rahisi kufuatilia malighafi zenye matatizo.

Kwa msingi huo anasema mafunzo ya uthibitishaji wa mifumo unamwezesha mzalishaji au mtoa huduma kufuata taratibu ambazo zitafanikisha kufikia malengo yake.

"Kwa hiyo kitengo cha utafiti na mafunzo kipo kwa ajili ya kuwapa watu uelewa kuhusu matakwa ya kiwango yanayohitajika ili mwisho wa siku mzalishaji aweze kuambiwa mifumo yake imethibitishwa na inafuata kiwango husika," anasema.

Kwa mujibu wa Sudi jambo ambalo TBS inajivunia ni kuongezeka idadi ya wanaoomba kuthibitishiwa bidhaa zao (certification) na kwamba wengi wametokana na mafunzo yanayotolewa na kitengo hicho.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Amani ya Tanzania mikononi mwa NEC






**NA JOSEPH KULANGWA**

SAFARI ya kuelekea Oktoba 28 siku ambayo Watanzania wataamua kuendelea na Rais aliyepo au kuweka mwingine itakapotimia, kwa kupiga kura zao za siri baada ya kusikia na kuona mengi kutoka kwa wagombea wa nafasi hiyo.

Ni siku ambayo Watanzania, hali kadhalika wenye sifa ya kupiga kura, watakuwa wanatafuta kupata wawakilishi wapya au kuendelea na waliokuwa nao katika Bunge, pia madiwani wapya au waliokuwa nao katika mabaraza ya madiwani.

Hivi sasa imekuwa ikitolewa miito mingi ya kudumisha amani na utulivu kabla, wakati na baada ya uchaguzi huo, viongozi wa kiserikali na wa kidini wamekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha tunu hizo adhimu zinadumishwa.

Sambamba na hilo, vyombo vya usalama navyo vimekuwa vikijitokeza kueleze au tayari wao wa kushirikiana na raia kuhakikisha uchaguzi hauwi sababu ya kutibu au tulivu, amani, umoja na ushirikano uliopo baina ya Watanzania.

Watanzania ni watu ambao kihistoria ni wapenda amani wanaothamini usalama wao na wa mali zao, lakini na wa Taifa zima, msingi waliowekewa na waasisi wa Taifa hili, waliopo na waliokwishatangulia mbele za haki.

Lugha moja ya mawasiliano –Kiswahili, imetoa mchango mkubwa kuunganisha Watanzania na hivyo kujenga mshikamano imara inayosababisha kuwapo amani na utulivu miongoni mwao, kizazi hata kizazi.

Kwa usikivu na uelewa walio nao, ndiyo sababu Tanzania imeendelea kuwa mahali salama pa kukimbilia na kuishi, ikithibitishwa na jinsi ilivyokuwa na inaendelea kupokea wakimbizi kutoka nchi jirani, ambao wamekuwa wakikimbia machafuko nchini mwao, hususan ya kisiasa.

Ukarimu wa Watanzania ni alama kimataifa kuwa wanaheshimu utu na haki ya kila mmoja na hivyo kuona umuhimu wa kuhifadhi wakimbizi wanaokimbia kutafuta amani na kuishia kuikuta Tanzania ambako, imekuwa kama sehemu ya mila na desturi.

Nchi nyingi duniani zimejikuta katika machafuko kabla na baada ya uchaguzi kutokana na mambo mbalimbali, lakini kubwa likiwa ni haki kutoonekana na imetendeka katika uchaguzi husika, hasa pale demokrasia inapokuwa imekiukwa.

Mara chache Tanzania imekuwa katika machafuko ya kinadharia, ambayo yanahusika na washindwa kulalamikia uchaguzi kwa msingi kuwa ama umevurugwa kwa kanuni kutofuatwa barabara au kwa uhesabuji kura, kutosimamia na asiyestahiki kupewa ushindi.

Lakini, pamoja na hayo, amani iliendelea kutamalaki isipokuwa kwa atukio machache yaliyopata kutokea Zanzibar, katika uchaguzi wa mwaka 2001 na kusababisha idadi ndogo yawakimbizi kutoka Tanzania, ikiwani mara ya kwanza na ya mwisho katika historia ya Taifa hili.

Ni matumaini ya Watanzania walio wengi, kwamba uchaguzi wa mwaka huu, hautakuwa kiini cha machafuko, ingawa hakuna uchaguzi kokote kule unaopita bila malalamiko, kwani ni imani kwamba Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imejipanga ipasavyo kuhakikisha haki inatendeka.

Hali hiyo inaimarishwa na kauli ya Mkuu wa Nchi, Rais John Magufuli, ambaye katika matukio mbalimbali ameendelea kusisitiza kuwa uchaguzi huu utakuwa huru na wa haki, hivyo hapana sababu ya wananchi kuwa na wasiwasi.

NEC inapaswa kujua kuwa ina dhima kubwa ya kuhakikisha uchaguzi unakuwa kama inavyotakiwa kidemokrasia na kwamba kila upande unaoshiriki, unaridhishwa na kitakachokuwa kimefanyika hasa kwa kuhakikisha uhuru na haki vinavyoelezewa vinaonekana dhahiri.

Mara nyingi katika jamii, vitu vinavyoweza kuharibu mambo huwa ni furaha inayopitiliza au hasira; furaha kwa wanaokuwa wameshinda uchaguzi, lakini hasira kwa wanaokuwa wamepoteza. Lakini, yote haya yanaweza kudhibitiwa.

Kama uchaguzi utakuwa huruna wa haki, bila shaka washindi hawatakuwa na furaha ya kupitiliza kwa sababu wataamini kuwa hakuna, sababu ya kufanya hivyo na hata washindwa hawatakuwa na lolote la kukasirikia kwani watakuwa wameamini matokeo.

Hivyo, macho na masikio yote yatakuwa yanaelekezwa kwa NEC kuona na kusikia ilivyojipanga, ili kukata kiu ya kidemokrasia ya Watanzania kwa kutenda haki, badala ya kuendelea kutoa miito ambayo pengine itakuwa ya kinadharia zaidi. Watanzania tudumishe amani iliyopo, ambayo ni gharama kuirejesha ikitoweka. Kila la heri!

**Simu: (+255) 713 410008 na baruapepe: jkulangwa@yahoo.com**

BIASHARA

# Wachimbaji wanahitaji kuona mbadala zebaki sasa migodini

**Na Gaudensia Mngumi**

KEMIKALI hatari ya zebaki iliyotumiwa kusafisha dhahabu migodini kwa miongo kadhaa mwaka jana, ilitangaziwa kiama baada ya serikali kuamua rasmi kuwa Tanzania itasaini na kuridhia mkataba wa Minamata unaokomesha matumizi ya sumu hiyo duniani.

Licha ya kutumiwa na wachimbaji wadogo karibu kila kona ya Tanzania yanapochimbwa madini haya zebaki ni sumu hatari inayotajwa kuwa ina athari nyingi mbaya ni huhusishwa na saratani ya ngozi na ini.

Inatajwa na wataalamu wa afya likiwamo Shirika la Afya Duniani (WHO) kuwa huleta ugumba na kuharibu mimba, kutibua mifumo ya fahamu na kusababisha kiharusi na huchafua mazingira na kutibua mfumo wa ikolojia.

Mkataba wa Minamata au 'Minamata Convention on Mercury' ni makubaliano ya kimataifa ya kulinda afya za watu na mazingira kutokana na athari za sumu inayozalishwa na zebaki au 'mercury'.

Unaitwa Mkataba wa Minamata ukipewa jina la mji wa Japan uliochafuliwa na kemikali za sumu hiyo kwa miongo mingi na kusababisha uharibifu wa maisha, afya na mazingira ya watu wa Minamata , uliokuwa unafanywa na kiwanda kilichokuwa kinazalisha bidhaa zinazotumia malighafi ya zebaki.

Mwaka jana Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) ilitangaza kuwa wakati umefika wa kuachana na zebaki ambayo inakadiriwa kuwa imeathiri asilimia 25 hadi 33 ya wachimbaji wadogo wa dhahabu nchini kwa kuwapa magonjwa kama ya mifumo ya fahamu, uzazi, njia ya hewa, figo, moyo na udhaifu wa mwili.

Azimio la kuridhia Mkataba wa Minamata kusitisha matumizi ya zebaki nchini liliwasilishwa bungeni na wabunge kuelezwa kuwa inadhoofisha kukua viumbe hai wanaoishi ndani ya maji, inachafua mfumo mzima wa ikolojia kuanzia chakula, mifugo, viumbe vya majini, vyanzo vya maji, hewa na udongo.

Pamoja na maelezo hayo na nia hiyo ni wakati wa kuona serikali ikianza kutekeleza mkataba huo kwa kuwapa wachimbaji njia mbadala ya kusafisha dhahabu, kwani lengo la Minamata ni kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari za uchafuzi wa mazingira unaotokana na kutumia zebaki katika hatua za uzalishaji, matumizi na utupaji wa sumu hiyo.

Zebaki ambayo imetumiwa sana kusafisha dhahabu katika ukanda mzima wa mikoa ya Mwanza, Shinyanga, Geita na Simiyu, imechafua pia mazingira ya mikoa ya Mbeya, Ruvuma na Tanga kando ya Mto Zigi kwenye machimbo ya dhahabu.

Serikali inasema kuwa sheria za kuanza kufanikisha utekelezaji wa mkataba huo zipo na hakuna kipingamizi kwa sababu sheria zipo kwa mfano Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya 2004, ya Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali za Viwandani na Majumbani ya mwaka 2003, ya Madini ya 2010, Afya ya Jamii ya mwaka 2009 na ile ya Chakula na Dawa ya Mwaka 2003.

Kinachosubiriwa sasa ni kuwa na kanuni na pia teknolojia mbadala wa zebaki ili wachimbaji wadogo waachane na kutumia sumu hiyo inayoishi kwenye ardhi au majini kwa miongo zaidi ya mitatu.

Inatajwa kuwa ni sumu inayosafiri umbali mrefu ikiwa ndani ya maji na hata ardhini hivyo kuwa na athari za miaka mingi zaidi.

Umoja wa Mataifa (UN), mwaka jana ulizindua mpango wa kuboresha sekta ya uchimbaji mdogo wa dhahabu ili kuondoa matumizi ya zebaki kulinda afya ya binadamu na mazingira, kazi inayoshirikisha wadau likiwamo Shirika la Mazingira la UN- UNEP lengo ni kuwasaidia kupata mbinu za kisasa za kuchejua dhahabu bila kutumia zebaki.

UN -UNEP wanaamini kuwa kuanzisha uchimbaji mdogo wa dhahabu usiotumia zebaki utasaidia kulinda afya za mamilioni ya watu na athari za sumu hiyo ambayo imeathiri watu wengi kwa Tanzania si kanda ya ziwa pekee bali maeneo mengi ya nchi.

Tanzania imeamua kuridhia mkataba wa Minamata ili kushirikiana na nchi nyingine kutafuta suluhisho la zebaki kwa teknolojia rahisi na rafiki kwa wachimbaji wadogo kwa gharama nafuu. Takribani nchi 113 zimeridhia huo ulioanza kutekelezwa Agosti 2017 mara baada ya mataifa 50 kuuridhia.

Katika kufuatilia matumizi ya zebaki Nipashe ilifanya ziara katika maeneo mengi ya wachimbaji wadogo wa mkoa wa Dodoma kwenye mgodi wa Noli na mkoani Geita kwenye machimbo ya Nyarugusu. Katika ziara hiyo wachimbaji wanakiri kuwa madini hayo ya zebaki ni sumu na kwao ni hasara mara mbili, mosi kudhurika kiafya na kupoteza dhahabu nyingi kwenye kuchenjua.

Wanasema wakichenjua na zebaki wanaambulia asilimia 20 mpaka 30 ya dhahabu, kiasi kingine kinabaki kwenye udongo na kinapotea.

Wanasema hata wao hawafurahii hali hiyo ni baadhi ya malalamiko ya wachimbaji wadogo wa Noli mkoani Dodoma ambayo kwa ujumla wanataka teknolojia mpya na hawana shida na mkataba wa Minamata.

Kulwa Limbu mchimbaji mbobezi anayelala na kuamka na zebaki kwa miaka mingi, anafafanua kuwa wachimbaji wadogo wamechoka na zebaki wanaitumia kwa vile hawana mbadala, lakini kuacha zebaki bila kupata teknolojia mpya ni jambo lisilowezekana. Hivyo ni jukumu la serikali ambayo hukusanya mrabaha na yenye wataalamu kusaidia wachimbaji kupata teknolojia mpya sasa na kuachana na zebaki ili kuridhia mkataba wa Minamata.

Japo kuna unga wa 'borax' au 'sodium cyanide' wachimbaji wanaona matumizi ya borax hayajafanyiwa uchunguzi kikamilifu, wala haipatikani kwa wingi hapa nchini, lakini kemikali ya 'sodium cyanide' inayotumiwa na wachimbaji dhahabu wakubwa duniani haiwezekani kutumiwa na mchimbaji wa kawaida kama sisi.

Kwenye kutumia 'cynide' uchenjuaji unahitaji mchanga wa dhahabu mwingi kiasi cha chini ni tani 100 hivyo kwa mchimbaji mdogo anaweza kuchimba udongo huo kwa miaka mingi zaidi ya miwili, hivyo ni vigumu kwani atakula nini? Ataishije? Kwa hiyo ni wakati wa serikali kuonyesha kemikali au teknolojia mpya na kupiga marufuku matumizi ya zebaki na kufurahia taifa kuridhia mkataba wa Minamata.



Wachimbaji 'watoto' wakichenjua dhahabu kwa kutumia zebaki kwenye machimbo ya Noli Dodoma. **PICHA: MWANDISHI WETU**

> **Wakichenjua na zebaki wanaambulia asilimia 20 mpaka 30 ya dhahabu, kiasi kingine kinabaki kwenye udongo na kinapotea.**



# TARI yajipanga kuzalisha mbegu tani 10,000

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Kilimo kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imejipanga kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mazao kutoka tani 1,000 kwa sasa hadi 10,000 mwaka 2025.

Akizindua matrekta saba kwa ajili ya uzalishaji mbegu hizo unaofanywa na TARI, Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, alisema serikali imedhamiria kuhakikisha uzalishaji huo unaimarika nchini ili kuondokana na uagizaji wa mbegu nje ya nchi.

Hasunga alisema wizara imepata mafanikio mbalimbali kupitia TARI ikiwamo uzalishaji wa miche ya michikichi milioni mbili kwa mwaka 2019/20 na inategemea kufikia miche milioni 41 mwaka 2025.

"Hatua hizi zinalenga kuhakikisha zinakidhi mahitaji ya mbegu bora kwa wakulima kwa mwaka, hivyo kupunguza uagizaji wa mafuta ya kula na mbegu toka nje ya nchi. Uzalishaji wa mbegu nchini bado upo chini na mahitaji ni makubwa," alisema.

Hasunga alisema matrekta hayo yatatumika kuongeza uzalishaji wa mbegu unaofanywa na taasisi hiyo wa kutoa mbegu bora zinazokidhi viwango kwenye maeneo mbalimbali nchini.

"Leo nimefurahi kuzindua matrekta na zana zake kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za mazao ya kilimo. Hii ni mojawapo ya mikakati ya wizara na serikali kuimarisha miundombinu ya vituo vya utafiti hapa nchini," alisema.

Kwa mujibu wa Hasunga, mwaka 2019/20, serikali kupitia Programu ya Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II), ilitenga fedha katika mfuko wa maendeleo kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu. Lengo la kufanya hivyo lilikuwa kuchangia upatikanaji wa mbegu bora ili kukidhi mahitaji ya Wakala wa Mbegu (ASA), kampuni binafsi zinazohitaji mbegu kutoka TARI ili kuwasambazia wakulima.

"Serikali imetupatia fedha za kununua matrekta saba na zana zake ambazo zitatumika kupanua mashamba ya uzalishaji mbegu na miche bora ya mazao na pia kuimarisha mashamba ya utafiti kwa kuzalisha aina mpya za mbegu bora za mazao mbalimbali," alisema.

Alipongeza TARI kwa kuzalisha mbegu bora zenye sifa ya kutatua matatizo ya mkulima ikiwamo mbegu zenye ukinzani wa magonjwa na wadudu, ukame na zinazotoa mavuno kwa wingi ukilinganisha na zingine.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alimhakikishia waziri huyo kwamba TARI itatumika matrekta hayo kuzalisha mbegu bora zinazotosheleza mahitaji nchini kutokana na serikali kuamua taasisi hiyo ichangie upatikanaji wa mbegu hizo.

Hata hivyo, alisema kampuni binafsi zimejikita kuzalisha mbegu za mahindi na maharage kutokana na kuwa na thamani kubwa na kuacha mazao mengine, jambo ambalo TARI imeliona na kudhamiria kuzalisha mbegu kwa mazao yote.

Alisema kwa sasa taasisi hiyo inazalisha kwa wingi mbegu za mihogo, viazi, nazi, korosho na michikichi na kuwasambazia wakulima.




Mwenyekiti wa Bodi ya Dawa za Tiba Asili kutoka Umoja wa Waganga na Wakunga Tanzania (UWAWATA), Nurdin Lyimo (katikati waliokaa), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma jana, kwenye maadhimisho ya tiba ya asili ya Mwafrika yaliyoandaliwa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Dodoma, ambayo yatahitimishwa leo. Kulia ni mratibu wa mafunzo ya kuinua tiba asili nchini, Ally Maganyari. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TAKUKURU yarejesha mil. 5.5/- mkopo umiza

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, imerejesha Sh. milioni 5.5 za Jumanne Nyamsinyo, zikiwa ni fedha za mkopo umiza kutoka kampuni ya Kihenga Investment Co. Ltd.

Akizungumza jana wakati wa kukabidhi fedha hizo, Naibu Mkuu wa taasisi hiyo mkoani hapa, Manyama Tungaraza, alisema fedha hizo zimerejeshwa kutokana na kuchukuliwa kinyume cha utaratibu.

Alisema Nyamsinyo alifika TAKUKURU kutoa taarifa na kubainika kuna mazingira ya utoaji mikopo yanayofanyika ni kinyume cha mazingira halisi ya utoaji mkopo kwa jamii.

Naibu huyo alisema jitihada zimefanywa na taasisi hiyo kuhakikisha mteja huyo anapata haki yake na kupewa fedha hizo.

"Tunaomba wananchi msisite kuja kutoa taarifa pale mnapoonewa. Kama una uhakika utoaji mikopo una viashiria vya rushwa, basi sogea TAKUKURU nasi tutakulinda," alisema Tungaraza.

Alisema lengo lao ni kuona kila mmoja anapata haki yake ya msingi katika biashara zinazofanyika baina ya mtu na mtu.

Tungaraza alisema wananchi wengi wamekuwa wakidhulumiwa na kukaa kimya bila kutoa taarifa yoyote kwa taasisi ambazo zinauwezo wa kutoa msaada.

Naye Nyamsinyo aliishukuru TAKUKURU kutokana na msaada waliompa kuhakikisha anapata fedha hizo.

Alisema alishakata tamaa kutokana na kuamini tayari fedha zake hizo zimepotea.

# Waganga walia gharama usajili dawa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAGANGA wa tiba asili na tiba mbadala nchini, wamelalamikia gharama kubwa zinazotozwa na serikali kwa ajili ya kusajili dawa zao, hali inayosababisha wengi wao kushindwa kuzimudu.

Wakizungumza na Nipashe katika Maadhimisho ya Tiba Asili ya Mwafrika yanayoendelea jijini hapa, waganga hao waliomba serikali kupunguza gharama hizo ili wasajili dawa zao.

Mwakilishi wa Shekilindi Bosnia Ant-Covid, Bashiru Iddy, ambao ni watengenezaji wa dawa inayotumika mapambano dhidi ya virusi vya corona, alisema kuwa hivi sasa gharama za usajili wa dawa umekuwa kikwazo kikubwa kwa waganga, hali ambayo inasababisha wengi kuuza bila kusajiliwa.

"Tatizo kubwa ni usajili wa dawa hivi sasa upo juu sana. Dawa hii unayoiona tunaiuza hapa kuisajili dawa moja tuu imetugharimu zaidi ya Sh. 600,000. Sasa kwa mtu wa kijijini kweli anaweza kuja kusajili?" Alihoji Iddy. Alisema kupitia Baraza la Tiba Asilia na Tiba Mbadala, serikali inatakiwa kutoa elimu kwa waganga ili kujisajili na kuondokana na vikwazo mbalimbali ambavyo vimekuwa vikiwapata. Pia aliiomba serikali kutenga vitalu na mashamba ya misitu kwa ajili ya uchimbaji wa dawa asili, hali itakayosaidia kuondoa tatizo la uharibifu wa mazingira na uchimbaji wa miti isiyofaa kwa tiba.

Akizungumzia dawa wanayoitengeneza ya Shekilindi Bosnia Ant-Covid, alisema hivi sasa wako katika hatua za mwisho kuomba kibali serikalini ili kuanza kusafirisha na kuuza ndani na nje nchi.

"Tunamshukuru sana Rais (John) Magufuli, kwa kutupa kipaumbele sisi waganga wa tiba ya asili kwani hivi sasa tunatambulika na hata wengi wetu tupo hapa kutokana na serikali kutuamini," alisema Iddy.

Hata hivyo, alisema tatizo ambalo wanakumbana nalo ni uelewa duni kutoka kwa jamii juu ya tiba asili na tiba mbadala.

"Watu wengi hivi sasa bado hawaamini katika tiba ya asili kuwa ni suluhu ya matatizo yao, lakini katika kipindi cha corona, watu wengi walibadili mitazamo yao kwa namna tiba yetu ilivyosaidia watu wengi," alisema. Naye Mwenyekiti wa Waganga Kata ya Nkinga, Igunga mkoani Tabora, Ishila Intenya, alisema pamoja na gharama za usajili wa dawa kuwa juu, wamekuwa wakizungushwa kwa muda mrefu.

Alisema waganga wamekuwa wakihitaji sana dawa zao zisajiliwe lakini mamlaka zinazohusika na hatua hizo zimekuwa zikiwazungusha kwa muda mrefu.

"Unakuta mtu unakwenda kufuatilia kibali unazungushwa hadi miaka miwili na waganga wengi tupo vijijini, hatutaweza kumudu kuzungushwa kwa muda huu inadidi kufanya kazi kienyeji," alisema.





# Kanisa latoa elimu ubunifu kwa jamii

**Na Grace Mwakalinga,** RUNGWE

KANISA la Moravian Jimbo la Kusini lililopo eneo la Mwakaleli katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya, limeanza kutoa elimu ya ubunifu kwa jamii kama njia muhimu ya kusaidia watu kuondokana na umaskini wa fikra kuanzia ngazi ya kaya.

Elimu hiyo inalenga kuiwezesha jamii kuona fursa kwa kutumia fikra bunifu ili kunufaika na rasilimali zinazowazunguka katika maeneo yao na kutumika kama vyanzo vya mapato ili kuondoa dhana ya umaskini kuanzia ngazi ya familia.

Akizungumza jana wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo walengwa wa elimu hiyo, Katibu Msaidizi, Idara ya Ustawi wa Jamii wa kanisa hilo, Mchungaji Lilian Mwambeta, alisema kuwa zaidi ya watu 40 wakiwamo watu wa makundi maalum wamenufaika na elimu hiyo katika Wilaya ya Rungwe, mkoani Mbeya.

Alisema kanisa linakusanya makundi mbalimbali ya watu kwa ajili ya kuwaambia mambo ya Mungu, lakini kanisa linawajibu wa kutoa elimu ya uchumi ili kupunguza umaskini kwa kuwa watu kwa kuwa wana mahitaji mbalimbali kwa ajili maendeleo ya maisha yao.

Akitoa mada kuhusu uchumi kuanzia ngazi ya familia, mwezeshaji wa mafunzo hayo kutoka Shirika la ELIMISHA, Festo Sikagonamo, alisema kuwa jamii inahitaji kupewa elimu zaidi kuhusu tafsiri ya umaskini kwamba ni mtu wa namna gani.

Alisema kuwa jamii nyingi kutokuwa na utamaduni wa kutunza kumbukumbu za rasilimali walizonazo na kuto kutunza kumbukumbu za uzalishaji, wengi wamejikuta wameingia kwenye kundi la umaskini wa kifikra bila wao kujijua.

"Kwa mfano kwa maeneo ya vijijini unakuta kaya moja ina mashamba zaidi ya moja ambayo yana mazao ya chakula na biashara, kama vile chai, kahawa, pamba, mpunga, mahindi na mengine, lakini ukimuuliza mkuu wa kaya kwamba rasilimali zake zina thamani ya kiasi gani hana majibu na bado anajiita maskini," alisema Sikagonamo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo walieleza namna walivyonufaika na elimu hiyo, kuwa utunzaji wa kumbukumbu za uzalishaji na upangaji wa bajeti kuanzia ngazi ya familia unaweza kuleta mabadiliko chanya ya kiuchumi kuanzia ngazi ya kaya iwapo watu watazingatia hilo.

Laiton Mwaituka, mmoja wa washiriki wa mafunzo hayo alisema kuwa katika kaya yake amejaliwa kuwa na mashamba, analima, anafuga lakini bado alikuwa hajui mapato na matumizi yake kwa mwaka na kwamba kupitia mafunzo hayo ameongeza thamani ya maarifa yake.

# Mgombea ajinadi kwa utekelezaji miradi miaka 5

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MGOMBEA ubunge wa Jimbo la Mbeya Vijijini kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM), Oran Njeza, ameanza harakati za kuomba kura kwa wananchi wa jimbo hilo, huku akijivunia miradi ya maendeleo ambayo imetekelezwa na serikali miaka mitano iliyopita.

Kampeni za ubunge na udiwani za Jimbo la Mbeya Vijijini kwa CCM, zilizinduliwa rasmi juzi katika Uwanja wa Mahubiri uliopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi na viongozi mbalimbali wa chama hicho wa mkoa na wilaya walihudhuria.

Akijinadi kwenye mkutano huo, Njeza alisema katika kipindi kilichopita cha uongozi wake, serikali imejenga mradi wa maji ambao ni mkubwa kuliko miradi yote ndani ya jimbo hilo na kwamba utamaliza tatizo la maji katika mji wote wa Mbalizi pamoja na Bonde la Songwe.

Alisema kabla ya mradi huo mji wa Mbalizi ulikuwa unatumia zaidi ya lita 40,000 kwa siku kutoka Mbeya Mjini na kwamba kwa sasa maji hayo yataendelea kuwasaidia wananchi wa Mbeya Mjini.

Vile vile, alisema katika kipindi cha miaka mitano, serikali ilijenga hospitali ya wilaya hiyo pamoja na vituo vitatu vikubwa vya afya ambavyo vimeondoa tatizo la wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma za afya hasa wa vijijini.

"Mwaka 2015 hamkunichagua kwa kuangalia sura bali mlinichagua kwa kuangalia kazi, sasa mnaona kazi nilizofanya, naombeni mniamini tena ili nikawatetee na kuwaombea miradi ya serikalini, Rais wetu Magufuli ni msikivu ndio maana maji haya ya Mbalizi tuliomba siku moja tu sasa yanamwagika," alisema Njeza. Alisema kwenye Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya 2020/2025, miundombinu mbalimbali ya wilaya hiyo imeainishwa kuwa itaboreshwa ikiwamo barabara ya Mbalizi-Shigamba Isongole, ambayo inatarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami.

Alisema zipo pia barabara ambazo zinatengenezwa kuelekea kwenye maeneo mbalimbali ambayo wananchi wanajishughulisha na kilimo ili ziwasaidie kurahisisha usafirishaji wa mazao yao.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Mbeya, Mchungaji Jacob Mwakasole, aliwaomba wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini kuwachagua wagombea wa CCM mwaka huu ili kukamilisha mafiga matatu ambayo yatarahisisha upatikanaji wa huduma.

Alisema kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa, uliofanyika mwaka jana, viongozi wote wa vijiji, mitaa na vitongoji ni wa CCM, hivyo akawataka wananchi kuwachagua wagombea wa chama hicho kwenye uchaguzi mkuu ili kukamilisha safu.

Alisema Rais Magufuli wakati anaingia madarakani mwaka 2015 aliahidi kuwa yeye atakuwa rais wa wanyonge na kwamba kauli hiyo ameitekeleza kwa vitendo miaka mitano kwa kutekeleza miradi mikubwa ambayo inawasaidia wananchi hao.

"Nina uhakika wananchi wa Mbeya Vijijini mtampigia kura Rais wetu Magufuli, hii ni kwa sababu kabla hajaja huku ametuonyesha ni kwa nini anafaa kuchaguliwa tena, miradi tuliyopewa ni kama upendeleo kwetu, sasa naomba mrahisishie kazi kwa kuwachagua mbunge na madiwani wa CCM," alisema Mwakasole.

Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, ambaye ndiye alikuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa kampeni hizo, aliwaomba wananchi wa vyama vyote kumchagua Njeza, Oktoba 28 kwa maelezo kuwa ni mtendaji mzuri.



Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akionyesha kwa waandishi wa habari jijini humo juzi, baadhi ya vyombo vya wizi ambavyo jeshi hilo, lilivikamata katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo na Mji wa Tunduma, mkoani Songwe. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Serikali kuboresha miundombinu ya maji kurahisisha gharama

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI wilayani Kyela katika Mkoa wa Mbeya, imesema inaendelea kuboresha miundombinu ya maji, ili wananchi wapate huduma hiyo kwa urahisi na kwa gharama nafuu kuepuka magonjwa ya mlipuko.

Mkuu wa Wilaya ya Kyela, Cloudia Kitta, aliyasema hayo juzi alipokuwa kwenye ziara ya kukagua vyanzo mbalimbali vya maji yanayotumika wilayani humo ambavyo vingi vinapatikana katika Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe.

Alisema serikali imeipatia Halmashauri ya Kyela pesa nyingi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi mingi na kwamba baadhi ya miradi hiyo imekamilika na mingine ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Kitta alisema, ili miradi inayotekelezwa na serikali iwe na faida kwa wananchi na idumu kwa muda mrefu, ni lazima kila mwananchi ashiriki kwenye utunzaji wa vyanzo vya maji ikiwamo kutokata miti kwenye vyanzo hivyo.

"Tuna miradi mingi sana ambayo asilimia kubwa ya vyanzo vyake vipo Busokelo, sasa ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunavitunza vyanzo hivi kwa kuvitembelea mara kwa mara ili tuwe na uhakika wa kupata maji muda wote," alisema Kitta.

Alizitaka jumuiya za watumia maji wilayani humo kuhakikisha zinakusanya mapato ya kutosha matengenezo ya baadhi ya vifaa kwenye miradi hiyo yawe yanafanyika mara kwa mara.

Baadhi ya wananchi wa wilaya hiyo, waliishukuru serikali kwa kutekeleza miradi ya maji ambayo waliahidiwa kwa madai kuwa kwa sasa huduma hiyo ipo kwa kiwango kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali na walikuwa hawana uhakika wa huduma hiyo. Joseph Mwakifuna, mkazi wa mji wa Ipinda, alisema awali walikuwa wanategemea maji ya visima ambayo usalama wake ni mdogo kwa afya zao, lakini sasa hivi wanatumia majisafi ya bomba.


Alisema kabla ya maji ya bomba kuanza kutumika, mara nyingi wananchi walikuwa wanaumwa matumbo na mlipuko wa kipindupindu ulikuwa unawasumbua hasa kipindi cha mvua yanapoingia kwenye visima.

"Sasa hivi maji ya visima tunayatumia kwa ajili ya kufulia nguo na kuoga, hakuna tena kunywa kwa sababu tuna majisafi ya mabomba na tunahamasishwa kila mwenye uwezo avute bomba nyumbani kwake," alisema Mwakifuna.

Alisema hata katika Kituo cha Afya cha Ipinda ambacho ni miongoni mwa vituo bora vya afya katika Mkoa wa Mbeya, maji ilikuwa ni tatizo kubwa awali, lakini kwa sasa yapo ya kutosha.

Mwaka jana Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, alifanya ziara ya kukagua miradi ya maji katika wilaya hiyo na kuzindua mradi wa maji wa Kapapa Group, ambao umegharimu zaidi ya Sh. bilioni 3.5.

Mradi huo unaanzia katika chanzo kilichopo Busokelo wilayani Rungwe na unahudumia wananchi zaidi ya 13,000 wa vijiji vinane kutoka katika kata nne za Ipinda, Mwaya, Talatala na Ikama.



# Msajili wa vyama aombwa kubaini vyama 'vikorofi'

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimemtaka Msajili wa Vyama vya Siasa kufanya utafiti ili kubaini chama cha siasa Tanzania Visiwani na Bara kinachotumia fursa ya uwanja wa siasa katika kuleta uvunjifu wa amani.

Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Abdullah Juma Sadala (Mabodi), aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za chama hicho, Kisiwandui mjini Zanzibar.

Alisema msajili ndio msimamizi na mlezi wa vyama hivyo ana wajibu wa kufanya utafiti huo ili kuvibaini vyama ambavyo vina nia ya kuleta fujo, vurugu vituko na uvunjifu wa amani hasa katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi mkuu.

"Namwambia Msajili afanye utafiti wa kina na ikiwezekana achukue hatua inayostahiki kwa chama ambacho kinaashiria kuzungumza kauli au vitendo vya uvunjifu wa amani, fujo vituko na ubadhirifu wa mali za umma hapa Tanzania," alisema.

Mabodi alisema, CCM imegundua viashiria vya kauli na vitendo ambavyo vinafanywa na baadhi ya wanasiasa na kushawishi wananchi kutaka kufanya fujo.

Alisema CCM inasikitishwa na kauli za uchochezi zinazotolewa na watu ambao wamo katika vyama vya upinzani nchini kwa ajili ya kuchafua amani iliyodumu kwa muda mrefu.

"Kama tulivyoona uongozi wa Dk. Ali Mohamed Shein tumesimamia amani ya nchi kwa nguvu zote na tumeona matunda yake, hivyo wananchi msikubali kushawishiwa na hoja ambazo hazitakuwa na msimamo zenye fikra mgando kwa kuwa zitasababisha kuturudisha nyuma baada ya kwenda mbele," alisisitiza.

Alisema CCM ilikubali kwenda katika mfumo wa vyama vingi vya siasa kwa ushindani kwa kushindana na sera na sio kauli ambazo hazina dhamira njema na wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

"Tanzania tumekubali ushindani wa vyama vingi ili kuwe na vyama mbadala vya kutoa mawazo, lakini kuikosoa CCM ambayo ndio inayoongoza dola kwa sehemu ambazo zinastahiki kukosolewa, tunajenga nyumba moja ya utanzania na sote tunapita katika reli moja, hivyo hatuta stahamili mtu yeyote mwenye nia ya kuiondoa amani ya nchi yetu," alisema.

Alisema CCM inaahidi kufanya kampeni na hamasa za kisayansi zitakazoendeleza amani na utulivu nchini kama ilivyokuwa kabla ya uchaguzi.

Hata hivyo, alisema ana imani kuwa uchaguzi wa Oktoba mwaka huu, utakuwa huru na haki.

Akizungumzia mgombea urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hicho, alisema CCM itahakikisha mgombea wake Dk. Hussein Mwinyi, anakubalika na ahadi anazozitoa kwa wananchi wa Zanzibar.

"CCM tumeshaanza kampeni zamani kwa kuwa utekelezaji wa ilani yetu chini ya uongozi wa Dk. Shein imefanya kazi vizuri na hata mambo ambayo hayamo katika ilani, hii mpya itamgusa mtu mmoja mmoja kuanzia ajira, uchumi na masuala mengine ya kijamii," alisema.

Alisema hayo yasingepatikana kama si kuthamini Mapinduzi, Muungano, utu na utaifa ambayo yamo katika kifungu kimoja cha amani, mshikamano, utulivu na ulinzi wa nchi hivyo CCM itasimamia hayo kabla na baada ya kampeni.

Alikipongeza Chama Cha Mapinduzi kwa ukomavu wake na viongozi huku akivisihi vyama vingine kutoibeza amani ya nchi ambayo ndio lulu kubwa kwa taifa la Tanzania.

Aliwataka wagombea wa nafasi za udiwani, uwakilishi na ubunge kupitia chama hicho kuhakikisha wanapofanya kampeni kutoa ahadi kwa wananchi zinazotekelezeka ili waendelee kukiamini chama chao.



Mtakwimu wa Kitengo cha Takwimu za Bei katika Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Salma Saleh Aliy, akiwasilisha taarifa ya mfumuko wa bei kwa mwezi Agosti 2020, kwa waandishi wa habari, Mazizini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kasi ya mfumuko wa bei yashuka Visiwani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KASI ya mfumuko wa bei kwa mwezi Agosti imeshuka visiwani hapa ambayo ilikuwa asilimia 2.4 ikilinganishwa na 3.6 kwa mwezi wa Julai, mwaka huu.

Mtakwimu wa Kitengo cha Takwimu za Bei, Salma Saleh Ali, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari mjini hapa. Alisema bei za chakula na vinywaji visivyo na kilevi imeshuka kwa asilimia 4.9 Agosti ikilinganisha na 6.7 Julai.

Alisema miongoni mwa vyakula vilivyoshuka ni pamoja na mchele wa Mbeya, mchele wa pembe, unga wa sembe, ndizi mbichi, samaki, mafuta ya taa na saruji.

Meneja wa Idara ya Uchumi Tawi la Zanzibar (BOT), Moto Ngwinganele, alisema hali iliyosababisha mfumuko wa bei kushuka ni kuwapo kwa chakula cha kutosha.

Alisema kwa upande wa mafuta ya taa, dizeli na petroli yameshuka kutoka soko la dunia kwa sababu ya ugonjwa wa corona.

Vile vile, alisema malengo ya serikali ni kuona wananchi wanaendelea kupata bidhaa kwa bei nafuu, ili waweze kujikwamua kimaisha na kumudu kununua bidhaa ambazo zimeshuka katika masoko yote.

## Walimu watakiwa kutimiza wajibu wao

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Idara ya Elimu Sekondari wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Asiya Iddi Issa, amewataka walimu wa sekondari kutimiza wajibu wao muda wa kazi ili kuleta ufaulu mzuri kwa wanafunzi.

Alisema kumekuwapo na tabia ya baadhi ya walimu kuacha kusomesha muda wa kazi na kufundisha muda wa ziada (tuisheni), jambo ambalo linawanyima haki ya msingi baadhi ya wanafunzi.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika mkutano wa pamoja na maofisa elimu kutoka Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali na wenyeviti wa kamati za wazazi wa shule za mkoa wa Mjini Magharibi.

Alisema kufanya hivyo kunawasababishia wazazi wasiokuwa na uwezo wa kulipia masomo ya ziada na kuwaweka katika wakati mgumu watoto wao.

Alisema kuna baadhi ya walimu wanasomesha vizuri katika masomo ya ziada, lakini wanapokua shuleni wanafundisha kwa kulipua.

Alisema zipo baadhi ya shule pia zimeanzisha masomo ya ziada bila kuwa na usimamizi maalum wa masomo hayo na kusababisha wanafunzi kujiingiza katika vishawishi na kushuka kwa kiwango cha ufaulu.

Aliwataka wenyeviti hao kusimamia na kufuatilia ipasavyo maendeleo ya shule na kuwahimiza walimu wakuu kuwasimamia walimu wao kufundisha ipasavyo, ili wanafunzi wapate haki yao ya msingi ya kupata elimu.

Naye ofisa kutoka Idara ya Elimu Sekondari, Mussa Abdurabi, alisema ushirikiano mzuri baina ya kamati za shule, walimu wazazi na jamii yatasaidia kuleta matokeo mazuri ya wanafunzi katika mitihani yao.

Alisema kamati za shule zina nafasi kubwa katika maendeleo ya shule kwa kuhakikisha wanafunzi wanapata haki yao.

Pia, alisema ingawa taifa limepitia katika kipindi kigumu cha ugonjwa wa corona na kusababisha shule kufungwa, lakini Idara kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu Zanzibar ilihakikisha kuwa elimu inapatikana katika kipindi hicho. Aliwataka walimu kuhakikisha wanafuata maelekezo yaliyotolewa na wizara kwa kwenda kufundisha hadi siku za Jumamosi na kumeripotiwa baadhi ya walimu hawafuati agizo hilo na kuwaacha wanafunzi pekee wakiwa shuleni.

Wenyeviti wa kamati za shule waliiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuunda kamati madhubuti ya kutembelea masomo ya ziada yanayoanzishwa katika shule kwa lengo la kuangalia ubora wake, ili kuwasaidia wanafunzi kusoma katika mazingira mazuri na kupata ufaulu mzuri.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA, K**IWANJA CHA COMMERCIAL 1300SQM KINAUZWA KIPO REGENT ESTATE HAKUNA DALALI TUPIGIE: 0693 689996/ 0757 129546

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba ya gorofa moja inauzwa, ina frem 3 za biashara zote zinawapangaji. Ipo ukonga Dar es salaam. Simu 0757 07 90 57.

## MATANGAZO MCHANGANYIKO

**FAITH BACKBORN CLINIC!!** TUNATIBU UTI WA MGONGO DISC PROBLEM KIUNO SELLULITIES GANZI PARALIZE BODY MEDICATED FULLBODY MASSAGE AND HOME SERVICES AVAILABLE 0714 919199

*NIPASHE NI JIBU LAKO*

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## PASSPORT IMEPOTEA



115885402

**MWESIGA ERICK ISHENGOMA** anatangaza kupotelewa na Hati ya Kusafiria (Passport) yenye namba **AB725255** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam mwaka 2015. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu. Taarifa ya polisi: **DSM/PHQ/RB/640725/2020.**

## KUPOTEA KWA CHETI



215884902

**MARON RAPHAEL MBISE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0980-0055** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KING'ORI SEKONDARI** mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **NAC/RB/1711/2011.**

## KUPOTEA KWA KADI

**Subira Kasimu Kasitu** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya Mitsubish Canter yenye namba ya usajili **T930 DGJ** iliyotolewa na Mamlak ya mapato Tanzania. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/KJN/RB/638545/2020**

115884702

## KUPOTEA KWA KADI YA TRAILER

**CREN TRANSPORT AGENT CO. LIMITED** INATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA TRAILER YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 387 CVD.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/CEN/RB/634208/2020.**


115885502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DORICA G. GWICHALA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA CAMI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 990 BKL.** KWA YOYOTE ATAKAYE IONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/623440/2020.**

115885802

## KUPOTEA KWA CHETI



115885102

**ELLY GODSON MSHANA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0558-0059** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MWANGA SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/TAB/RB/630336/2020.**

*Uza,*

*Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa*

*Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe

MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Chuo Mwalimu Nyerere chaita walio mbali kujiunga masomo

**Na Romana Mallya**

CHUO cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam, kimewataka wazazi au walezi wenye vijana walio na sifa za kujiunga na chuo hicho na wako mbali, milango iko wazi.

Mhadhiri na Mkuu wa Idara ya Uongozi na Maadili ya Chuo hicho, Dk. Samuel Lunyelele, aliyasema hayo jana katika viwanja vya Mnazi Mmoja kwenye maonyesho ya Vyuo Vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Dk. Lunyelele alisema kwa muda wa siku tatu tangu maonyesho hayo yaanze mwishoni mwa mwezi uliopita, wamepokea wazazi na walezi wengi wenye watoto walioko mbali wakitaka kujua namna ambavyo vijana wao wanaweza kujiunga na chuo hicho.

"Tumehudumia idadi kubwa ya vijana wanaotaka kujiunga na elimu ya juu, lakini wapo wazazi na walezi wengi ambao wamejitokeza kuja kuulizia utaratibu wa namna watoto wao wanaweza kujiunga na chuo hiki," alisema.

Dk. Lunyelele alitoa wito kwa vijana ngazi ya cheti, stashahada na shahada ambao wanataka kujiendeleza zaidi kielimu na wana sifa zote, wajitokeze ili kupewa mwongozo wa namna ya kujiunga.

Mwanafunzi wa mwaka wa pili anayesomea Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kutoka chuoni hapo, Jumbe Ismail, alisema amefika kwenye maonyesho hayo kuhamasisha vijana wabunifu kukuza vipaji vyao.

Alisema pamoja na kwamba anaendelea na masomo chuoni hapo, amebuni mfumo wa kuzuia wizi kwa njia ya dirisha.

Ismail alisema mfumo huo ameubuni baada ya kubaini kuwapo kwa vitendo vya wizi mdogo mdogo kwa kutumia dirisha kama vile simu na vitu vingine vyenye thamani.

"Endapo tukio la wizi litafanyika nyumbani mfano mwizi anakata nyavu ili afanikisha wizi, mfumo huu utamtaarifu mhusika kwa njia ya simu ya kijanjani," alisema.



Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Hadija Mcheka (kushoto), akizungumza na walimu wakuu na viongozi wa shule za sekondari za mkoa huo, wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo kwa kutoa elimu kwa wanafunzi yaliyoratibiwa na Shirika lisilo la Kiserikali la GESCI, mjini Kibaha jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Shule yaweka vifaa vya kisasa zimamoto

**Na Mwandishi Wetu**

SHULE ya Msingi Hazina ya jijini Dar es Salaam, imeweka vifaa vya kisasa vya kuzimia moto kama hatua ya kuwahakikishia usalama wanafunzi.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Shule hiyo, Omary Juma, alisema wamechukua uamuzi huo ili kuhakikisha usalama wa wanafunzi kutokana na matukio ya moto.

Juma alisema miaka ya hivi karibuni kumekuwa na matukio ya mabweni na shule kwa ujumla kuungua hivyo hatua waliyochukua ni kujihami endapo moto utatokea.

"Vifaa hivi ni vya kisasa kutoka Ujerumani na Hazina imekuwa shule ya kwanza Tanzania kununua vifaa vya aina hii kwa ajili ya kuwalinda wanafunzi wetu na mali zao kwa ujumla," alisema.

Alisema vifaa hivyo vimewekwa kwenye maeneo mbalimbali ya shule ikiwamo madarasani na kwenye mabweni kwa ajili ya kuzimia moto unapotokea.

"Hiki kifaa ni kama mpira ambao ukirushwa sehemu unapowaka moto kinalipuka na kuzima moto wote kabisa. Ni kifaa cha kisasa ambacho kitasaidia kuepukana na majanga ya moto yanapotokea tunashukuru uongozi kwa kuona umuhimu wa kuweka vifaa hivi," alisema.

Shule nyingi zimekuwa zikiungua na kusababisha hasara kwa shule na wakati mwingine vifo na madhara kwa wanafunzi. Matukio ya hivi karibuni ya moto yametokea katika shule sita za sekondari mkoani Arusha na kuzua sintofahamu.

Ilianza kuungua Shule ya Sekondari Lowassa iliyoko Monduli, Nanja na Longido Sekondari zilizoko wilayani Longido, Sokoine (Monduli), Mlangarini wilayani Arumeru na Shule ya Sekondari Winning Spirit. Pia Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Engutoto, nayo iliingua moto mwanzoni mwa mwaka huu.

Mwaka jana Shule ya Sekondari Lindi, nayo iliungua moto na kusababisha madarasa tisa, samani, ofisi nne za walimu, maabara mbili za kemia na fizikia na madawati 300 kuteketea kwa moto.

Februari mwaka huu, majengo mawili ya Shule ya Sekondari Iyunga iliyoko mkoani Mbeya, yaliungua moto na kusababisha magodoro, nguo na vifaa vingine vya wanafunzi kuungua.

Mwaka 2008 mabweni ya Shule ya Sekondari ya Wasichana Mkalamo iliyoko Wilaya ya Korogwe, mkoani Tanga yaliteketea pamoja na vifaa mbalimbali vya wanafunzi ambapo lilikuwa ni tukio la pili kutokea shuleni hapo.

**Vifaa hivyo vimewekwa kwenye maeneo mbalimbali ya shule ikiwamo madarasani na kwenye mabweni kwa ajili ya kuzimia moto unapotokea.**

# Serikali yawaangukia wadau wa utalii

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

WIZARA ya Maliasili na Utalii imewaomba wadau wa sekta ya utalii nchini kujikita kutangaza maeneo ya malikale zaidi ya 100 yaliyopo nchini ambayo hayapewi kipaumbele licha ya kuingizia mapato serikalini.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, kwenye kikao cha kujadili hali ya uhifadhi na uendelezaji wa maeneo ya malikale yaliyokasimishwa kisheria.

Alisema tangu kuanzishwa idara ya malikale maeneo 500 yalibainika na 133 kutangazwa, lakini 18 pekee ndiyo yanayotumika na kusisitizia jitihada zaidi zifanyike kuyatangaza ili yaweze kuwa chachu ya mapato kwa taifa.

"Niwaombe wadau wa utalii na wananchi kwa ujumla kuthamini malikale tulizonazo kwa sababu tukizitangaza vizuri tutaongeza pato la taifa maradufu zaidi ya ilivyo sasa na tumetilia mkazo maeneo 18 tu kati ya 133 yanayotambulika nchini," alisema Dk. Nzuki.

Alisema kuwa vivutio vilivyopo katika maeneo ya mali kale ndio yamekuwa yakivutia watalii wengi duniani ambao mara nyingi wanatamani kujifunza historia ya miaka ya zamani namna binadamu walivyokuwa wakiishi.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa masuala ya sera idara ya malikale, Dk. Fabian Kigadye, alisema pamoja na kuwapo kwa maeneo mengi ya utalii, bado hayatumiki ipasavyo katika kuukuza.

Alisema maeneo mengi ya utalii malikale hajayahifadhi vizuri, jambo ambalo linafanya watu wengi kutoona umuhimu wake na kuwataka watumishi wa idara hiyo kufanyia kazi changamoto hiyo.

"Maeneo mengi ya malikale tulionayo bado hayajahifadhiwa ipasavyo katika kuwavutia watalii wanaokuja hivyo ni lazima kila mhifadhi atumie nafasi aliyonayo katika kuboresha mazingira ya malikale hizo ili malengo yetu yaweze kutimia," alisema Dk. Kigadye.

# Mahakama Tanzania yapongezwa utekelezaji mradi wa hakimiliki

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Hakimiliki Duniani (WIPO), limeipongeza Mahakama ya Tanzania kwa mafanikio katika utekelezaji wa mradi wa hakimiliki nchini.

Akizungumza katika mkutano wa nchi wanachama uliofanyika kwa njia ya video 'video conference', Septemba Mosi, mwaka huu, Ofisa Programu wa WIPO, Alexandra Bhattacharya, aliisifu Mahakama kwa utekelezaji mzuri wa mradi huo na kuahidi kuendelea kufanya kazi kwa ukaribu zaidi.

"Napenda kuipongeza Mahakama ya Tanzania kwa kujitoa kwa dhati kupigania mradi huu kuwa ajenda ya mahakama na ya kitaifa kwa ujumla," alisema Bhattacharya.

Katika mkutano huo, Mahakama ya Tanzania ilitoa uzoefu wake katika utekelezaji wa mradi wa Hakimiliki kwa nchi wanachama wa shirika hilo. Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Elieza Feleshi, Mkuu wa Kitengo cha Maboresho ya Mahakama walishuhudia wasilisho hilo.




# BALE AFIKIRIA KURUDI EPL

**MADRID,** Hispania

GARETH Bale anafikiria kurudi Ligi Kuu ya England na ameilaumu Real Madrid kwa kushindwa kumruhusu kuondoka klabuni hapo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales amecheza mechi 20 tu katika mashindano yote msimu uliopita na aliachwa kwenye kikosi kilichocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya Manchester City.

Alikaribia kuondoka na kwenda kwenye Ligi Kuu ya nchini China, Super League, mwaka jana, lakini Madrid ilisitisha uhamisho huo saa 11 baadaye.

Na amekuwa akihusishwa na kuwaniwa na klabu za Manchester United na timu yake ya zamani ya Tottenham Hotspur. Lakini sasa Bale amebainisha kwamba amehuzunishwa na namna Madrid ilivyoshindwa kumruhusu aondoke.

"Nilijaribu kuondoka mwaka jana, lakini walisitisha uhamisho wangu katika dakika ya mwisho kabisa," alisema akiiambia Sky Sports.

Alipoulizwa kama ana mpango wa kurudi kwenye Ligi Kuu ya England, Bale alisema: "Kama itatokea, ni kitu ambacho nitakianglia kwa uhakika kabisa. Tutaona nini kitatokea."

# Henderson amwonya De Gea Man Utd

**MANCHESTER,** England

DEAN Henderson amemwonya, David de Gea kwamba yeye anataka kuwa golikipa chaguo la kwanza katika kikosi cha Manchester United.

Baada ya kuwa na msimu wa kuvutia akicheza kwa mkopo kule Sheffield United msimu uliopita, Henderson amerudi pale Old Trafford na amesaini mkataba wa miaka mitano mwezi uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye bado hajawahi kuichezea timu ya wakubwa ya Manchester United, alianza katika mechi 36 za Ligi Kuu England msimu wa 2019-20.


Na Henderson amesema anataka kocha Ole Gunnar Solskjaer amfanye kuwa chaguo la kwanza dhidi ya De Gea ambaye aliyefanya makosa kadhaa ya wazi msimu uliopita.

"David de Gea ni golikipa mkubwa na amecheza kwenye kikosi cha kwanza kwa miaka mingi. Ni mtu wa aina yake," alisema Henderson akiwaambia waandishi wa habari.

"Kitu ambacho hata mimi nataka kuwa hivyo kwenye klabu hii, na kwa sasa nataka kuwa na nafasi ya kuanza kwenye kikosi cha kwanza.

"Siwezi kukata tamaa, kwani nimejipanga kuhakikisha nakuwa chaguo la kwanza. Namheshimu David, lakini naamini huu ni wakati wangu."

Henderson amecheza kwa mkopo Stockport County, Grimsby Town, Shrewsbury Town na Sheffield United kwa misimu ya hivi karibuni.







# *Rakitic: Nitaipaisha Sevilla kwenye LaLiga*

**SEVILLA,** Hispania

IVAN Rakitic ana matumaini ya kuirudisha Sevilla kwenye changamoto ya kupambania taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, baada ya kurudi hapo "nyumbani" baada ya miaka sita ya kucheza kule Barcelona.

Rakitic mwenye umri wa miaka 32, alikamilisha usajili wa kurudi Sevilla Jumanne na ilithibitishwa kwamba amesaini mkataba wa miaka minne, huku klabu hiyo ya Andalusia ikilipa ada ya awali ya euro milioni 1.5, huku ikitarajiwa kukamilisha kiasi cha uero milioni tisa kama ataonyesha kiwango cha juu zaidi.

Uhamisho huo wa Rakitic umemfaya arudi nyumbani ambako ndiko alikojiimarisha yenye mwenyewe na kuwa mmoja wa viungo bora barani Ulaya alipoichezea kwa kipindi cha misimu mitatu, akiwasaidia kushinda taji la Ligi ya Europa msimu wa 2013-14.

Na hilo ndilo likawafanya Barca wamsajili Rakitic ambaye alinyanyua mataji 13 kwa kipindi alichocheza pale Catalunya, na sasa ana matumaini ya kuipaisha Sevilla.

"Kwa heshima zote, nipo na washindi mara sita wa Kombe la Ligi ya Europa na tupo tayari kutoa changamoto kwenye LaLiga," alisema Rakitic wakati akitambulishwa kwa waandishi wa habari, Jumatano.

"Lakini nataka tufike hatua ya mbele zaidi, kwenye LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya. Wote tunajua nini maana yake, kwani ni jambo muhimu kufika katika hatua kama ile."

# Rais Napoli: Koulibaly, Milik wanaondoka

**NAPLES,** Italia

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis amethibitisha Kalidou Koulibaly na Arkadiusz Milik wataondoka kwa ofa inayotakiwa.

Koulibaly amekuwa akihusishwa na uhamisho wa kwenda Manchester City, huku AS Roma ikiripotiwa kuongoza kwenye mbio za kumwania kumsajili Milik.

Akizungumza Jumatano, De Laurentiis alisema wawili hao wataondoka Napoli kwa ada inayotakiwa.

"Koulibaly na Milik wote wanaondoka, soko linaruhusu," alisema akiiambia Canale 21.

"Hivyo, kama soko linaruhusu hali hiyo, wote wataondoka na tutajua namna ya kuwatafuta warithi wao.

"Vinginevyo tutazungumza kuhusu wao mwakani."

Koulibaly mwenye umri wa miaka 29, amejiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora wa kati tangu alipotua Napoli akitokea Genk mwaka 2014.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal mkataba wake unamalizika mwaka 2023, lakini amekuwa akihusishwa na mpango wa kundoka kwa pauni milioni 57.7 kwenda Man City.

Milik, ametumia misimu minne akicheza Napoli na kufunga mabao 14 katika mechi 35 alizocheza msimu wa 2019-20.





# TONALI KAITOSA BARCA ATUE MILAN – CELLINO

**MILAN,** Italia

SANDRO Tonali alikataa ofa ya kujiunga Barcelona na Manchester United kwa sababu alitaka kwenda AC Milan, kwa mujibu wa Rais wa Brescia, Massimo Cellino.

Tonali ambaye ameichezea timu ya Taifa ya Italia mechi tatu na kung'ara kule Brescia msimu wa 2019-20, lakini klabu hiyo ilishuka daraja kutoka Serie A.

Dogo huyo mwenye umri wa miaka 20, ambaye anatajwa kuwa nyota wa baadaye wa Italia, alikuwa akihusishwa na Inter Milan, lakini sasa anajiunga na AC Milan.

Cellino amesema Tonali alikuwa tayari kujiunga na Milan licha ya ofa kutoka Barcelona na United.

"Januari tulipata ofa ya euro milioni 65 kutoka Barcelona. Siku 10 baadaye tulipata ofa yenye ongezeko la euro milioni 10 kutoka Manchester United," alisema akiiambia Top Calcio 24.

"Lakini kijana aliamua kwenda kwa 'Rossoneri'."

Cellino aliongeza: "Najua kwamba, (Antonio) Conte alikuwa anamfuatilia sana Tonali, na mimi pia nilishawishika kuwa atakwenda Inter."

# *Van de Beek rasmi atua United*

**MACHESTER,** England

MANCHESTER United imekamilisha usajili wa kiungo wa Uholanzi, Donny van de Beek kutoka Ajax kwa ada ya uhamisho ambayo inaweza kupanda hadi pauni milioni 39.1.

United italipa ada ya awali ya pauni milioni 34.7 kwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye amesaini mkataba wa miaka mitano, huku kukiwa na kipengele cha kuongeza miezi 12 na kuwa mchezaji wa kwanza kwa kocha, Ole Gunnar Solskjaer kumsajili msimu huu wa 2020-21.

Van de Beek alikuwa mmoja wa nyota walionyesha kiwango cha kuvutia sana wakati Ajax ikitinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2018-19.

Hata hivyo, sasa amefuata nyayo za wachezaji wenzake, Frenkie de Jong, Matthijs de Ligt na Hakim Ziyech kununuliwa kwa kitita kikubwa cha fedha na kuondoka hapo kwenye dimba la Johan Cruijff Arena, huku pia akiachwa kwenye mchezo wa kirafiki wa wikendi iliyopita wa Ajax dhidi ya Eintracht Frankfurt.

"Siwezi kuelezea namna gani nina furaha ya kujiunga na klabu kama hii ambayo ina historia ya kuvutia," alisema akiiambia tovuti ya United.

"Ningependa kumshukuru kila mtu pale Ajax. Nimekuwa pale na mara zote nitaendelea kuwa na mahusiano mazuri na klabu ile.

"Sasa nipo tayari kuchukua hatua inayofuata na kucheza kwa kiwango cha juu na hakuna sehemu nyingine zaidi ya Manchester United.

"Kila mtu ameniambia namna gani hapa Old Trafford palivyo na historia ya kuvutia, natarajia mengi na kupata uzoefu zaidi. "Timu ina baadhi ya viungo bora duniani na najua kwamba naweza kujifunza kutoka kwao na pia kuimarisha kundi hili.

"Nikiwa nimezungumza na kocha kuhusu maono yake kwa timu, mwelekeo wa klabu hivyo nafurahia kuwa sehemu ya kundi hili."

Van de Beek amecheza mechi 175 kwa kikosi cha kwanza cha Ajax baada ya kutokea timu ya vijana na amefunga jumla ya mabao 41.

Sasa atatakiwa kujiimarisha yeye mwenyewe kwenye safu ya kiungo akiungana na Bruno Fernandes na Paul Pogba.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# RAMOS AMGEUKIA MESSI ABAKI BARCA

●●● Si jambo linalotuhusu, lakini kwa faida ya LaLiga, Clasico tungependa kumuona akibaki...

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa Real Madrid, Sergio Ramos, ana matumaini nyota wa Barcelona, Lionel Messi atabakia na 'Blaugrana' hao kwa mazuri ya LaLiga, wakati baba mzazi wa raia huyo wa Argentina akijaribu kutaka mwanawe aruhusiwe kuondoka.

Messi wiki iliyopita aliwasilisha maombi ya kutaka kuondoka klabuni hapo na baba yake Jumatano alifanya mkutano na Barcelona, ambao haukufikiwa muafaka wowote.

**Ramos aliulizwa kuhusu hali ilivyo hivi sasa pale Barcelona wakati Messi akitaka kuondoka katika klabu hiyo aliyokaa nayo kwa kipindi cha miaka 20.**

"Si jambo linalotuhusu sana (Madrid)," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Ameamua kuangalia maamuzi yake na majaliwa yake ya siku za usoni.

"Lakini sijui kama anafanya uamuzi bora kwa upande wake, soka la Hispania, kwa Barcelona na kwa upande wetu sisi (Madrid), tungependa kumuona akibaki pale.

"Itafanya LaLiga na timu yake kuwa bora, na mchezo wa Clasico kuwa mzuri zaidi. Naona kwamba ni vizuri zaidi akabaki pale alipo sasa.

"Kuna uvumi mwingi, ngoja tusubiri nini kitatokea. Kwetu sisi sio habari ya kuhofia sana."

## ZISIKUPITE

### MESSI ABADILI MAAMUZI

HABARI kutoka nchini Argentina zinabainisha kwamba mshambuliaji wa Barcelona, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 33, anafikiria kubadilisha uamuzi wake wa kuondoka klabuni hapo. ***(TyC Sports, via Mirror)***

### UNITED YAITIWA ALCANTARA

Bayern Munich imeialika Manchester United kwa ajili ya mazungumzo ya kiungo wa Hispania, Thiago Alcantara mwenye umri miaka 29. ***(ESPN)***

### GARCIA KUONDOKA CITY

MLINZI wa Hispania, Eric Garcia mwenye umri wa miaka 19, amesema ataondoka Manchester City wakati mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa msimu huu. ***(Sun)***

### RAIS BARCA AMKAZIA MESSI

RAIS wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, pia amesema klabu hiyo haitafanya majadiliano ya makubaliano ya kumuuza Lionel Messi mwenye umri wa miaka 33. ***(Marca)***

### HENDERSON AIONYA UNITED

GOLIKIPA Dean Henderson mwenye umri wa 23, ameionya Manchester United kwamba ataondoka klabuni hapo kama atacheza kama chaguo la pili mbele ya David de Gea, licha ya kutia saini mkataba mpya utakaomweka pale Old Trafford hadi mwaka 2025. ***(Mail)***

### KOEMAN AMTAKA WIJNALDUM

KOCHA mpya wa Barcelona, Ronald Koeman ameitaka klabu hiyo kufanya kadri inavyoweza kumsajili kiungo wa Liverpool na Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 29. ***(ESPN)***

### VILLA, NEWCASTLE KWA WILSON

ASTON Villa itakabiliana na ushindani kutoka kwa Newcastle katika mbio za kuwania kumsajili straika wa Bournemouth na England, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 28. ***(Telegraph)***

### MESSI, BARCA HAKIELEWEKI

MKUTANO wa kwanza wa Barca na baba mzazi wa Lionel Messi, ambaye pia ni wakala wake, Jorge, tangu mwanawe aombe kuondoka klabu hapo umemalizika bila kufikia makubaliano. ***(Mundo Deportivo)***

### PSG YAJITOA KWA GUENDOUZI

PARIS St-Germain imejiondoa kwenye nafasi ya kumsajili kiungo wa Ufaransa, Matteo Guendouzi mwenye umri wa miaka 21 kutoka Arsenal. ***(Telegraph)***

### HUGUAIN AWINDWA DC UTD

KLABU ya DC United inawania kumsajili mshambuliaji wa Juventus, Gonzalo Higuain mwenye umri wa miaka 32, na pia inamtaka kiungo wa Everton, Gylfi Sigurdsson raia wa Iceland mwenye umri wa miaka 30. ***(The Athletic)***

### WATFORD KURUHUSIWA

KLABU ya Watford inaweza kufikiria kumruhusu straika wa Uingereza, Troy Deeney mwenye umri wa miaka 32, kuondoka kwa mkopo na kumuita tena kama watapanda kurudi Ligi Kuu ya England. ***(Telegraph)***

## 'Ligi Kuu Bara kivutio Kenya'

**Na Adam Fungamwango**

KIPA mpya wa Azam FC, David Kissu, amesema wachezaji wengi wa Kenya, wamekuwa wakiifuatilia sana Ligi Kuu ya Tanzania Bara na wamekuwa wakitamani siku moja wacheze, kutokana na kutangazwa mno, kuonyeshwa kwenye televisheni, pamoja na msisimuko wa mashabiki wake.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, kipa huyo Mtanzania ambaye amejiunga na Azam akitokea Gor Mahia ya Kenya, amesema kuwa Ligi Kuu Bara imekuwa maarufu sana nchini Kenya, kutokana na mechi nyingi kuonyeshwa kwenye televisheni, tofauti na ligi ya Kenya ambayo ni mechi chache tu ambazo zimekuwa zikionyeshwa, hasa zile kubwa.

"Wachezaji wengi wa Kenya wanaipenda sana kwa sababu inaonyeshwa sana, kiasi kwamba wachezaji wengi wa Tanzania wanakuwa maarufu kuliko wa Kenya, hata kama hawana uwezo mkubwa kama wa kwao. Mchezaji wa Kenya anaweza kuwa na uwezo mkubwa, lakini asiwe maarufu mitaani, labda kwa wale tu ambao wanafuatilia sana mpira, lakini mchezaji wa Tanzania hata akifika Mtwara kutoka Dar es Salaam, anajulikana na anakuwa maarufu kwa sababu kila mara anaonekana kwenye televisheni, hiyo ndiyo tofauti kubwa na ndiyo maana wachezaji wa Kenya wanapenda kucheza ligi ya Tanzania," alisema Kissu.

Kuhusu soka la uwanjani, alisema kuwa Kenya hutumia zaidi nguvu kwenye uchezaji wao, tofauti na soka la Tanzania ambalo baadhi ya timu hutumia nguvu, lakini nyingi hucheza kwa ufundi zaidi.

## JKT Tanzania yaipania Kagera

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa JKT Tanzania, Abdallah Mohammed 'Bares', amesema changamoto ya muda wa maandalizi haijaathiri mipango yao ya kuandaa kikosi chao kwa msimu wa 2020/21, na ana uhakika wa kuanza vema mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Bares alisema muda mfupi wa maandalizi haujaharibu mipango yake ya kuhakikisha anaandaa kikosi chenye ubora.

Alisema suala la muda ni kwa timu zote, lakini ana imani timu yake itafanya vizuri kutokana na usajili wa wachezaji waliowaongeza kutoka timu ambazo zilikuwa katika Ligi Kuu.

"Kwa kipindi kifupi tumefanikiwa kujenga kikosi, si kwa kiwango kikubwa, nina imani na wachezaji wangu kufanya vizuri katika mechi zetu zote tukianzia dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Kaitaba, Nukoba," alisema Bares.

Alisema wanawaheshimu Kagera na ana imani utakuwa mchezo wa ushindani ila mipango yake ni kuhakikisha timu yao hiyo inafanya vizuri katika michezo yake yote, ili waendelee katika mikikimikiki ya Ligi Kuu.

"Suala la ubingwa huko hatuwezi kulisema kwa sasa, ila mipango yangu ni kufanya vizuri katika michezo yote kwa ajili ya kujiweka katika nafasi za juu na kuendelea kucheza ligi," alisema Bares.

# GWAMBINA YATAMBIA NYOTA WAZOEFU VPL

**Na Saada Akida**

LICHA ya ugeni wao kwenye Ligi Kuu Bara, Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Fulgence Novatus, amesema ugeni huo ni jina tu, lakini wachezaji walionao kikosini ni wazoefu wa ligi hiyo na watatoa upinzani mkubwa.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Fulgence alisema hawana ugeni katika ligi hiyo kwa sababu timu hiyo imesajili wachezaji wazoefu wenye uwezo wa kuhimili mikikimikiki ya Ligi Kuu kutokana na ukweli kwamba wengi wao wameshacheza wakiwa na klabu mbalimbali.**

"Maandalizi yetu yanaendelea vizuri, hatuna ugeni katika ligi hii, ukiangalia wachezaji tuliowaongeza katika usajili wetu, wengi wao wanauzoefu na wanaweza kuhimili mikikimkiki ya ligi," alisema Fulgence.

Aliwataja wachezaji hao kuwa ni Mohamed Makaka na Baraka Mtui kutoka Ruvu Shooting, Aron Lulambo akitokea KMC, Lameck Daniel aliyesajiliwa kutoka Biashara United, Novartus Lufunga na Paul Nonga wote kutoka Lipuli na Said Mkangu kutoka Sahare All Stars ambayo imeshuka hadi Ligi Daraja la Pili licha ya kucheza michuano ya Kombe la FA na kufika robo fainali.

Wengine aliwataja kuwa ni Japhet Makarai kutoka Kagera Sugar, Moric Mahela na Miraji Saleh, hawa akieleza wamesajiliwa kutoka Stand United na Stali Nyambe kutoka Buildcon FC ya Zambia, timu ambayo alikuwa akiichezea Lamine Moro kabla ya kujiunga na Yanga.

Kocha huyo alisema maandalizi yao yanaendelea vizuri na kwamba licha ya kuwa na muda mfupi wa kutafuta kikosi cha kwanza, watahakikisha wanatumia mechi za ligi hiyo kupata timu yenye ushindani mkubwa.

"Hakuna Mwalimu ambaye atakosa kikosi chake cha kwanza, hivyo kwa kipindi kifupi cha maandalizi hatujaweza kupata ila baada ya michezo miwili nitapata muunganiko mzuri wa timu," alisema Fulgence.

Gwambina itashuka dimbani Jumapili kufungua pazia la Ligi Kuu dhidi ya wenyeji wao, Biashara United, katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Karume mjini Musoma.

WANANCHI...



Wachezaji wa Yanga wakiwa mazoezini jijini Dar es Salaam kujiandaa na Ligi Kuu Bara msimu mpya wa 2020/21. Yanga itafungua ligi hiyo dhidi ya Tanzania Prisons katika Uwanja wa Mkapa Jumapili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Katwila aahidi Mtibwa ya tofauti*

**Na Shufaa Lyimo**

USAJILI mzuri walioufanya msimu huu, unampa matumaini Kocha Mkuu wa Klabu ya Mtibwa Sugar, Zuberi Katwila, wa kufanya vizuri tofauti na ilivyokuwa msimu uliopita, ameeleza.

Mtibwa Sugar itaanzia nyumbani Jumapili kwa kuikaribisha Ruvu Shooting, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara, na tayari Katwila ameeleza kuwa na matumaini ya kufanya vizuri katika mchezo huo.

Akizungumza na gazeti hili jana kwa njia ya simu kutoka Morogoro, Katwila alisema msimu uliopita haukuwa mzuri kwa upande wao kutokana na kuvurunda kwenye ligi hiyo, lakini msimu huu wamejipanga vizuri.

"Msimu uliopita haukuwa mzuri kwa upande wetu, japokuwa tunashukuru hatujashuka daraja, lakini sasa tunarudi na nguvu mpya msimu huu ambao utaanza rasmi wikiendi ya wiki hii," alisema Katwila.

Alisema kikosi chake kitaonyesha mabadiliko makubwa msimu huu, kutokana na usajili mzuri wa wachezaji ambao wameufanya kwa kukiimarisha kikosi chake.

"Tumefanya usajili mzuri ambao utatusaidia kuboresha kikosi chetu na kushika nafasi ya juu msimu ujao," alisema.

Alisema kwa sasa wachezaji wanaendelea vizuri na mazoezi asubuhi na jioni lengo likiwa ni kuanza vizuri Jumapili.

Kuhusu morali ya wachezaji, Katwila alisema kila mmoja yupo vizuri na tayari kuelekea katika mchezo wao wa kwanza ambao utapigwa katika Uwanja wao wa nyumbani wa CCM Gairo.

"Kwa sasa bado sijaona ushindani wa namba katika kikosi changu mpaka ligi itakapokuwa imeanza, nitajua uwezo wa kila mchezaji naomba mashabiki wetu watulie wazidi kutupa ushirikiano," alisema.

Michezo

Ijumaa Septemba 4, 2020

Nipashe



Ramos amgeukia Messi abaki Barca UKURASA 22

# Sven: Hesabu zangu sasa kwa Ihefu si Kagere

●●● Ageukia mechi Jumapili akijivunia vipaji na morali, huku akieleza mengine ni…

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akishangazwa na uvumi unaoendelea kupitia mitandao ya kijamii na baadhi ya vyombo vya habari (si Nipashe), ukimhusisha kugombana na mshambuliaji wake, Mnyarwanda Middie Kagere, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Sven Vandenbroeck, amesema hesabu zake ni pointi tatu dhidi ya Ihefu FC Jumapili na si vinginevyo.

**Tangu Jumatatu kulizuka uvumi kuwa kocha huyo na Kagere wamegombana mazoezini na uongozi wa Simba kupitia kwa Meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alipokanusha kwa kueleza kwamba hawajafanya mazoezi siku hiyo, zilizuka taarifa zingine zikidai kuwa wawili hao waligombana wakiwa kwenye ndege wakati wakielekea Mbeya.**

Hata hivyo, Sven ameibuka na kueleza huo ni uvumi mtupu na kwamba hajagombana na mshambuliaji huyo na mahusiano yao ni mazuri kambini hadi mazoezini jijini Mbeya wakati huu wakijiandaa na mechi yao ya ufunguzi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Ihefu FC Jumapili.

"Mimi siwezi kutumia nguvu nyingi kwenye mambo yasiyo ya maana ambayo sijui yanatoka wapi. Mimi sina tatizo, Meddie hana tatizo, hilo ndilo ninaloweza kusema," alisema Sven.

Akionyesha kupuuzia uvumi huo, Sven aligeukia maandalizi yao kuelekea mechi dhidi ya Ihefu itakayopigwa Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine, na kueleza kuwa kila timu msimu huu imejiandaa vizuri na itahitaji pointi tatu, lakini anajivunia vipaji katika kikosi chake.

"Natambua mchezo utakuwa mgumu, lakini ninajivunia vipaji na morali kwa wachezaji wangu, ninaimani tutapigana kuweza kupata pointi tatu," alisema Mbelgiji huyo.

Alisema kikosi chake kinaendelea vizuri na maandalizi ya mechi hiyo tangu kiwasili jijini Mbeya Jumanne wiki hii na matarajio yao ni kuanza vizuri ligi hiyo.

"Jambo zuri ni kwamba hatuna majeruhi, kila mmoja yupo sawa, kila mmoja yupo tayari kucheza, hivyo nina nafasi ya kuchagua kati ya wachezaji wote niliona," alisema.

Simba imewasili jijini Mbeya ikiwa na kikosi cha nyota 25 tayari kwa mchezo huo ambao unatarajiwa kuwa mkali na wakuvutia kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu zote.

Ligi Kuu Bara inatarajiwa kuanza Jumapili ambapo mbali na mchezo huo wa Simba na Ihefu utakaoanza majira ya saa 10:00 alasiri, mechi nyingine zitakazopigwa siku hiyo itakuwa kati ya Yanga watakaoikaribisha Tanzania Prisons ya Mbeya kuanzia saa 1:00 usiku kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Mechi nyingine za Jumapili, Namungo FC watawakaribisha Coastal Union ya Tanga Uwanja wa Majaliwa, Ruangwa mkoani Lindi, Mtibwa Sugar wakiwakaribisha Ruvu Shooting Uwanja wa CCM Gairo mkoani Morogoro. Wageni wengine katika Ligi Kuu, Dodoma Jiji FC watawakaribisha Mwadui FC Uwanja wa Jamhuri jijini Dodoma huku Biashara United wakiwa wenyeji wa Gwambina FC waliopanda Ligi Kuu msimu huu katika Uwanja wa Karume, Musoma.

WANATUZUSHIA…



Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, akiwa mazoezini kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya na mshambuliaji wa timu hiyo, Middie Kagere. Kocha huyo amekanusha vikali taarifa zinazodai yeye na Kagere wamegombana. **PICHA: SIMBA**

## Yanga yamaliza kazi kwa Prisons

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema kikosi chao kiko kamili kuivaa Tanzania Prisons kwenye mechi ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, huku kikimkosa kiungo wake Balama Mapinduzi ambaye bado ni majeruhi.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Juma Mwambusi, alisema wanaendelea vizuri na maandalizi ya ligi, ikiwamo mechi yao dhidi ya Prisons huku akishirikiana vema na bosi wake, Zlatko Krmpotic kuhakikisha kikosi chao kinazidi kuimarika.

Alisema Mapinduzi ni mchezaji pekee ambaye bado hajaanza mazoezi kutokana na majeraha aliyoyapata msimu uliopita huku beki wao Lamine Moro, tayari ameanza mazoezi na huenda akawa miongoni mwa wachezaji watakaocheza siku ya Jumapili.

"Tuko vizuri maandalizi yanaendelea na tayari wachezaji wapo, kuhusu mfumo kocha mkuu anaweza kubadilika kulingana na mpinzani tunayekutana naye, hivyo kwa sasa tumekuwa tukiwafuatilia Prisons hasa mbinu na mfumo ambao anatumia kocha wao kwa akuangalia timu alizotoka," alisema Mwambusi.

Alisema wanahitaji kupata matokeo mazuri katika mchezo huo, licha ya kutowafahamu vizuri wapinzani wao, lakini wanapambana kufuatilia mbinu za kocha wa Prisons, Salum Mayanga ambaye amejiunga msimu huu kukinoa kikosi cha timu hiyo akitokea Ruvu Shooting.

"Maandalizi yanaendelea na ameridhishwa na viwango hasa kwa wachezaji wetu wapya na matumaini yetu makubwa ni kufanya vizuri katika michezo yote ili kufikia matarajio yanayotarajiwa na wanachama na mashabiki wa Yanga," alisema Mwambusi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >